

## **ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

### **MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

- |                                       |   |
|---------------------------------------|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali               | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.   |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa        | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.  |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma             | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.   |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi          | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.              |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.                   |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee              | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.   |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri               | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji       | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.                    |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed       | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.                     |
| 10. Mhe. Abubakar Khamis Bakary       | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.  |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman         | MBM/ Waziri wa Afya/ Jimbo la Ziwani.   |
| 12. Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban     | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.                           |
| 13. Mhe. Juma Duni Haji               | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.                                 |
| 14. Mhe. Zainab Omar Mohammed         | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.    |
| 15. Mhe. Abdillah Jihad Hassan        | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.  |
| 16. Mhe. Ali Juma Shamuhuna           | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.                                     |
| 17. Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya         | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.  |
| 18. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui          | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.                                   |
| 19. Mhe. Said Ali Mbarouk             | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.                           |
| 20. Mhe. Haroun Ali Suleiman          | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.            |
| 21. Mhe. Haji Faki Shaali             | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.                                  |
| 22. Mhe. Machano Othman Said          | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.                                     |

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi/Jimbo la Mpandae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni

53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

**Ndugu Yahya Khamis Hamad**

**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

## Kikao cha Sita – Tarehe 18 Machi, 2015

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

### Dua

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

### HATI ZA KWASILISHA MEZANI

**Kaimu Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, naomba kuweka mezani Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Wizara ya Afya kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yanayotokana na Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2013/2014.

**Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, naweka Hati mezani muhtasari wa Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

### MASWALI NA MAJIBU

#### Nam. 7

#### Mtaro wa Maji wa Kisima Majongoo

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Ublovu wa mtaro wa maji wa Kisima Majongoo umekuwa kero kwa muda mrefu na suala hili Wizara inayohusika inalifahamu kwa vile taarifa zilishaletwa hapa na majibu yakatolewa kuwa itaitishwa tenda ya kutafuta wataalamu wa kufanya matengenezo ya mtaro huo.

- (a) Je, Tenda hiyo imeshatangazwa.
- (b) Kama bado, ni lini tenda hiyo itatangazwa ili mtaro huo upate kujengwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni swali lake Nam. 7 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, ujenzi wa mtaro huu umejumuishwa katika ujenzi wa mitaro kuitia mradi wa *ZUSP* ambayo tenda yake imeshatangazwa na hivi karibuni atapatikana mjenzi.
- (b) Mhe. Spika, kama nilivyo sema katika jibu langu (a) kuwa ujenzi wa mtaro huu utajengwa pamoja na mitaro mengine ambayo ipo chini ya Mradi wa *ZUSP* wa Uendelezaji wa Huduma za Mijini ili kuwaondolea kero wananchi ambao wako karibu na mtaro huo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Pamoja na majibu ya rafiki yangu Mhe. Waziri ya kusikitisha na kama nafanya *reference* vizuri suala hili mwaka 2013 kikao cha Oktoba, tarehe 22 hili lilijibowiwa kwa rafiki yangu Mhe. Saleh

Nassor Juma, aliuliza na tenda hiyo ikaambiya imeshatangazwa. Sasa Mhe. Waziri nishike wapi mbele, nyuma. 2013 kauli nyengine, 2015 kauli hii, huku wananchi wanazidi kutekeseka na mtaro ule. Hilo la kwanza.

Serikali kuwa na kauli mbili inaleta picha gani kwa wananchi na utendaji unakuwepo wapi na tuangalie kipindi hiki cha masika tunachokwenda nacho, magari hayapiti, watoto wanacheza watakuja kukata miguu na matibabu hali hoi kama ilivyo Mnazi Mmoja.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwanza yeze aendelee kuangalia mbele tu sio nyuma, katu Serikali haiwezi kwenda nyuma na mbele. Serikali ikiamua kwenda inakwenda na ndivyo tunavyoendelea.

Mhe. Spika, utaratibu wa tenda unelewaka, kwa nini tunatangaza tenda, tunatangaza tenda kwa sababu ya kutaka kuwa na umakini wa kumpata mkandarasi ambaye atafanya kazi yetu vizuri. Ni kweli kabisa tenda hii iliwhi kutangazwa, lakini ikakosewa, ilibidi zaidi kutokana na masharti ya *World Bank* tenda hii irejewe na ndio maana imetangazwa tena upya na baada ya kutangazwa upya nimuombe Mhe. Mwakilishi asubiri, tusingekuwa na njia nyengine ya kuweza kulifanya jambo hili bila kupitia mradi huu wa *ZUSP*, si muda mrefu mkandarasi atapatikana ili aweze kuendelea na ujenzi wa mtaro huu.

## UTARATIBU

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Kifungu cha 37, yeze hana haja ya kusoma Mhe. Spika, swali (b) Mhe. Waziri kasahau kunijibu.

**Mhe. Spika:** Hebu kumbusha swali Mhe. Jaku.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Serikali kuwa na kauli mbili kunaleta picha gani kwa wananchi ambao ndio wanakabiliwa na tatizo hili, lini mradi huu utaanza kufanyiwa kazi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, nimesema nitajibu kwa pamoja na nimesema suala hili litafanyiwa kazi baada ya mradi wa *ZUSP* kuanza kazi kupitia kutangazwa kwa tenda ambayo mkandarasi atapatikana hivi karibuni. Hakuna jibu jengine zaidi ya hilo.

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza kama ambavyo majibu ya Mhe. Waziri amekwisha kutoa.

Mhe. Spika, pamoja na mtaro wa maji wa Kisimamajongoo ambao ni wa muda mrefu na tayari imepatikana na hiyo tenda nyengine na tupo katika kusubiri, lakini Mhe. Spika, Jimbo la Kikwajuni ni jimbo ambalo limekuwa ndio mamalizio ya mitaro mingi ambayo ipo katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Sasa tukiachilia mbali mtaro ambao upo Kisimamajongoo, kuna mtaro ule ambao umetokea Kwahani na *sin tank* kubwa sana ambayo ipo maeneo yale ya *high hill* kwa nyuma ambalo *sin tank* hili ni la muda mrefu nalo lina utata na tunaambiwa kila siku kesho, keshokutwa na keshokutwa tena inayoendelea, je, Mhe. Waziri ataliambia nini Baraza lako hili juu ya hii mitaro pamoja na *sin tank* makubwa ambayo yanatishia amani ha watoto wetu ambaowanacheza katika maeneo ya bahari.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, ningemuomba suala la *sin tank* liliopo katika eneo la Kilimani alipeleke kwenye Idara ya Nyumba na Makaaazi ndio wahusika wakuu wa suala hilo na sio Wizara yangu, aulize swali la msingi atapata jibu. Lakini mitaro mengine yoyote iliyopo katika jimbo lake itajumuishwa katika mradi huu mkubwa kupitia mradi wa *ZUSP* kuweza kujengwa upya na kuyapeleka maji kule ambako Serikali imekusudia yaende ikiwemo mitaro ya Jimbo lake la Kikwajuni; ukiwemo huo wa Kisimamajongoo na mitaro mengine yote kwa pamoja.

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa** - Aliuliza:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba inakabiliwa na changamoto za deni linalotokana na malimbikizo ya maposh ya likizo ya walimu 145 yenye thamani ya Tshs. 136,231,000/- (Milioni Mia Moja na Thelathini na Sita na Laki Mbili na Thelathini na Moja Elfu) na deni la fedha za walimu 159 ambazo zilikatwa kimakosa katika mishahara yao zenye thamani ya Tshs 18,487,900/- (Milioni Kumi na Nane Laki Nne na Themanini na Saba Elfu na Mia Tisa). Hata hivyo, fedha zilizokatwa katika mishahara ya walimu tayari imeshatolewa idhini ya malipo na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa barua ya tarehe 10/9/2012 kuwa malipo yafanyike kwa walimu hao, lakini taitizo linalojitokeza ni kuwa fedha za malipo hayo zimekwama katika Wizara ya Fedha – Unguja.

- (a) Je, ni lini walimu 159 waliopo Pemba ambaa fedha zao za mishahara zilizokatwa kimakosa watalipwa.
- (b) Je, kuna utaratibu gani uliopangwa ambaa utasaidia katika kupunguza deni la malimbikizo ya posho za likizo kwa walimu 145 waliopo Pemba.
- (c) Wizara ina mpango gani wa muda mrefu ambaa utapelekeea katika kunyanya maslahi ya walimu katika nchi yetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake namba 22 lenye kifungu

(a), (b) na (c), lakini kwanza naomba maelezo ya utangulizi kama hivi  
ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa, Wizara yangu inakabiliwa na madeni ya malimbikizo ya posho la likizo la walimu kwa Skuli za Unguja na Pemba. Madeni hayo yanatokana na uchache wa fedha zinazoingizwa ukilinganisha na idadi kubwa ya walimu na wafanyakazi wengine wanaohitaji kupatiwa huduma ya likizo. Kutokana na uhaba wa fedha, Wizara yangu imekuwa na utaratibu wa kutenga fedha kila mwezi ili kupunguza deni la likizo.

Pia, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Ofisi ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Pemba inakabiliwa na deni la malimbikizo ya posho la likizo la walimu 145 na deni la fedha za walimu 159 ambaa mishahara yao ilikatwa kimakosa wakati wa uhakiki wa sifa za wafanyakazi kutokana na kutowasilisha vyeti vyao. Pia, ni kweli kuwa fedha walizokatwa walimu zimeshatolewa idhini ya kulipwa kwa barua kutoka Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma ya tarehe 10/9/2012. Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

- (a) Walimu 159 ambaa fedha za mishahara yao zilikatwa kimakosa watalipwa mara baada ya kuingiziwa fedha hizo kutoka Wizara ya Fedha kama ilivyoidhinishwa na barua kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma, kwenda kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Uchumi.
- (b) Wizara yangu italipa madeni ya walimu ya likizo kila baada ya mwezi na kutenga fedha maalumu za kulipia huduma za likizo kila tunapoingiziwa fedha za matumizi mengineyo. Kwa mfano kuanzia mwezi wa Julai 2014 hadi Disemba 2014, Ofisi ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Pemba, imeingiziwa jumla ya Tshs. 198,000,000/= kwa matumizi mengineyo; katika fedha hizo jumla ya Tshs. 52,000,000/= sawa na asilimia 26.3 fedha hizi zimetumika kwa malipoya malimbikizo ya likizo za walimu na wafanyakazi wengine. Wizara yangu itaendelea kulipa madeni ya likizo kila mwezi kwa kadri ya fedha za matumizi mengineyo zitakavyopatikana.
- (c) Serikali imeandaa muundo wa utumishi wa walimu ambaa umezingatia sifa za kielimu na uzoefu wa walimu. Muundo huo wa utumishi utakapoanza kutumika utasaidia sana katika kunyanya maslahi ya walimu. Pia, katika vipindi mbali mbali Serikali imekuwa ikipandisha maslahi ya walimu. Hivi karibuni Serikali imefanya marekebisho ya mishahara ya walimu wenye sifa za cheti na utumishi wa kazi wa miaka 30 na zaidi Marekebisho hayo yatasaidia sana katika kunyanya maslahi ya walimu wenye uzoefu pia.

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nikawezza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Je, ni kiasi gani cha fedha za maposh ya walimu wote wa Zanzibar kinahitajika kila mwezi na je, fedha hizo zimejumuishwa katika bajeti ya Wizara 2014/2015.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu:** Mhe. Spika, idadi ya walimu na wafanyakazi wetu tulionao ni karibu 13,000. Kwa hivyo, tukigawa likizo hilo kwa sababu kila baada ya miezi mitatu wanatakiwa kwenda likizo si chini ya shilingi 430,000,000 ambazo zinatakiwa kwa mwaka. Pesa hizo tunazibajeti, lakini tatizo ambalo linatokea ni ule uingizishwaji wa pesa kwa kila mwezi ndio tatizo kubwa ambalo tunalo.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa walimu hawa amekiri Mhe. Naibu Waziri kwamba walikatwa fedha hizo za mishahara kimakosa. Na kwa kuwa muda sasa hivi umeshakuwa mrefu na walikatwa kimakosa.

Je, kuendelea kutowalipa haoni kama ni kuendelea kulimbikiza madeni na kuibebesha mzigo Serikali. Kwa hiyo, ni lini hasa wataona haja ya kuwalipa hasa ikizingatiwa kama hizi fedha zilikatwa kimakosa kuendelea kudai haoni kama ni kuwadhalilisha walimu hawa.

Na je, kwa kuwa suala la malimbikizo ya madeni ya likizo, likizo ni jambo la kawaida na kwa kuwa Serikali imeshapanga kama kila muda fulani walimu wanakwenda likizo. Je, haoni kama kuandaa mpango maalum wa kujua kama mwaka huu walimu watakaowenda likizo ni kadha na zikawekwa pesa zao wakalipwa bila ya kuachia kudai kwa sababu wanapokwenda likizo wana haja ya kutumia zile pesa zao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kama alivyosema na mimi nilisema kwenye jibu langu mama kama pesa hizi zilikatwa kimakosa kutoptana na wao wenyewe walimu kuchelewesha kupeleka vyeti vyao vya uhalisia katika masomo yao.

Lakini pia tujue Serikali kwamba kuna wizara ambazo zinategemea na ndio maana niliposema hapa kwamba sisi kama Wizara ya Elimu baada ya kupata malalamiko hayo kutoptana na walimu wetu na wafanyakazi wetu tuliwaandikia utumishi kudai madai haya na utumishi nao walichukua nafasi yao kwa kuwaandikia Wizara ya Fedha barua tokea tarehe 10/09/2012. Tunachosubiri ni Wizara ya Fedha sasa *ku-respond* yale madai ambayo tulidai na Wizara ya Utumishi ambayo iliidhinisha, ndicho hicho ambacho Wizara ya Elimu tunakisubiri.

Na kama ambavyo nilizungumza mwanzoni kama hizi pesa tunazi-*budget* kwa kila mwaka tunajua ni walimu wetu wangapi ambao wanataka kwenda likizo. Lakini nilisema kama mzigo wa likizo kwa walimu wetu ni mkubwa kwa sababu takriban tunabebea nusu ya wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tuna walimu karibu elfu kumi na tatu, tunahitaji milioni mia nne na thalathini kwa mwaka ili walimu wetu wote waweze kwenda likizo.

Na takriban walimu wetu wana kawaida ya kwenda likizo kwa mwezi wa Disemba. Sasa hizi pesa ambazo tunaingiziwa, tunaingiziwa kidogo kidogo, ndio tatizo ambalo tunalo.

**Mhe. Salum Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kupata kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizopo kwa hizi shilingi milioni mia moja na thalathini na sita na hizi kumi na nane ni jumla ya shilingi milioni mia moja na hamsini na nne na ushei wizara imekuwa ikidaiwa na walimu hawa katika mambo haya mawili.

Na kwa sababu barua iliyotoka kwa kulipwa hawa wanaodai milioni kumi na nane ni tokea tarehe 10/09/2012 ni muda mrefu sasa. Na kwa sababu Mhe. Naibu Waziri kaeleza kuwa anatarajia kuendelea kuwalipa baada ya kupata OC kutoka serikalini na wakati muda hamna tena keshokutwa ni June mwaka umemaliza.

Mhe. Spika, masuala yangu yapo hapa. La kwanza, hili deni la shilingi milioni mia moja na thalathini na sita, laki mbili na thalathini na moja elfu ni la tokea muda gani na hili deni la shilingi kumi na nane milioni laki nne na thamanini na saba na mia tisa ni la muda gani. Na kwa sababu deni hili lishachukua muda mrefu na Mhe. Naibu Waziri anasema kuwa yeye ana wafanyakazi wengi na wakati tunavyojua ni kwamba shule zinaongezeka, wanafunzi wanaongezeka na walimu wataongezeka.

Hivyo, ni sawa na kusema kuwa wizara yake ndivyo itakavyokuwa katika mtindo huu wa kuwawekea watu madeni kutokana na kuwa walimu ni wengi na fedha anazozipata ni kidogo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, idadi ya fedha ambazo amezitaja za deni ambalo tunadaiwa, hiyo si idadi halisi ya deni ambalo tunaidawa, hiyo ni idadi ya wanaodai. Nilisema posho ni mia moja na arubaini na tisa na wale ambaao wana malimbikizo ni mia moja na hamsini na tisa, idadi ya watu. Lakini lile alilosema kama mwaka umemalizika bado Mheshimiwa tuna robo ya mwisho na kwa sababu madai tayari yapo Wizara ya Fedha, naamini Wizara ya Fedha na Serikali haina nia ya kumdhulumu mtu, hizi pesa ni haki yao, kwa hivyo, watazipata kabla ya mwaka huu kumalizika. (*Makofî*)

### Nam. 37

#### **Matumaini ya Wananchi Katika Mabadiliko ya Baraza la Mawaziri**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-**

Mnamo tarehe 24/8/2014, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Ali Mohamed Shein, alifanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri ambapo mionganoni mwa Wizara zilizoguswa ni Wizara ya Afya ambayo kama ziliyyo Wizara nyengine ni Wizara muhimu inayogusa ustawi wa jamii.

- a. Je, kutokana na mabadiliko hayo wananchi wawe na matarajio gani ya kupata huduma bora za afya, kwa vile muda mrefu kumekuwa na malalamiko ya kutopatikana kwa baadhi ya huduma muhimu za afya kwa muda muafaka.
- b. Serikali inategemea mabadiliko haya yatachukuwa muda gani kuleta mafanikio na tija iliyokusudiwa kwa wananchi kupata huduma bora za afya.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-**

Mhe. Spika, ahsante sana kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia wote tuliokuwepo hapa katika Baraza lako tukufu katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar tukiwa na afya njema na uzima.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 37 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa ni kweli Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein alifanya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri mnamo tarehe 24 Augosti, 2014. Na kwa upande wa Wizara ya Afya alifanya mabadiliko ya Waziri na Naibu Waziri wa Afya na baadae kuteuliwa Naibu Katibu Mkuu mpya katika Wizara hii ya Afya na kwa mara ya kwanza kabisa nafasi hiyo mpya ya Naibu Katibu Mkuu imeshikiliwa na mwanamke aliye makini na mahiri sana. (*Makofî*)

- a) Mhe. Spika, mabadiliko yaliyofanywa na Mhe. Rais ni ya kawaida kwa nafasi za kisisasa na nafasi za kiutendaji kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa Mhe. Rais. Hivyo, wateuliwa wapya (Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri na Naibu Katibu Mkuu) wao ni wajibu wao kuendeleza na kutekeleza Sera ya Afya kama ilivyo katika Dira ya Serikali ya mwaka 2020 pamoja na MKUZA, pamoja na Malengo ya Maendeleo ya Millennium (*Millennium Development Goals*) na wananchi wa Zanzibar wategemee kupata huduma bora za afya kila kukicha.
- b) Mhe. Spika, mabadiliko haya tayari yameshazaa matunda kwa kujenga mahusiano mazuri zaidi baina ya uongozi uliopita wa Wizara ya Afya na uongozi uliopo hivi sasa. Pia, kujenga mashirikiano ya karibu zaidi ya kimaendeleo kati ya watendaji wa Wizara ya Afya, madaktari, wauguzi, wanaafya ya jamii, wataalamu wa lishe na kada nyengine zote za kinga na tiba ndani ya Wizara ya Afya, kwa mashirikiano hayo ya karibu

na kwa kuongeza huduma mbali mbali mpya za afya ambapo hapa awali hazikuwepo hapa Zanzibar ambapo ilibidi Serikali kutumia ghamara kubwa kuwahudumia wananchi wake kwa kuwapeleka nje ya Zanzibar kwenda nchini India kupata huduma hizo.

Tunapenda kutamka wazi kuwa sasa tayari tumeshapunguza takriban asilimia 30 ya wale wote waliokuwa wakikosa huduma hizo hapa awali na sasa wanapatiwa huduma hizo hapa hapa Zanzibar.

Hii ni kwenda hatua kwa hatua hadi kufikia malengo tuliojiwekewa. Inamaanisha kuwa asilimia 30 ya ghamara zote kubwa zilizokuwa zikitumika kuwasafirisha wananchi wa Zanzibar kwenda nje ya nchi sasa zitakuwa zimepungua na kupelekeea kupunguza matumizi makubwa yaliyokuwa yaktumika hapa awali kwa kuwasafirisha wagonjwa nje ya Zanzibar.

Tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi mahiri na makini wa Dkt. Ali Mohammed Shein imeshapitiliza malengo yake katika huduma za afya kwa miaka mitano ya ridhaa ya wananchi waliompa Dkt. Ali Mohammed Shein, hili na tunaomba waendelee kutarajia kila hatua tunazopiga basi mafanikio zaidi yatapatikana. Mhe. Spika, nashukuru sana.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kusema hii wizara yake au watendaji wake imeshazaa matunda, lakini na mimi mvua hizi naomba ayajaalie yapate kupea vizuri, lakini ni matunda kweli na naona kama hayajapea bado matunda hayo alivyokuwa akijibu swali la msingi. Lakini mvua hizi Mwenyezi Mungu atajaalia yazidi kupea.

Ni lini wananchi watapata huduma muhimu kama za matibabu ya mifupa na kensa ili kupunguza idadi, yaani bado watu wanakwenda Tanzania Bara kwenda kutafuta vipimo, ni lini mtaanza kupunguza idadi hii kupatikana vipimo ikiwemo vya mifupa, kensa na lini mtaweka daktri masaa 24 pale wa kitengo cha mifupa baada ya wananchi kupata usumbufu wa hali ya juu, ingawa vifaa hivyo huwenda wakanunu wenyeve ili kupata huduma hiyo ya matibabu. Lakini ukienda kununua vifaa daktari hayupo, ni lini mtaweka daktari masaa 24 wa kitengo cha mifupa. Hilo la kwanza.

Na lini ikiwa wewe na Waziri wako na Katibu wako Mkuu na huyo Naibu Katibu Mkuu aliyeteuwa juzi ulosema yuko makini mtafuatana na mimi kwenda kukuonesheni sehemu ambazo hazihitaji bajeti, kutohana na usimamizi wenu mbovu wa Wizara ya Afya. Ni lini mtafuatana na mimi kwenda kukuonesheni mambo mengine hayahitaji bajeti ikiwemo huduma ya taa, kusafishwa vyoo, hali ya *jik* haihitaji bajeti, *gloves* hazihitaji bajeti, ni lini mtakuwa tayari kufuatana na mimi Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu uliosema yuko makini.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, maswali yake nitayaanza kwa mtiririko wa kuanzia chini kuja juu.

Mhe. Spika, naomba nilieleze Baraza lako tukufu mara nyingi Mhe. Mwakilishi amekuwa akizungumza hapa anafurahisha hili Baraza na kuwfurahisha wananchi, hasa pale anaposema kuwa atafuatana au lini tuko tayari kufuatana nae. Hili si mara ya kwanza kusema ameshasema zaidi ya mara tano ni lini tutakwenda ameshatwambia tujiuzulu hapa na wakati mamlaka iliyotuweka sisi ni Mhe. Rais akiamua kutuondosha atatuondosha wakati wowote ule.

Mhe. Spika, akishasema hivyo hapatikani, sisi tunamwambia leo tuko tayari kwenda; mimi Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, lakini ye ye Mhe. Mwakilishi akishasema hayo huwa hapatikani. Ana tabia na mwenendo wa kufurahisha Baraza hili na wananchi wa Zanzibar, nasema tena mbele yako Mhe. Spika na Baraza hili leo sisi tuko tayari apatikane ye ye twende akatuuneshe hivyo vitu. La kwanza hilo. (*Makofit*)

Mhe. Spika, najua hili Baraza lako ndio linalotunga sheria, linalosimamia Serikali katika utendaji wake, linalosimamia matumizi yote ya Serikali. Kwa hiyo, mtu akiwa anazungumza humu ndani natarajia na atasimamia kauli zake kuwa thabiti pia hivyo hivyo.

La pili, Mhe. Spika hivi sasa kweli kuna upungufu wa daktari wa mifupa (*orthopedic surgeon*) tunae mmoja wa hapa nchini na mmoja ambaye tumepata kutoka nje kama msaada unatusaidia yuko pale katika kitengo cha mifupa. Hivi sasa pia tunachukua jitihada ya vijana wawili ambao wamepelekwa nje kwenda kusoma masuala ya *orthopedic surgery*, watakaporudi tu wataungana nao ili kuweza kufanya kazi nao pamoja.

Lakini pia Mhe. Rais wa Zanzibar siku akitoa vyeti kwa madaktari wetu waliohitimu 38 wa Cuba waliosoma *University of Matanzas* ile *degree* inayotolewa na ile *University* ambayo tunashirikiana nayo ya Cuba hapa katika Chuo cha Afya Mbweni alitutaka vijana hao wapelekwe kwenda kuwasomesha masuala ya *specialization*, yaani taaluma maalum ya kuweza kupata fani mbali mbali.

Katika kauli yake hiyo alitutaka sisi na alitupa agizo ya kwamba taaluma ya *oncology*. Mhe. Mwakilishi, *oncology* ni *field* ya kensa yaani matibabu ya kensa yanaitwa *oncology* katika *field* ya *oncology* na *field orthopedic surgery*. Kwa hiyo, tumo katika jitihada tumeshazungumza na vyuo vikuu vitatu nje pamoja na *Oakland University* ya Norway ambayo wakati wowote taratibu zikikamilika tutapeleka wanafunzi hao kwenda kupata taaluma zaidi.

Lakini hapo hapo katika masuala ya kensa tayari tuna mkataba mzuri ambao tunashirikiana na wenzetu wa *ORCI*, *ORCI* ni kile kitengo cha kensa cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilicho pale pale *Ocean Road*, wao tuna mkataba nao wanatusaidia na wale wagonjwa wote wanaokwenda pale huwa tunawalipia huduma za usafiri na huduma zote nyenginezo kwenda kupata matitabu.

Matibabu ya kensa sio rahisi hata nchi zilizokuwa zimeendelea zinatumia fedha nyingi sana na kwa hapa Tanzania uwekezaji wa Serikali mpaka sasa hivi mkubwa kabisa umefanyika pale *Ocean Road, Ocean Road Cancer Institute Research (ORCI)*. Kwa hiyo, wao ndio waliokuwa *appointed* yaani ni kitengo ama Idara Maalum na rasmi ambayo inahudumia wagonjwa wote wa saratani za aina mbali mbali na huwa wanatuletea sisi ripoti kila baada ya muda kuwa wagonjwa wangapi kutoka Zanzibar wamefika huko.

Naomba nimalizie hapo Mhe. Spika, na naomba niseme kwamba matunda yatapea na yatakuwa mabivu na tutaendelea kufaidika.

Mhe. Spika. ahsante sana.

## UTARATIBU

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, kifungu cha 37, waziri au mjumbe yeoyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi, kwa ufupi isipokuwa kwamba swali aliloulizwa waziri mmoja linaweza kujibiwa na waziri mwengine na Mwanasheria.

Mhe. Naibu Waziri, nataka uuthibitishie umma huo uliokuwepo hapa, lini ulonipangia safari nikakiuka safari yako, naomba uthibitishe hapa ndani. Hiki ni chombo cha wananchi sio cha masihara, mimi uteuzi wangu haukutoka Ikulu wala viti maalum, nimekuja kwa niaba ya wananchi na hoja yangu ya msingi ya wananchi, nthibitishie lini umenipangia safari na nikakataa safari na uniambie leo niko tayari wakati wowote mimi niko tayari, twende mguu kwa mguu.

**Mhe. Spika:** Sitaki tufungue boksi la malumbano hapa ila anachosema Mhe. Waziri leo hii muende huko ulikotaka muende ili kufuatilia hayo masuala uliyohitaji, boksi la malumbano hapa hairuhusiki. (*Makofii*)

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri anayoyajibu Mhe. Naibu Waziri, lakini kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim, tunategemea mabadiliko baada ya wizara hii kubadilishwa.

Sasa namuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipojengwa ilikuwa inahudumia wananchi laki tatu tu kwa Zanzibar na kwa kuwa *population* ya watu imeongezeka sasa hivi tuko watu 1,300,000 (milioni moja na laki tatu) na kwa kuwa hospitali ile sasa hivi imezidiwa na wananchi wa Zanzibar na kwa kuwa

tunahitaji mabadiliko ni lini Wizara ya Afya itaona umuhimu wa kujenga hospitali nyengine zaidi ya rufaa ili kuisaidia mzigo Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo imezidiwa sasa hivi na wananchi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, nakishukuru sana kiti chako lakini ningependa kuendelea kujibu zaidi, lakini naheshimu sana kiti chako.

Mhe. Spika, naomba nimfahamishe Mhe. Subeit Khamis pamoja na Baraza lako tukufu kuwa hivi sasa kuna miradi mikubwa mitatu ya kujenga Hospitali za Wilaya. Tunakwenda mbio sana tukishirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha, tunawashukuru sana Mhe. Waziri na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ambao wanatupa moyo pamoja na msaada mkubwa sana katika hii miradi mitatu, ambapo mmoja tunazungumza na Serikali ya Watu wa China, pili, tunazungumza na Serikali ya Norway katika Hospitali hizo za Wilaya.

Ningelijua tutakuwa na suala hili ningekuja na ramani zote zile kubwa hapa Waheshimiwa Wawakilishi mkapata kuyaona, lakini bado tuko katika hatua za awali. Moja ya hospitali hizo ni Binguni ambayo inatarajija kujengwa mara tu taratibu zote zitakapokamilika na itakuwa ni hospitali ya aina yake. Kwa sababu tunatarajia wakati huo watu kutoka Bara watakuwa wanakuwa hapa badala ya hapa kwenda Bara.

Mhe. Spika, pili, ni ile ya Abdala Mzee. Hospitali ya Abdalla Mzee itakuwa ngazi ya hospitali ya wilaya au pia naweza kusema ni hospitali ngazi ya rufaa kwa kule Pemba. Kwa sababu bahati nzuri tunamshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein baada ya kututeuwa tu alinipeleka mimi mwenyewe nchini China ili nikajifunze, nikajue na kutambua; ile kampuni inayojenga inaitwa *JCB* ambao wanajenga Hospitali ya Abdalla Mzee.

Tulipofika kule sisi hatukujua kwamba hospitali ile baada ya kuijenga wataitia na vifaa vya kila aina. Naomba niseme Mhe. Spika, mbele ya Baraza lako tukufu kwamba hospitali ile itakuwa na uwezo wa kushindana na Mnazi Mmoja na huenda kwa vifaa vitakavyokuwepo pale na *list* nzima tuliyopewa huenda watu wengine wakatoka Unguja kwenda kutibiwa Pemba.

Mhe. Spika. ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Nafikiri hili swali limechukua muda mrefu kidogo, Mhe. Waziri nyongeza ya majibu.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, pamoja na kauli yako naheshimu sana kwamba limechukua muda mrefu, nina maneno mawili matatu tu ya kuongezea kidogo. La mwanzo ambalo nilitaka kuongezea ni mabadiliko yaliyotokea. Mabadiliko yaliyotokea si ya kiutendaji kama ambavyo liliulizwa swali, itakumbukwa kwamba mimi mwenyewe nilikuwa ni waziri, kwa hivyo, nimeletwa katika wizara nyengine tu. Lakini kubwa zaidi ni aliyekuwa Naibu Waziri wa Afya yeche kapandishwa cheo kawa waziri mzima wa Kilimo na Maliasili.

Kwa hivyo, halikuwa suala la kiutendaji kwa waliopita ila lilikuwa ni suala la mabadiliko ya kawaida. Hivyo, kusiwe na fikra kwamba mabadiliko yaliyotokezea yalikuwa ni ya kiutendaji. Kama ni hivyo basi, mambo yangekuwa mengineyo, angepoteza mtu unga au mwengine akala mchanga. (*Makofî*)

La pili, ambalo nataka kusisitiza ni kwamba programu ya kuiendeleza Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kubwa na pia kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba, kwa sababu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ina mipaka yake ya kuiendeleza kutokana na nafasi ya ardhi iliyopo. Serikali iko mbioni katika kuendeleza hospitali nyengine ya rufaa, ambapo eneo limeshapimwa na liko tayari kwa ajili ya kujengwa hospitali huko eneo la Binguni. Kwa hivyo, wasiwasi huo kweli ni sahihi kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja inahitaji kupokewa. Lakini hata hivyo, bado inaendelea kutoa huduma.

Mhe. Spika. ahsante sana.

**Nam. 60**

**Ujenzi wa Barabara ya Mgagadu - Kiwani**

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:-**

Barabara ya Mgagadu-Kiwani tokea kufanyiwa “grading” huu haupungui mwaka wa sita, wizara inatoa maelezo gani ya kina kuhusiana na barabara hiyo na lini ujenzi wake utamalizika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 60 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli barabara ya Mgagadu-Kiwani ni mradi wa ujenzi unaotekelizwa kuitia fedha za Bajeti za Maendeleo na kazi za ujenzi kwa kufanyiwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara. Ujenzi wa barabara hii hutegemea upatikanaji wa fedha kutokana na fedha zilizotengwa katika bajeti ya wizara.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya, kwa miaka miwili iliyopita mradi huu umekosa fedha za kuuendeleza na hivyo utekelezaji wake kuwa si wakuridhisha. Kabla ya ujenzi huo kusita kutokana na ukosefu wa fedha, barabara hiyo tayari ilikuwa imewekwa kifusi cha tabaka la pili.

Mhe. Spika, wakati jitihada za kupata fedha ili tuweze kukamilisha barabara hiyo zinafanyika, wizara imeamua kujenga daraja (*kalvati*), kwa kuitia fedha za Mfuko wa Barabara katika eneo la Kiwani/Mbaoni ili barabara hiyo iweze kutumika kwa kipindi cha mwaka mzima.

Aidha, kupitia fedha za Mfuko wa Barabara, wizara inatarajia kufanya marekebisho barabara sehemu zote za vilima ambapo kifusi kimeanza kuchukuliwa na maji.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kuna vijiji ambavyo hadi leo bado vinahangaika na huduma ya barabara kama vile Jaani, Mtambile; Mitatuni, Kidatuni na hadi Sipwese. Ni lini Serikali itatatua kilio cha wananchi hawa angalau kupata barabara kwa kiwango cha fusi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, madhumuni ya Serikali ni kuona maeneo yote tunapeleka huduma, kinachotukwaza ni uwezo. Suala la msingi lilikuwa linaluzia barabara ya Mgagadu-Kiwani, tumeleeza kwamba hii tumekwama kwa sababu ya fedha hatuna za kutosha kwa ajili ya kumaliza mradi. Sasa Mhe. Mwakilishi anapokuja na maeneo mengine kuulizia kwamba barabara tutajenga lini, maana yake tutarudi palepale, aache tumalize haya ambayo tumeanza, tukimaliza haya tutatafuta mengine sasa ya kufanya. Madhumuni ya Serikali kujenga barabara kwa maeneo yote ya Unguja na Pemba.

**Mhe. Nassor Salum Ali:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini katika majibu yake amesema kwamba, wizara imeweza kukosa fedha na vile vile inafanya marekebisho katika sehemu za vilima kwa kuweka kifusi. Lakini kutokana na hali ya mvua ya kila mwaka. Je, wizara haioni kuweka kifusi kwa kila mwaka badala ya kuweka miundombinu ya kisasa ni kuendelea kupoteza fedha za wananchi walipa kodi wa nchi hii.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, malengo ni kujenga barabara za lami kwa maeneo yote, lakini kutokana na ukosefu wa fedha tunalazimika baadhi ya nyakati kufanya marekebisho maalum na kwa barabara hii tumeona kwamba kuna usumbufu hasa maeneo ya kwenye vilima. Inapokuwa kifusi kimeondoshwa na maji barabarani katika maeneo ya vilima inakuwa haipitiki. Kwa hivyo, wajibu wetu kuona kwamba eneo lile ambalo limechimbika kwa maji kwanza turejeshe kifusi na kama tutapata fedha kidogo kutoka Mfuko wa Barabara basi tunaona ipo haja ya kuweka lami angalau katika yale maeneo ya kilima, ili tuweze kunusuru fedha za wananchi. Lakini pia kuweza kufanya usalama mzuri zaidi kwa ajili ya watumiaji wa barabara husika.

Kwa hiyo, nimthibitishie tu Mhe. Mwakilishi kwamba hatuna dhamira ya kupoteza fedha, isipokuwa kile kidogo tulichokuanacho tunaona kwamba ipo haja na sababu za msingi za kuona tunasaidia wananchi wetu kuweza kupata huduma ya barabara hata kwa kiwango cha kifusi.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Spika, ahsante sana, mimi nitauliza swali dogo la mwisho la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, barabara hii ya Mgagadu-Kiwani imekuwa ni kama barabara ya hadithi ya paukwa pakawa.

Mheshimiwa, barabara hii takriban miaka sita au saba iliyopita kila mara inaingizwa katika bajeti na inajengwa wala haimaliziki. Pale wanapojenga wakiacha mnachimbuka mabata wanapata maziwa ya kuogelea. Je, Serikali hasa ni lini barabara hii watakamilisha ili kuacha kupoteza pesa za wananchi kila mwaka.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kusema kwamba Serikali lini tutakamilisha hatuna kauli na hatuna kauli kwa sababu jithada kubwa ya Serikali ni kuipanga kwamba barabara hii ijengwe. Jambo hilo kama wizara tumelifanya, tumeingiza katika bajeti ya Serikali, tumeingiza katika bajeti ya wizara yetu, lakini tatizo ni ukosefu wa fedha. Sasa ukisema kwamba lini tutaijenga hatuna kauli hiyo, tutakapopata fedha zitakazotosha tutaijenga barabara hiyo.

### Nam. 53

#### Ziara za Nje ya Nchi kwa Viongozi wa Wizara

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-**

Viongozi wa Serikali wakiwemo mawaziri wamekuwa na safari nyingi nje ya nchi zikiwemo za mafunzo na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ikionekana kuchukua nafasi kubwa kwa waziri wake. Hivi karibuni waziri katika kipindi cha mwezi mmoja amekwenda safari karibu mbili ikiwemo China na Uhlanzi.

- a) Safari hizo zimeleta tija gani kwa Zanzibar na wananchi wake.
- b) Kwa kuwa lengo kubwa la safari hizo ni kuona uwajibikaji na ufanisi wa kazi unapatikana kwa idara na taasisi zetu, kwa nini bado kuna malalamiko ya wananchi kutopata huduma kwa wakati muafaka kutoka wizara hii.
- c) Kuna sababu gani ya ziara za nje kwa viongozi wa wizara kuendelea kufanyika na kutumia kiwango kikubwa cha fedha wakati tija na malengo yake hayaonekani kutokana na taasisi na idara zake kuendelea kufanya kazi kwa mazoea.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-**

Mhe. Spika, ahsante naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 53 lenye kifungu (a), (b) na ( c ) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli Mhe. Waziri alisafiri kwenda nchini China, safari hiyo alisafiri akiambatana na ujumbe wa Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Idd, ambapo ulikwenda China kwa nia ya kuimarisha mahusiano ya Tanzania hususan Zanzibar katika ujenzi wa uchumi kwenye maeneo ya utalii.

Mhe. Spika, kwa upande wa safari ya Uhlanzi Mhe. Waziri alisafiri kwenda nchini Uhlanzi akiwa kama ni Mwenyekiti wa Kamati ya *Steering Committee* inayo ratibu makubaliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya *SHELL*. Ni safari ya siku tatu kuanzia tarehe 11/12/2014 na kikao kilifanyika tarehe 12/12/2014 na tarehe 13/12/2014. Mhe. Waziri alirudi safari hiyo na gharama za safari hiyo imegharimiwa na Kampuni ya *SHELL* na faida ya safari hiyo si muda mrefu itaonekana.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, lakini sikukusudia waziri huyu tu, ziara nyingi za mawaziri zinakuwa zinahusu maslahi ya wananchi. Lakini nilikuwa nataka utaratibu mawaziri wanapokuwa wakisafiri hawaelezi safari zao maslahi yanayohusu wananchi.

Pili, ni lini watendaji wakiwemo Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuiu na Wakurugenzi watakaa na waandishi wa habari kuwaeleza safari zao kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na faida inayopatikana katika safari hizo na zinazaa matunda ya aina gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, viongozi wa Serikali akiwemo Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein, Maalim Seif Sharif Hamad, pia na Makamu wa Pili wa Rais, wanapokwenda safari zote za nje basi wanafanya utaratibu wa kuonana na waandishi wa habari kuwaelezea kila kitu ambacho

wamekipata katika safari hiyo. Kwa hiyo, nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba hata mawaziri watafanya utaratibu huo wa kukaa na waandishi wa habari na kuwaelezea hali halisi ya safari zao.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, mara nyingi sana tunapoulizwa maswali tunakuwa hatujibu yale maswali ambayo tumeulizwa, swalii lililojitekeza hapa kuwa mawaziri wanapokwenda nje wanakuwa na wao hawafanyi ile *conference* ya *media* ya kueleza jinsi ilivyokwenda. Huko mimi nimeona nieleze kidogo na sasa niende katik swali.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, mara nyingi sana hasa viongozi wakuu Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili na hata Rais na Mhe. Spika, wakienda safari, ni sababu zipi zinawafanya wasichukuliwe angalau Waheshimiwa wawili watatu wa Baraza hili tukufu na wao wakaweza kutoa ufasha wa ile safari.

Pili, ni lini ambapo katika safari ambayo Mhe. Waziri alikwenda nje, tatizo ni lipi lililopelekea Mhe. Waziri akenda safari hiyo. (*Makofii*)

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa heshima yako naomba kuongezea majibu ya ziada.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Mawaziri wanaposafiri kwenda nje wanakwenda kwa madhumuni maalum na wanaporejea wanatakiwa kumuandikia Mhe. Rais ripoti au taarifa ya ziara zao, mafaniko na matokeo yote yanakuwemo katika ile ripoti ambayo wanamuwasilishia Mhe. Rais.

Vile vile, kwa upande wa Makatibu Wakuu nao wanatakiwa kumuandikia Katibu Mkuu Kiongozi ripoti juu ya taarifa na matokeo yote pamoja na mafaniko ya ziara zao. Lakini vile vile, haimzuii waziri ye yole kuita waandishi wa habari kutoa maelezo kwa mujibu wa sekta yake au kwa mujibu wa ile ziara mafanikio yaliyopatikana, ili wananchi waweze kufahamu hivyo. Kwa hivyo, hayo yanafanyika lakini baadhi ya wakati yanafanyika kwa kupitia sekta zao sio baada ya zile ziara.

Mhe. Spika, nikijibu swalii la Mhe. Makame Mshimba, nadhani wapo hawa Waheshimiwa Mawaziri wameshawahi kwenda na wakawachukuwa Waheshimiwa Wawakilishi. Mhe. Haroun Ali, ameshawahi kwenda safari na akawachukuwa Waheshimiwa Wawakilishi, mimi mwenyewe nimeshakwenda safari si moja mbili nimeshawachukuwa Waheshimiwa Wawakilishi na wengine. Lakini inategemea na hali yetu ya bajeti ilivyo.

Lakini kama Baraza la Wawakilishi litakuwa na fedha za kutosha, hakuna waziri atakaekataa kumchukuwa Mwakilishi kupitia vifungu vya Baraza la Wawakilishi. Sisi tuko tayari kwenda nao lakini kupitia bajeti za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti. ahsante. (*Makofii*)

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, wakati Mhe. Waziri alipokuwa akijibu jawabu mama alisema kwamba faida za safari alizokwenda Mhe. Waziri karibu zitaonekana. Mimi suala langu lilikuwa dogo tu.

Mhe. Spika, kabla ya kuziona hizo faida ambazo kasema karibu zitaonekana ningeomba basi atueleze lengo la dhamira safari hiyo zilikuwa ni nini na hizo faida zenyewe tunazotarajia kuziona ni faida gani.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, wakati Mhe. Naibu Waziri anajibu suala hilo, alijibu kwa mujibu wa suala mama lilolulizwa nchi mbili, muulizaji aliuliza Uhlanzi na akauliza na China.

Kwa upande wa Uhlanzi alisema kwamba Mhe. Waziri ni Mwenyekiti wa ile Kamati ya pamoja ya *SHELL* na mimi ni msaidizi wa Mhe. Mwenyekiti wa Mhe. Waziri ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ile. Kwa sababu Mhe Waziri hayupo naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Kamati ile ya pamoja baina ya Serikali na Kampuni ya *SHELL* ni Kamati ambayo tunajadili mpango mzima wa utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na ndio maana Mhe. Naibu Waziri alopojibu akasema kwamba

matunda yatakuja kuonekana baadae kwa maana kwamba hii Kamati kazi yake itakuja kuona pale ambapo tutakapoanza kuja kuchimba mafuta na gesi asilia.

Mhe. Spika, kama unavyoolewa uchimbaji wa gesi asilia na mafuta kwetu sisi ni zoezi jipya sana, kwa hiyo, tunafanya kila tunaloliweza tuweze kufahamu tunakwendaje katika masuala ya uchimbaji katika masuala ya kodii katika masuala ya ugawanaji wa ile rasilimali tutafanya vipi, hayo yote tunajadiliana na wenzetu wa *SHELL* na sio *SHELL* tu kuna Kamati vile vile ya Rasilhema, Mwenyekiti wake ni Mhe. Haroun Suleiman, Wajumbe wake kina Mhe. Haji Omar Kheir, Mhe. Mohammed Mazrui na mimi mwenyewe ni Mjumbe vile vile.

Mhe. Spika, hizi Kamati zinafanya kazi tunaagalia jinsi gani tutakavyokwenda na wenzetu katika suala zima la Sekta ya Mafuta. Ndio kwa maana Mhe. Naibu Waziri akasema kwamba matunda tutakuja kuyaona pale tutakapochimba mafuta, sisi tutakuwa tuko tayari tuna *knowledge* kwamba nini cha kufanya katika mafuta yetu. Mhe. Spika. ahsante.

**Mhe. Spika:** Nawashukuru Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri wa Kazi. Tunaendelea.

#### Nam. 72

#### **Vyoo vilivyopo Uwanja wa Amani Kugeuzwa Afisi**

**Mhe. Ali Salum Haji:-** Aliuliza :-

Kwa kuwa Serikali ilitumia fedha nyingi pamoja na wafadhili kuufanyia matengenezo Uwanja wa Amani na kuweka Ofisi za Huduma mbali mbali ikiwemo vyoo vya kisasa.

Je, ni sababu gani iliyopelekea choo kugeuzwa Ofisi ya *ZFA* Wilaya.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 72 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Uwanja wa Amaan ulifanyika matengenezo makubwa ya kuweka Ofisi za huduma mbali mbali za Ofisi pamoja na kujengwa vyoo vipyaa ndani ya eneo la uwanja huo.

Mhe. Spika, katika ujenzi wa vyoo vipyaa, kulijengwa majengo mawili moja mbele ya Jukwaa kubwa na jengo jengine nyuma ya Jukwaa la Urusi, kila jengo lilikua na sehemu mbili na vyoo ishirini, kukamilisha uwepo wa vyoo 80 vya kisasa kabisa. Lengo la ujenzi wa vyoo hivyo ni kuwapa huduma washirika wa sekta ya michezo wanaokuja kiwanjani hapo hasa wanaocheza nje ya uwanja wa ndani wa Amani.

Mhe. Spika, mwaka 2012, jengo hilo la vyoo lilioko nyuma ya jukwaa la Urusi lilitamiwa na watu wasiojulikana na sehemu moja ya vyoo 20 vikaharibiwa kabisa na miundo mbinu yake kuibwa yote tukio ambalo liliripotiwa polisi.

Mhe. Spika, kwa vile moja kati ya washirika wetu muhimu wa Uwanja wa Amani ni Chama cha Mpira wa Miguu *ZFA* Wilaya ya Mjini amba walikerwa sana na uharibifu huo, waliomba na kukubaliwa na uongozi wa Uwanja wa Amani kuweka ofisi ndogo katika eneo liloharibiwa kwa lengo la kusaidia ulinzi wa vyoo 60 vya nje vilivyobakia na wao kupata eneo la kufanya shughuli zao.

Uongozi wa *ZFA* Wilaya ya Mjini uliopo hivi sasa umekuwa na wazo wa kutoka mashirikiano na uongozi wa Uwanja wa Amani katika kulitunza eneo la Nje la Uwanja wa Amani wazo ambalo linazingatiwa na wizara yangu.

**Mhe. Ali Salum Haji:** (a) Mhe. Spika, nilitaka kujua tu ujenzi wa choo kile cha nyuma yaani Jukwaa la Urusi uligharimu kiasi gani katika matengenezo yake.

(b)Uharibifu uliofanywa uligharimu kiasi gani hata ikaonekana ni bora tuondokane katika suala la vyoo ili tuelekee katika suala la Ofisi na kupelekea kuleta matatizo kwa watumiaji wa michezo katika eneo la nyuma la Uwanja wa Amani.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, naomba arudie sijamsikia kabisa maswali yake.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, maswali yangu yalikuwa ni madogo tu.

(a)Mhe. Spika, nilitaka kujua tu ujenzi wa choo kile cha nyuma yaani Jukwaa la Urusi uligharimu kiasi gani katika matengenezo yake.

(b)Uharibifu uliofanywa ulilitia hasara kiasi gani hata ikaonekana ni bora kuondokana na vyoo na kuweka Ofisi na kupelekea kutoa matatizo kwa watumiaji wa michezo katika upande wa nyuma na pia kuchafua mazingira ya nchi yetu.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, majengo yale mawili ambayo yana vyoo 40 kila moja kwanza hayakufanyiwa matengenezo ni majengo mapya yaliyojengwa. Uharibifu ambaa umefanywa...

#### **TAARIFA**

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, maswali yangu ni dogo tu, nilitaka kujua *cost* ya awali ya matengenezo ya kile choo *and then* itakuja *cost* ya hasara iliyopelekewa na hao wezi ambaa waliharibu miundombinu hata ikapelekea kuondokana na choo baadae tuweke ofisi na kupelekea uchafunzi wa mazingira kwa watumiaji wa eneo lile kwa kukojoa ovyo.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, narudi kwenye suala la msingi kwamba wakati wa ujenzi wa vyoo vile ni kwamba hakuna marekebisho yaliyofanywa, *blocks* mbili mpya zimejengwa; moja mbele ya jukwa kubwa na moja nyuma ambayo kila *block* ilikuwa na *wings* mbili na kila *wing* lina vyoo 20.

Sasa kwa hivi sasa sina gharama halisi iliyotumika kujenga kila *block* na vyoo vingapi. Isipokuwa gharama za maharibiko yaliyofanywa tuliyoyafanya ni kama shilingi milioni thalathini katika vile vyoo 20 ambavyo viliharibiwa kabisa.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Spika, katika majibu ya Mhe. Waziri amesema kwamba kwa vile moja wa washirika wetu muhimu wa Uwanja wa Amani ni Chama cha Mpira wa Miguu ZFA Wilaya ya Mjini.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri Kiongozi ambaye ndie alikuwa ni Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo Mhe. Ali Juma Shamuhuna, kwa kuweza kuwapatia ZFA kuweza kupata kiwanja cha kujenga ofisi ambayo iko nyuma ya Uwanja wa Amani.

Mhe. Spika, ili kuondokana na vyama vyetu vya Mpira ya Miguu kuhamia ndani vya vyoo na ukizingatia kwamba vyama vyetu ni masikini havina uwezo wa kuijendesha na kwa vile hapa Mhe. Waziri amekiri kwamba ni moja kati ya washirika.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia ZFA kuweza kujenga lile jengo lao lilioko nyuma ya Uwanja wa Amani.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Salim Ali, mdau mkubwa wa michezo, aliywahi kuwa Katibu wa ZFA Wilaya ya Mjini siku nyingi na ambaye wakati wake bahati mbaya alishindwa kusaidia kujenga Ofisi ya ZFA Wilaya ya Mjini. Sasa...

#### **UTARATIBU**

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Spika, nadhani kauli ya Mhe. Waziri, sio sahihi kwa sababu hata hicho Kiwanja ambacho *ZFA* wamekipata imetokana na bidii yangu mimi pamoja na kwa msaada wa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, naomba arekebishe kauli yake. (*Kicheko*)

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, nakushukuru na nakubali kwamba Mhe. Nassor Salim, alisaidia kupata kiwanja, lakini akashidwa kujenga. Lakini pamoja na hayo kwamba wazo lake tumelichukuwa na wizara itajitahidi kwa kushirikiana na uongozi uliopo hivi sasa kuona kwamba *ZFA* imepata ofisi nzuri inayostahiki katika eneo letu la Mji wa Zanzibar.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, kwanza nacheka na sababu za kunifanya kucheka ninavyojuu ulimwenguni unapojenga kiwanja cha aina yoyote na hasa ukisema *National Stadium*, kwa kuwa viwanja hivi vya kimataifa vinaendana na ramani *special*. Je, Mhe. Waziri huoni hoja ya kusema katika Baraza hili tukufu kuwa umekuwa kuwa choo kugeuzwa kuwa ni ofisi ni kuchekesha ulimwengu wa mpira. (*Kicheko*)

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, nakushukuru na naomba nimjibu Mhe. Makame Mshimba, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kitope.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba, anatembea sana tu katika ulimwengu na juzi juzi alisema jana kama alikuwa Spein na unapotembea katika ulimwengu ni jambo la kawaida sana kwenda katika vyoo ukawakuta watu mle wana kiofisi kabla ya kuingia unalipa kwanza ndio unakwenda kujisaidia.

Kwa hivyo, hili si jambo geni hata katika ulimwengu, hili ni la kawaida kabisa Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa, kabla hatujaendelea kabla hatujaendela na leo kama kawaida tuna wageni wako pale juu. Naomba niwatambulise wageni wetu wa leo ni Serikali ya wanafunzi ya Chuo cha *Institute of Professional Study*, baadhi ya wanafunzi hao wako pale juu naomba tuwatambue. Ahsante sana tunaendelea. (*Makofii*)

## TAARIFA ZA KAMATI

### **Ripoti ya Kamati ya Katiba ya Sheria na Utawala ya Mwaka 2014/15**

(*Majadiliano yanaendelea*)

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia ripoti hizi za wizara mbili; Wizara ya Tawala za Mikoa na Idara Maalum pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe Spika, pia, naomba niwapongeze Mawaziri pamoja na watendaji wao na hasa kwa upande wa Idara Maalum Vikosi kwa kazi kubwa wanayoifanya kuimarisha amani na utulivu wa nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba pia niipongeze Serikali kwa kutekeleza vyema Idara ya 2020 MKUZA II, ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010/15 na Malengo ya *Millenium*. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono ripoti hii.

Mhe. Spika, nitakwenda katika Tawala za Mikoa na Idara Maalum. Ripoti ya Tawala za Mikoa ina karibu maagizo 39 ya Kamati na Wizara ya Katiba na Sheria ina maagizo kama 21 ya Kamati na tumeelezewa utekelezaji wake katika ripoti zote hizi, hatua mbali mbali zimekelezwa, nyengine zimechukuwa muda mrefu na nyengine muda mfupi, kwa sababu ukiangalia maagizo ya Kamati yaliyoanishwa kuna mengine yanachukuliwa hatua haraka, lakini kuna mengine yanahitaji mashirikianoa baina ya wizara na mengine yanahitaji kuomba ufadhili kutoka nje fedha ili kutekeleza shughuli mbali mbali ambazo zimeangizwa katika kamati hii.

Kwa hiyo, utekelezaji unakwenda hatua kwa hatua, haraka, taratibu unategemea na agizo lenyewe ambalo Kamati imeelekeza.

Mhe. Spika, naomba tu nitoe ushauri kwa wizara hizi wajitahidi kwa yale maagizo ambayo Kamati inatoa, wajitahidi, wafanye bidii kabisa, juhudhi za makusudi wachukulie hatua haraka na zile changamoto ambazo zimejitokeza katika utendaji, suala zima la maslahi mfano na mambo mengine wajitahidi wizara kulifanya kazi ili kuona kwamba malalamiko haya yanapungua au hata kuondoka kabisa.

Mhe. Spika, Serikali imetekeleza mambo mbali mbali na imeleta mafanikio makubwa yamepatikana katika nchi, hii ikiwemo suala la amani, umoja na mshikamo kwa Wazanzibari na Watanzania. Huduma mbali mbali zimeimarika Serikali imefanya huduma mbali mbali zikiwemo elimu, afya, miundombinu, uwanja ndege na zinaonekana tu.

Mhe. Spika, sitokwenda *deep* kwenye ripoti kwa sababu ripoti imejieleza na utekelezaji wake, nilikuwa naomba kwa vile Serikali imefanya mambo mengi ya mafanikio na yanaonekana naomba tu Waheshimiwa wenzangu basi wapitie hata ile hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenye Sherehe ya miaka 51 ya Mapinduzi, muna kila kitu mule ambacho kimefanya Serikali, miradi mbali mbali imejengwa, kila kitu hakuna kilichobakishwa. Kwa hivyo, ukiipitia ile utaiona hasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nini imefanya katika taarifa ile.

Mhe. Spika, kwa kumalizia tu naomba niseme Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hajashindwa kufanya kazi zake. Serikali inafaya kazi zake ipasavyo na hajashindwa chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein pamoja na Mawaziri wake na haitoshindwa kwa kweli, kwa sababu ni Serikali imara na itafanyakazi zake kama itakavyojipangia inafaa, haitoshindwa. (*Makofisi*)

Kwa hivyo, kwa wale wanaosema Serikali imeshindwa kwa kweli hawaitendei haki. Mambo ya maendeleo yanaonekana, hakuna asiyeaona, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni jamani.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofisi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Nimkaribishe Mhe. Rufai Said Rufai, baadae afuate Mhe. Ali Salim Haji wakati Mhe. Mohamed Haji Khalid, anajitayarisha.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Spika, awali ya yote sina budi na mimi sina budi kwanza kumshukuru *Allah Subuhana Wataallah* kwa kutujaalia hali ya uzima na afya njema asubuhi hii kuweza kukutana hapa na kuweza kuendelea na majukumu ya nchi yetu ambayo ni haki na wajibu kwa muda huu tulionao, kwa kusikiliza ziara za Kamati za Baraza katika taasisi na wizara mbali mbali zilizomo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, jana na leo tumo katika ripoti ya kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala Bora ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, ukiangalia Taarifa za Kamati hizi, Serikalini bado kuna changamoto nydingi ambazo ni kikwazo kwa watendaji, lakini ndani ya changamoto ndipo munapopata uwono na kujenga na kuondosha zile changamoto ili nchi yetu iweze kupiga hatua mbele.

Mhe. Spika, baadhi ya changamoto tulizonazo nyengine ni za muda mrefu. Kuna changamoto za mwaka jana zilizopita kabla ya Kamati hazijapangwa vyengine ziliwasilishwa hapa na bado na mara hii zinaendelea changamoto hizo, lakini ndiyo katika kutafuta ufanisi.

Mhe. Spika, kwa upande wangu leo mimi nianze na Wizara ya Nchi, (*OR*), Tawala za Mikoa na Idara ya Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, kuna changamoto ya mwanzo hapa iliyonekana na Kamati hii ni suala zima la ufinyu wa bajeti inayoingizwa idara za Serikali na ukosefu wa usafiri kwa ajili ya kazi za idara.

Mhe. Spika, inapoekwa idara ina maana idara ni taasisi na taasisi ile shughuli zake hazimalizikii pale tu ofisini. Shughuli zinakuwa zina mtandao mrefu, zina hitaji ufuatiliaji. Sasa idara kama itakuwa haina usafiri, hichi ni kikwazo na ni tatizo na kuifanya idara ile ikose kufanya haki na wajibu na ufanisi kwa masuala yake mazima kuifanyakazi idara husika.

Mhe. Spika, lakini pia zipo idara mbali mbali katika Wizara hii, tatizo hili lipo. Lakini pia ukosefu wa kuingiziwa fedha, hapa maelezo yanasema kwamba Kamati ilipotembelea idara hii imekuta katika robo moja ya mwaka imeingiziwa kiasi cha shilingi milioni tano tu kwa miezi mitatu. Hii ni pesa ndogo kwa idara, haziwezi kukifu, haiwezi kufanya shughuli zake vizuri.

Kwa hivyo, tunaiomba sana Serikali ijaribu sana iwe makini katika kuingizia hizi idara zile fedha ambazo wameziomba ili iweze kufanya kazi zake vizuri. Lakini ikiwa robo nzima idara inaingiziwa pesa ndogo mno, kwa kweli pesa hizo inashindwa hata namna gani itagaiwa katika idara hiyo. Hivyo, changamoto kama haya ni vyema Serikali iweze kujiandaa vya kutosha.

Mhe. Spika, nikija katika Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ. Kuna karibuni changamoto tano lakini mimi nitazungumzia moja katika changamoto hizo. Kamati ilipopita katika Tume hii imekuta Ofisi ipo katika eneo finyu ambalo Katibu wa Tume anatumia eneo moja dogo na Katibu Muhtasi na watendaji wengine wanatumia kijiofisi hicho hicho. Hili ni tatizo.

Hii ni Tume ya Utumishi katika hizi Idara Maalum. Kwa hivyo, kiofisi hicho kifinyu kiduchu ikawa watendaji wote wanatumia ofisi hiyo, hili ni tatizo. Mambo ya *files* yanaweza yakakosa kuwekwa vizuri, unaweza ukapita ubahirifu, kwa sababu ofisi inapokuwa na zaidi ya watendaji wawili kumbukumbu zinaweza zikachukuliwa. Nani utamlaumu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, bado changamoto hii nasema kwamba zinahitaji kufanyiwa ufanisi ili kuliondosha haraka tatizo hili. Kuweka watendaji wawili ofisi moja tena tena ni ndogo mno, hili si jambo zuri hata kidogo.

Lakini Mhe. Spika, niingie katika changamoto zilizopo katika Chuo cha Mafunzo. Kuna changamoto karibuni sita walizozionesha wenzetu hawa katika Kamati yao, lakini mimi nizungumzie katika changamoto ya pili na ya tatu.

Mhe. Spika, Kamati ilipopita katika idara hii hasa kwa upande wa Pemba mara nyingi hawashirikishwi katika uandaaji wa bajeti, yaani katika kuandaa bajeti kwa Idara ya Mafunzo Pemba hawashirikishwi katika kuandaa bajeti.

Mhe. Spika, Waswahili wanasema kwamba "yule mwenye kukaa mavani ndiye anayevijua vizuu". Kwa hivyo, matatizo ya idara hii Pemba, wale waliopo Pemba ndiyo wanaojua matatizo yao. Kama hawashirikishwi katika kuandaa bajeti, waliopo Unguja ndiyo wanaoandaa bajeti ya waliopo Pemba. Vipi wataweza kuondosha matatizo yao. Na ukiangalia ripoti hii mara nyingi waliopo Pemba shughuli zao hawashirikishwi wanaofanya watu waliopo Unguja. Kwa hivyo, hizi idara zetu hasa huku kwa upande wa Pemba itakuwa hazifanyiwi haki yake.

Mhe. Spika, na sijui naomba nije nielezwe ni sababu gani ambazo idara zilizokuwepo Pemba zikawa hazishirikishwi katika kuandaa bajeti. Sasa hii inakuwa ni tatizo. Ni vyema hizi idara zishirikishwe kwa hali yoyote ili matatizo yao waweze kuyasema na yaweze kurekebishwa. Lakini aliyekuwepo Unguja anaandika matatizo ya waliopo Pemba, ataandika yale anayoyahisi yeye. Unaweza ukabuni jambo ukasema hili ni tatizo kwa Pemba, lakini kumbe kwao lile siyo tatizo. Kwa hivyo, ni vyema idara hizi zishirikishwe ili waweze kusema yale ambayo ni makero kwao na yaweze kuingiziwa fedha ili tuondokane na tatizo hilo.

Mhe. Spika, lakini katika Idara hii ya Mafunzo uchakavu na ubovu wa majengo ya ofisi pamoja na nyumba za kuishi askari na ubovu wa Magereza, hii ni changamoto ambayo ipo.

Mhe. Spika, hili ni tatizo sugu na kila ripoti inayokuja masuala haya ya uchakavu wa majengo pamoja na nyumba za kuishi askari, tatizo hili lipo.

Mhe. Spika, hawa wanaofanya kazi, kuna wengine wanafanya kazi, kuna wengine ni wafungwa. Lakini kwa hali hii inaoneshea kwamba wote wapo katika sehemu moja, wote ni wafungwa. Aliyefungwa analala katika jengo bovu, chakavu kabisa na ofisi zao zinalingana na hizo nyumba wanazolala wafungwa. (*Makofit*)

Mhe. Spika, hili ni tatizo. Sasa watu wote, mfungwa anatiwa adabu na yule anayesimamia mfungwa naye anatiwa adamu. Kwa hivyo, itakuwa hapa hatuwatendei haki. Hii si haki. Hata huyo anayefungwa ana haki zake za kibinadamu, ni lazima alale phalaha ambapo panastahiki kulala mwanadamu. Sio kulala katika maeneo ambayo

hayastahiki mwanadamu. Leo utakuta kwamba kuna ofisi wanafanyakazi wanalala humo humo, kesi zinaendeshewa humo humo. Kamati inasema hapa walikwenda katika maeneo ule mkutano wa Kamati unafanywa chini ya mti kwa ukosefu wa ofisi.

Mhe. Spika, hii si haki na hivi sasa kila kukicha tunaongeza tena kuajiri. Baada ya haya majengo tuliyokuwa nayo baada ya kutafuta ima wafadhili ya yakajengwa upya au Serikali ikaona kwamba hili ni tatizo ikaiingiza fedha za kutosha, haya majengo yakajengwa upya, kulikoni kuongeza wafanyakazi kuajiri vijana lakini pa kuwaweka hatuna. Itakuwa hatujafanya haki na lazima ya mwanadamu iheshimiwe. Mwanadamu ni kiumbe bora kuliko viumb vyengine vyote.

Kwa hivyo, ukamlaza maeneo ambayo kukiwa na mvua yeze anaroa, kukiwa na jua yeze anateseka, hii itakuwa haki yake hatujampa mwanadamu huyu.

Mhe. Spika, kwa hivyo. hili ni tatizo na tatizo hili kila kipindi linajirudia na sijui vipi...

**Mhe. Spika:** Una dakika 5.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Haya tunayoyazungumza sijui Serikali haitaki kuyasikiliza na kufuatilia vipi, inakuwa ni tatizo.

Mhe. Spika, nikiendelea kwamba kuna aidha Kamati ilisisitiza kuwa suala la upatikanaji wa huduma za maji safi na salama ni muhimu katika eneo la kambi zote.

Mhe. Spika, bila ya maji hakuna kuishi. Kwa hivyo, kupatiwa maji katika kambi hizi za Mafunzo ni muhimu mno, kwa sababu mfungwa anastahiki kupata maji na yule msimamizi wa mfungwa na yeze pia anastahiki kupata maji safi na salama. Kwa hivyo. ni vyema Mhe. Spika, Mhe. Waziri. nadhani hapo ananisikia vya kutosha, masuala haya yanahitaji changamoto hizi kuzisimamia na kuzifuatilia vya kutosha.

Mhe. Spika, vile vile, nikiendelea kidogo nizungumze katika maoni na maagizo ya jumla ya Kamati katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mimi nitakuwa na suala moja tu hapa, ni suala zima la Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, suala la usafi, tukitaka tusitake kwamba Manispaa ya Mji wa Zanzibar bado hali yake hairidhishi na mvua hizi zinazoanza, kila kipenyo unachopita hasa maeneo ya Mji Mkongwe harufu inayotoka inakuwa inahatarisha amani ya wananchi.

Mhe. Spika, usafi ni dira na kila kitu kinasimamia usafi. Hata katika Uislamu wetu, Uislamu imeipa namba moja usafi. Na Serikali imechukua sera hiyo ya usafi, usafi wa kimwili, usafi wa nguo na usafi wa mazingira. Kwa sababu usafi unaepusha maradhi mengi, maambukizi mengi na mambo mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa kweli hali halisi ya Mji ni mbaya. Mimi ningeshauri sana Mhe. Waziri, kuanzisha katika kuhifadhi hizi taka taka ndogo ndogo, kuweka *ma-dust bins* yale ya kutilia taka kila maeneo, hasa maeneo ya kule Mji Mkongwe. Kuna kuratasi hizi za *tissues* na mambo mengine, zile zikiingia maji huwa ni uchafu, lakini karatasi kama ile mtu anapoitumia kama pana eneo la kuhifadhi ile karatasi haiangushi katika barabara au katika uwanja wowote, inahifadhika vizuri basi inaweza kutusaidia.

Mhe. Spika, Mji wa Zanzibar umesafika siku moja tu. Kumbe kuwa wasafi tunaweza. Siku kabla ya kuja Rais wa Ujerumani, siku mbili tu Mji ulisafika vya kutosha. Kwa sababu eti anakuja Rais wa Ujerumani. Sasa sisi wenyewe uchafu tukae nao, hivi Mji usafike kwa kuja mgeni hadi mgeni?

Mhe. Spika, hili ni tatizo kabisa. (*Makofî*)

Mhe. Spika, kumbe tuna uwezo wa kuusafisha Mji ukawa safi. Kuja kwa Rais wa Ujerumani na kutembea na siku hiyo nzima, sisi wengine tulio wahii kutembea, karatasi ulikuwa huikuti chini, uwanjani au barabarani, yaani karatasi ilikuwa ndio siku 90 uwanjani au barabarani, kwa sababu pana Rais wa Ujerumani. Mhe. Spika, kumbe uwezo wa kuwa mji wetu safi upo, lakini inategemea kumbe usimamizi hautoshi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, na Mhe. Waziri suala hili kumbe upo uwezekano wa mji kuwa safi. Kibaya usimamizi bado haujaka vizuri, ningkuomba hili pia uweze kulisimamia kama uliviyosimamia kuja kwa Rais wa Ujerumani na mji ukawa safi.

Mhe. Spika, umeniambia dakika tano, kwa hivyo sipendi nikukope muda wako sana. Kwa hayo machache nadhani nimeeleweka, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Ali Salum Haji, afuate baadaye Mhe. Mohammed Haji Khalid, wakati Mhe. Farida anajitayarisha.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa dhati, kwa sababu ya uchache wa muda na ingawa kwa bahati nzuri mimi hujanipa muda sijui kama tano au kumi, lakini nitajaribu kuzungumza kwa haraka haraka kwa ujumla. Unajua taarifa za wizara tatu hizi, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, zaidi nitajikita katika hizi wizara mbili; Wizara ya Nchi, Kazi na Utumishi wa Umma na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Mimi nilitaka niwashukuru tu waheshimiwa kwa taarifa zao nzuri ambazo wamezileta, baada ya mapitio ya kamati na maagizo ya kamati. Kwa kweli nataka niwapongeze kwa dhati kabisa namna walivyoonesha jitihada ya kutekeleza yale maagizo ya kamati ambayo wamepewa, na niwaombe kwa dhati kabisa waendelee kuchapa kazi ili kuleta matumaini kwa wananchi wa nchi hii katika kuwaaletea maendeleo na kuwaondoshea matatizo yao siku hadi siku. Tumeanza kufarijika na kupata imani juu ya utendaji wa kazi namna wanavyozifanya.

Mhe. Spika, katika Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma katika ukurasa wa 4 Idara ya Nyaraka. Hapa mimi namuomba Mhe. Waziri, yalitolewa maelezo pale namna wizara ilivyoombwa na kamati katika kuangalia afya za wafanayakazi wale. Nimuombe Mhe. Waziri kufuatilia kwa kina suala hili, kwa sababu kuna taarifa za uhakika kwamba pale kuna mfanyakazi mmoja alipata athari ya kupata maradhi ya kutapika damu na baadaye kufariki dunia. Sasa wafanyakazi wa kitengo kile cha nyaraka wamekuwa wakipatwa na hofu kutoptana na *chemicals* au na makabrasha ambayo wanatunga katika hali ile, nimuombe afanye jitihada kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ili kuona wale vijana wanatengewa bajeti ambayo itawapa matumaini ya kuweza kufanya kazi kwa ufanisi, kwa sababu hali ya afya ya mwanadamu kila mmoja anafahamu nini afya ya mwanadamu katika maisha yake. Sasa hili lilikuwa ni ombi la msisitizo kwa Mhe. Waziri katika jitihada anazofanya basi na hili nalo atoe msisitizo.

Jengine Mhe. Spika, katika Wizara hii ya Kazi na Utumishi wa Umma, nilitaka nizungumzie tu, kuna kipengele katika kabrasha lako umeelezea namna ya kuanza kusambazwa kwa sheria ya utumishi wa umma namba 2 ya mwaka 2011.

Mhe. Spika, ni jambo jema wananchi wetu walikuwa wakipiga makelele katika suala la uajiri, waajiri wengi walikuwa hawana nia njema na watu wetu na walikuwa wameshafikia pahala kufanya mambo ambayo yanakwenda kinyume na utaratibu.

Lakini nimuombe tena Mhe. Waziri katika hili pamoja na kusambazwa, basi pia ajitahidi kusimamia ili kuona ile kazi ina dhamira ya kufuatwa kwa sheria hii kwa waajiri inatekelezwa kwa vitendo, kwa sababu mara nydingi sheria zinakuwepo lakini kinachokosekana ni utendaji wa ile sheria yenye na kufuatwa. Kwa sababu hata hizo sheria zenye wote wanafahamu. Sheria hii imetungwa tangu mwaka 2011 kama mwajiri ni lazima sheria ya kazi aielewe na ni lazima ajue namna ya kutoa haki kwa wafanyakazi wake ambao ye ye anawaajiri. Sasa nimuombe Mhe. Waziri nalo hili pia ajitahidi katika kusitiza. Mimi sina mashaka na Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma, kazi nzuri maendeleo siku hadi siku tunayaona na mabadiliko ya nchi yetu katika utumishi wa umma basi yanazidi kupiga hatua.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nataka niende katika Tawala za Mikoa. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri au bahari mbaya wajumbe wengi wanaochangia taarifa hizi, wengi wao wanajikita katika suala la Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, na wengi wao wamekuwa wakipiga kelele ya kukatisha tamaa na kutoa matumaini kwamba wizara hii haifanyi kazi, haisimamiwi na mji mchafu.

Mhe. Spika, kila mtu na mtazamo wake, unajua tunaelekea katika wakati wa kisiasa, kila mtu anachangia kwa namna ambavyo anaona, lakini Mhe. Spika, mimi nataka niwasaidie wenzangu namna gani ambavyo wizara hii imeweza kufanya kazi, na lazima tukubali ukweli utabakia kwamba ni ukweli, na kama mtu hataki kuamini ukweli itakuwa hiyo ni imani yake.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 9 kifungu cha 9, kuna suala la kutoa elimu kwa wanafunzi. Hili nilitaka nimuunge mkono Mhe. Waziri, kwamba ni jambo jema la kuanzisha mpango wa elimu kwa wanafunzi wa magerezani. Namuomba zaidi Mhe. Waziri katika taaluma ambazo atazitoa, basi wajilenge zaidi katika kutoa taaluma za ujasiriamali ili wanafunzi wale watakapotoka katika magereza basi waweze kupata kazi za kujiajiri wao wenyewe.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilitaka nizungumzie ni suala zima la usafi ambalo wajumbe wengi wamelipigia kelele za kutosha, na wengine wakafika kudirika kusema kwamba walishindwa kula katika maeneo ya Darajani. Mimi sitaki kulizungumzia zaidi hilo, kwa sababu kila mtu anajua heshima yake na anajua kazi yake. Mimi kama Ali Salum siwezi kwenda kukaa Darajani pale kwenye kibanda nikala, kwa sababu najua *status* yangu ni ya aina gani, lakini zaidi nataka nizungumzie katika suala la Manispaa.

Mhe. Spika, ni kweli, lazima tukiri kwamba taka ni nyingi, na taka hizi zinatokana na kuzidiwa kwa ndugu zetu wa Manispaa. Uzalishaji umekuwa ni mkubwa, lakini uwezo wa kuondosha taka katika mji wetu umekuwa ni mdogo. Hili Mhe. Spika, limekuwa linatokana na uchakavu wa magari pamoja na vitendea kazi, lakini kwa heshima kubwa nilitaka niishukuru na niipongeze serikali pamoja na wizara husika, kwa jitihada ambazo wameamua kuzifanya katika kutokomeza au kukabiliana na tatizo hili. Mhe. Spika, kwa nini niseme hivi. Mhe. Spika, nina taarifa za uhakika ambazo tayari Baraza la Manispaa limejipanga katika kukabiliana na suala hili.

Sasa kama serikali au wizara imeamua kujipanga na kujitahidi kukabiliana na hili suala, basi tuwasubiri yale mafanikio ambayo wameyaanzisha tuone yamatilizika vifi. Mhe. Spika, Baraza la Manispaa karibuni wameweza kupata gari 5 kuititia mradi wa ZUSP, mradi huu ulikuwa umeanza muda mrefu, lakini siku hadi siku umekuwa ukileta mabadiliko katika nchi yetu.

Mhe. Spika, magari ambayo yalipatikana karibuni ni gari za *compressor* mbili, *tipper* mbili na makontena karibu 193. Mhe. Spika, vifaa hivi ambavyo siku mbili tatu zilizopita vilikabidhiwa kwa Baraza la Manispaa, tuna imani kwamba zitakapoanza kazi basi yale masikitiko na yale maneno ambayo tulikuwa tukiyapigia kelele yanaweza yakatoweka kabisa.

Mhe. Spika, Baraza la Manispaa hivi sasa hivi uwezo waliokuwa nao ni kuweza kuondosha tani 300 sawa sawa na asilimia 45 kwa siku. Kwa kweli ukiangalia uwezo huo yaani hata nusu ya taka ambazo zinazalishwa katika mji wetu walikuwa hawana uwezo wa kuuondosha, lakini kutokana na mazingira ya jitihada ya serikali kutafuta zana, magari na vifaa tena vya kisasa katika kufanya kazi ya kuweza kuondosha tatizo hili, basi mimi nina imani kwamba kazi hii itaondosha manung'unico.

Lakini niumombe Mhe. Waziri pamoja na jitihada zenu ambazo mumezifanya kama serikali, kuweza kusaidia vifaa hivi ambavyo nimevielezea hapa, bado kutakuwa kuna changamoto ambazo wenzetu zinaweza zikawakabili, ningekuomba kuangalia changamoto ambazo zinaweza zikawakabili ili kuweza kulisiaidia suala hili.

Mhe. Spika, tunapongeza magari, tunapongeza na zana za kisasa, yaani kuna magari ya *compressor* ya kisasa yale magari yanahitaji huduma za mara kwa mara. Sasa kuna haja njema ya kujipanga katika suala la kibajeti kuona kama magari yale baada ya kufika yasije kuchukua muda mfupi yakaanza kulala.

Jengine Mhe. Spika, hivi sasa hivi Baraza la Manispaa wanatumia karibu milioni 26 kwa magari waliyokuwa nayo kwa mwezi katika kutoa huduma katika suala la taka katika mji wetu wa Zanzibar. Milioni 26 ambazo wanazoa tani 300 na ni asilimia 45. Sasa kutokana na kupata magari haya, basi tujijue kwamba tunaweza tukatumia mara mbili zaidi ya gharama ya mafuta ambayo tuliyokuwa nayo hivi sasa. Sasa niumombe kutafuta namna ya kuweza kulisiaidia Baraza la Manispaa kuweza kuondosha tatizo hili ili magari yasijekuwa yako tayari, magari yanataka kufanya kazi lakini tukabakia na tatizo la mafuta, kwani tunafahamu Baraza la Manispaa bado lina matatizo ya ukusanyaji wa kodi ya mapato, kodi wanayokusanya haitoshelezi kuweza kutoa huduma katika mji wetu wa Zanzibar, na niishukuru serikali kwamba imewasaidia kwa kuweza kuwapatia ruzuku ya mishahara ili kuondosha matatizo ya kuweza kuendesha hiyo huduma.

Mhe. Spika, magari haya na hususan haya magari ya *compressor* ambayo wanatumia ni magari ambayo yana matatizo, pamoa na kwamba yanahitaji huduma za kila wakati, lakini pia yanakuwa yanahitaji kwa kila wakati yanakuwa ya *full tank* katika magari hayo ili yawewe ku-*survive* katika mazingira mazuri. Sasa mimi naishukuru serikali kwa jitihada baada ya wao wenyewe kuona ni kweli kwamba tatizo la taka lipo na kuweza kufanya jitihada katika hili suala.

Mhe. Spika, hayo yote yanaweza kufanyika kwa namna gani. Mambo hayo Mhe. Spika, yanaweza kufanyika kwa kuwa na uwezo serikali na wengi waliochangia walikuwa wakipiga kelele kwamba serikali bajeti ndogo, haitoi ipasavyo, wizara zinashindwa kufanya kazi zake ipasavyo. Mimi Mhe. Spika, nataka niseme kidogo tu katika hili, kuna mambo lazima tukubaliane na lazima haya mambo Mhe. Spika, tuwe wakweli katika kuyazungumza. Unajua unaweza ukazungumza kitu ukaonekana unazungumza.

Kwa mfano, kama mimi ni Muislamu Mhe. Spika, lakini naweza nikajinata mbele ya hadhara ya watu kwamba mimi ni Muislamu, lakini naweza nikaulizwa umeswali lini, kwa sababu wajibu wa Muislamu ni kusali, sasa inawezekana unazungumza vitu mdomoni, lakini katika nafsi yako Mhe. Spika, hivi vitu havipo, kwa nini nazungumza hivi. Nazungumza hivi kwa sababu sote tunapiga makelele hapa kwamba serikali hii haitoi pesa kwa wizara, wizara hazina pesa kazi hazifanyiki, lakini serikali hii hii inatafuta namna ya kufanya jitihada ya kupata hizo fedha ili uweze kupeleka fedha nyingi katika taasisi zetu, lakini hao hao wanapiga kelele kwamba serikali hii haitoi pesa, ndio hao hao zile njia ambazo serikali wanapanga za kutafuta fedha ndio wao muda unapofika wanaporudi nyuma na wakazorotesha ule uwezo wa serikali wa kuweza kupata pesa. Kwa nini Mhe. Spika, nasema hivyo.

Nasema hivyo Mhe. Spika, kwa sababu ndogo tu. Mhe. Spika, karibuni tu tulikwenda kwenye Bunge la Katiba, na tulikuwa tukipiga kelele kwamba mambo mengi uchumi wa Zanzibar umebarwa na Bara, sijui kuna mambo haya na haya. Lakini tumekwenda kule ili kuona tunapata fursa ya kuweza kusaidia nchi yetu kuweza kukuza uchumi, katika maeneo gani, katika maeneo ya kuweza kuchimba mafuta sisi wenyewe, katika maeneno ya kuweza kujiunga na kanda za kimataifa, ili zile taasisi ziweze kutusaidia katika maeneo mbali mbali. Tulipiga kelele kwa wenzetu ili serikali ikubalike, ikishakbalika mambo haya katiba ikipita hii basi serikali hii itakuwa na uchumi mkubwa. Haya tunayolalamikia, huo uwezo tunaouzungumza utaondoka, lakini ndio hao hao wanaopiga kelele serikali haina pesa, ukitafuta njia wao ndio wa mwanzo kutoka katika mabunge na matokeo yake zile faraja za kuweza kusaidia Mhe. Spika, zinakuwa haziwezekani.

Mhe. Spika, nataka nimalizie hili kwa kumtolea mfano mtu mmoja tu. Kulikuwa kuna *actors* Mwenyezi Mungu amrehemu, alikuwa anaitwa Dk. Ayoub. Mhe. Spika, Dk. Ayoub kuna mchezo mmoja ali-*act* yeeye akawa Afisa mmoja wa Polisi wa Mkoa, sasa katika mkoa wake ulikuwa hauishi kufanyika uhalifu, sasa akawa na yale ninayoyazungumza kwamba anayoyazungumza mengine na anayotenda mengine. Kwenye vikao vyake yeeye mwenyewe alikuwa ni mionganoni mwa wale wahalifu. Sasa kila siku kwenye vikao anapiga kelele, wahalifu wengi, watu wanauliwa, askari hamfanyi kazi, kumbe na yeeye mwenyewe ni mionganoni mwa wale wahalifu. Sasa siku ya kupanga kazi anajua kwamba leo wahalifu wake ameshawapanga wanakwenda Kusini, yeeye askari anawapangia kazi Kaskazini. Kwa hivyo, matokeo yake askari wanakwenda Kaskazini, uhalifu unafanyika Kusini akifika anapiga kelele uhalifu unakuwa mwingu.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru na nataka kuwaomba Waheshimiwa Mawaziri pigeni kazi, sisi ndugu zenu tupo na tunajenga matumaini na nchi yetu. Najua mtapata tabu sana, sasa hivi wakati wa kupiga siasa umefika, maneno mengine ni maneno ya siasa sio maneno ya kujenga nchi wala kwa watu wetu. Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofsi*)

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuchangia machache kuhusu ripoti hii ilioko mbele yetu. Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyetuwezesha kufika hapa kufanya shughuli zetu za kawaida za kila siku. Pia nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi hii, na pia nikushukuru kuwa tunaweza tukayarudisha ya Dodoma hapa, kama alivyokwishaonesha Mhe. Ali Salum, ingawaje mimi sitofanya hivyo.

Mhe. Spika, mimi nitaanza mchango wangu mdogo kwanza kwa kuzipongeza hizi wizara tatu ambazo zimewasilisha ripoti zao na maagizo ya kamati, na yale ambayo wameweza kutekeleza wametekeliza na mengine kwa kweli hayakutekelezwa, lakini wameonesha pengine kwa nini hayakutekelezwa.

Mhe. Spika, niseme kwamba muda wa kamati hautoshi. Kwa mfano kama hii tulioizungumza leo inazo wizara tatu. Katika kutembelea taasisi za wizara hizi, ziko taasisi ambazo hawakuwahi kuzitembelea, hii ina maana ni kwa sababu ya upungufu wa wakati. Kwa hivyo, ipo haja Mhe. Spika, ya muda wa kamati kuongezwa ili idara na taasisi zote ziliomo katika wizara husika ziweze kupitiwa na kamati kuonesha maendeleo yao na matatizo yao, kwa nyinyi watu wa sasa na changamoto zao.

Mhe. Spika, mimi nianze na Idara ya Chuo cha Mafunzo. Mhe. Spika, nina ombi hapa maalum. Naomba hili jina Chuo cha Mafunzo tulifanyie marekebisho ili turudishe jina lake la awali, la kabla ya kuitwa hili ilikuwa inaitwa magereza. Kwani Mhe. Spika, jina la Chuo cha Mafunzo liliuja wakati maalum na liliuja kwa sababu maalum. Gereza kubadilishwa kuitwa Chuo cha Mafunzo liliuja kwa wakati maalum na kwa sababu maalum. Sasa nadhani imefika wakati lile jina la kimsingi tukalirudisha, kwa nini nikasema hivyo. Kwa sababu bado jina hili halijatoka katika mdomo wa serikali.

Kwa mfano, katika agizo la mwanzo la kamati kuhusu idara hii, kamati imeeleza kuwa; "kamati inaishauri wizara na serikali kwa ujumla kufanya utaratibu wa kuchukua                    mradi wa ujenzi wa gereza jipya la Hanyegwa Mchana..."

Lengo langu ni kuonesha hili gereza tu na *response* ya serikali kwenye kujibui pia wamesema, ujenzi wa gereza hilo. Kwa hivyo, bado serikali neno gereza katika mdomo wake limo, hakutumia kwa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo, katumia ujenzi wa gereza. Kwa hivyo, kwa sababu ndio jina lake la msingi ni vyema hili jina Mhe. Spika, likarudi ili kuondoa neno chuo, kwa sababu tuna vyuo vingi, tuna vyuo vya amali na vyenginevyo. Kwa hivyo hii tukiita gereza itakuwa ni rahisi zaidi kwa mawazo yangu kuliko kuita Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Spika, niende kwenye agizo la pili la kamati. Kamati inaishauri wizara kukisaidia Chuo cha Mafunzo kwa kuzungumza na uongozi wa Wizara ya Afya na kukubaliana juu ya suala la kuwapatia dawa za kila mwezi Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya matibabu ya wanafunzi. Aidha, kamati inaishauri wizara itafute wafadhili watakoosaidia ujenzi wa hospitali katika kambi za Ubago, Kangagani na Kengeja.

Mhe. Spika, hapa kamati iliagiza mambo mawili tofauti. Moja hivi vyuo vya mafunzo vipatiwe dawa na Wizara ya Afya za kila mwezi. Pia ikaiomba Wizara itafute wafadhili kujenga vituo vya afya katika hizi kambi zilizotajwa, lakini jibu la Serikali wamesema wametafuta mfadhili wa ujenzi wa mnara kwa kuwekea tangi la maji katika kambi ya Bambi, agizo liko vyengine na jibu liko vyengine, agizo dawa jibu ujenzi wa tangi la maji hapa kidogo ningependa Mhe. Spika, nipate maelezo zaidi inaweza kuwa Kiswahili changu mimi hakieleweki, lakini agizo liliikuwa vyengine na Serikali imejibu vyengine, lakini akaendelea kwa upande wa ujenzi wa kituo cha afya mazungumzo yanaendelea kufanyika kwa taasisi nyengine.

Mhe. Spika, kwenye majibu amesema mazungumzo yanaendelea, hapa huwa lile suala bado halijapatiwa muafaka wa utekelezaji, pale Serikali iliposema mazungumzo yanaendelea, pale serikali waliposema mipango iko mbioni hapo huwa bado suala husika halijapatiwa jibu la Serikali.

Mhe. Spika, nisogee mbele kidogo katika agizo la sita kwenye sehemu hiyo hiyo, kamati ilitaka au iliagiza kuhusiana na deni kubwa la umeme. Kamati imekubaliana na ushauri uliotolewa na Idara ya Chuo cha Mafunzo kuwa fedha za bajeti ya umeme zilizotengwa kwa idara zipelekwe moja kwa moja *ZECO*, ili wakate deni hilo kwa lengo la kulipunguza na hatimae kumalizika kabisa, hivyo ndivyo kamati ilivyoshauri kwa kukubaliana na uongozi wa Idara yenye. Lakini jibu la Serikali idara imekaa kikao cha pamoa na bodi ya Shirika na Wizara ya Fedha kujadili uwezekano kwa Wizara ya Fedha kulipia deni la umeme moja kwa moja kutoka bajeti ya Idara.

Sasa hapa Mhe. Spika, tuliona kuwa Idara yenye imekubali kile kidogo wanachokipata chochote kwa ajili ya umeme kiende *ZECO* moja kwa moja, lakini hapa kwenye jibu inatakiwa Wizara ya Fedha kulipia deni la umeme moja kwa moja, hii ina maana ile bajeti ambayo sisi tunaidhinisha hapa isiingie katika mfuko wa chuo lakini Wizara ya Fedha ihaulishe moja kwa moja, sijui kama itakuwa ni utaratibu ulio sahihi au laa. Ningombaa Mhe. Spika, Waziri anisaide kidogo.

Mhe. Spika, kwenye agizo la tisa kwenye Vyuo vya Mafunzo. Agizo hili kamati ilikubaliana na ushauri uliotolewa na baadhi ya wanafunzi waliopo gerezani kwa kuwashirikisha wadau na wawekezaji kuwekeza katika magereza

yetu kwa lengo la kuvutia vitengo mbali mbali vikiwemo, kitengo cha ushoni. Hapa ni kuwa wapewe taaaluma ya ufundi kwa mambo mbali mbali.

Mhe. Spika, vyuo vyetu nya Mafunzo bado vinajishughulisha na jambo moja tu kubwa kuliko mengine yote zaidi ni kilimo, kilimo pengine hata sio cha kisasa. Na pengine ile sababu ya kuitwa vyuo nya mafunzo ni kuwa wale watu wanaoingia pale wanafunzi watapata taaluma mbali mbali na ufundi mwengine, lakini kazi kubwa inayofanyika katika vyuo vyetu hivi ni ile ile ya kilimo, hili neno Chuo cha Mafunzo itakuwa halikukidhi haja, kwa hivyo ningeomba Mhe. Spika, haya mafunzo mengine na amali nyengine zitekelezwe katika hivi vyuo nya mafunzo kila wanafunzi wanapotoka wawewe kujitegemea katika maisha.

Mhe. Spika, niende kidogo kwenye Baraza la Manispaa. Baraza hili lina wajibu mkubwa sana na lina kazi kubwa na ngumu, moja katika kazi yake ni kuhakikisha kuwa mji wetu unakuwa safi na wa kuvutia, mji wetu unakuwa ni mfano na uko kwenye haiba.

Mhe. Spika, wapo wafanyakazi wa ngazi za chini ambazo wale wanaohusika na ule usafishaji wa mji, wafanyakazi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu. Wengine wanazoa taka kwa mikono ambayo haina hifadhi yoyote hata hizo *simple gloves* hawavai, taka chafu wanazoa katika hali hiyo wanahatarisha maisha yao namna hiyo, hawana kinga yoyote na sina hakika kama wanachunguzwa afya zao baada ya muda fulani. Wengi katika wafanyakazi hawa wa chini baadae wanamaliza kazi zao wakiwa watu dhaifu sana kutokana na kazi ngumu ya uchafu wanaozoga, hawana kinga yoyote sio ya mikononi wala si ya puan kujihifadhi na ile harufu mbaya.

Ningeomba Wizara kwa hilo wafanyakazi hawa watafutiwe kinga hizo ili wafanye kazi hii wakiwa angalau wako salama wakati wa kufanya hizi kazi, pamoja na hivyo Mhe. Spika, bado uchafuzi wa mazingira kutokana na taka bado upo na mara nyingi nasema kuwa ili uamini kuwa umefika Mjini Zanzibar ni ile kusikia harufu mbaya, unavyosikia harufu mbaya basi utakuwa na uhakika sasa niko mjini.

Mhe. Spika, zamani ukiingia mji wa Unguja ulikuwa unasikia harufu nzuri ya asumini za Jimbo la Mheshimiwa Mahmoud, sasa imebadilika baada ya kusikia harufu ya asumini unasikia harufu ya machango ya samaki. Ningeomba Mhe. Spika, Serikali ifanye juhud zote za kuhakikisha kuwa haiba, uzuri wa mji wetu unarudi hasa Darajani ambapo ndio kitovu cha mji wenyewe.

Mhe. Spika, niende katika Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mhe. Spika:** Una dakika tatu.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Haya haki yangu ya kusema leo nimeongeza kidogo, kwa hivyo nitaanza kwenye Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo.

Mhe. Spika, afisi hii ni muhimu sana kwa sababu ina utoaji wa vyeti nya aina mbili; cha kuzaliwa na kile cha kifo. Wananchi wengi tayari tumeelimika kutafuta vyeti nya kuzaliwa nya watoto wetu lakini wengi hatujaelimika kutafuta cheti cha kufa cha mtoto wetu au cha mzee wetu. Kwa hivyo elimu inahitajika Mhe. Spika, ya kuelimishwa watu kuwa na hiki cheti cha kifo nacho ni muhimu, sio aliye kufa kwa sababu aliye kufa ndio hataki cheti, wahusika waliofilika wapate cheti cha kifo cha yule aliye fariki.

Mhe. Spika, mara nyengine mzee anafariki tujaalie baba, watoto wanatafuta misaada katika taasisi mbali mbali wanatakiwa ili wathibitishe kuwa mzee wao kafa wanatakiwa cheti cha kifo cha mzee wao, cheti huwa hakipo, kwa hivyo watu waelimishwe kutafuta hivyo vyeti. Pia hivi vyeti nya kuzaliwa mara nyengine vinaonekana kuwa ni vyeti feki na tunajua vipi pale tunapokwenda navyo katika taasisi ya kutafuta vitambulisho nya Mzanzibari wanapochunguza wanatwambia cheti hichi ni feki.

Mhe. Spika, sina hakika kuwa hapa ipo taasisi nyengine iliyo jificha pahala ambayo inatengeneza vyeti, imani yangu vyeti vyote hivi vinatoka katika pahala husika, inakuwaje sasa mwananchi apewe cheti feki. Naomba nipate maelezo hichi cheti feki hasa kinatokea wapi na hakuna taasisi nyengine Mhe. Spika, inayotengeneza hivi vyeti.

Dakika moja ingalipo, jengine Mhe. Spika, niende kwenye Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kuna agizo namba tatu pale ambayo kuna sheria moja kongwe sana ya ushahidi, sheria ambayo ni ya mwaka 1917 sheria hiyo mpaka

leo Mhe. Spika, ipo inatumika, wakati mwengine ushahidi pengine mtu anakwenda malipo yake ni shilingi moja na nusu au shilingi mbili ambao wengi waliomo humu shilingi moja hawaijui na bado ikawa sheria ile iko hai na inatumika.

Ningeomba Mhe. Waziri mbali ya maelezo yake aliyotoa kuwa hatua imechukuliwa imefika hapa lakini bado aongeze *speed* ya sheria hii kongwe ambayo haina maslahi tena iondoke na iwe sheria ambayo italingana kwa nyinyi watu wa sasa na kulingana na wakati, ili ushahidi unapotakiwa kama kuna malipo kwa yule mtu awe analipwa kulingana na hali ya sasa ilivyo. Lakini mpaka leo kutumia sheria ya 1917 pengine wengi humu mlikuwa hamjazaliwa ni tatizo.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa muda umemalizika. Waheshimiwa Wajumbe tunakusudia jambo hili tulimalize leo lakini bahati mbaya au nzuri jana tulitumia muda mkubwa kidogo kuliko vile ambavyo ilitegemewa, kwa hivyo ili nipate nafasi ya kuwaita Waheshimiwa Mawaziri chini ya kamati hii kabla ya kumuuta Mwenyekiti wa Kamati, niombe tu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wafuatao ndio watakaopata nafasi.

Nilimtaja mapema Mhe. Farida, Mhe. Jaku, Mhe. Abdalla Juma na hatimaye tumalizie Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa. Haya Mhe. Farida baadaye Mhe. Jaku.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa na mimi nafasi ya kutoa mchango wangu mdogo katika Wizara hii. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalisa kutufikisha hapa tukiwa na afya njema.

Pia naomba niwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa jinsi walivyofanya kazi zao katika mizunguko yao ya kamati katika visiwa vyetu hivi vya Unguja na Pemba na pia Dar es Salaam. Naomba niwapongeze Mawaziri wote watatu wa Wizara hii jinsi walivyoweza kujibu baadhi ya maoni na ushauri kwa Kamati zetu hizi.

Mhe. Spika, mimi nataka kwanza nianze kwenye Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Hapa naomba nije kwenye Zimamoto Mhe. Spika, suala la uhamisho katika taasisi zetu hizi ni jambo la kawaida na hatulikatai lakini uhamisho wenye unatakiwa ufuate zile taratibu zake. Kamati ilipopita katika taasisi hizi imegundua kuna uhamisho wa askari wetu hawa vikosi vya zimamoto kutoka kiswiwa kimoja kwenda kisiwa chengine na ambapo huko wanakokwenda hawana nyumba za kuishi walizopangiwa na kwa bahati mbaya sana hawakupewa pesa zile za kukodia angalau yale majumba ya kukaa, sasa askari wetu hawa wanafanya kazi kubwa, wanafanya kazi ya uokozi, jambo hili la uokozi linatokezea wakati wowote. Sasa wanataka wapate pahala pazuri na muda mzuri wa kupumzika ili likitokezea lile jambo la maafa wapate kulismamia haraka haraka.

Sasa naiomba sana Wizara inayohusika waliangalie kwa kina hili, wale vijana wetu wanapowatoa katika kisiwa kimoja kwenda chengine waangaliwe angalau na yale maslahi yao kule wanakokwenda ili wapate wafanikishe kazi zao vizuri.

Mhe. Spika, sasa nataka niende katika Ofisi ya Mrasis wa Vizazi na Vifo. Wengi wamezungumza kuhusu suala hili, lakini pia mimi nataka nije kwenye changamoto walivoiona kamati walipopita hasa ndani ya Wilaya yangu ya Wete. Changamoto iliyonekana pale Ofisi ya Mrasis wa Vizazi na Vifo ina ufinyu wa maeneo ya kukaa katika shughuli zao na kwa bahati mbaya humu walimo ni ndani ya Afisi ya Mkuu wa wilaya ya Wete, jengo lenyewe bovu haliridhishi.

Mhe. Spika, ofisi ile ina mambo mengi, ina mambo ya kutunza kumbukumbu za mtoto tokea atakapoanza kuzaliwa na kupelekwa kile kirisiti chake na kujaza zile fomu mpaka kufikia kupewa kile cheti cha kuzaliwa, lakini kwa bahati mbaya katika ule ufinyu ule uliojitokeza pale unafanya Ofisi nzima yote ile ikawa utendaji wake unazorota.

Mhe. Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri inafika wakati mtu pale anazaliwa mtoto anapeleka kile kirisiti anakwenda leo anaambiwa njoo baada ya wiki mbili, wiki mbili njoo mwezi, mwezi wa pili mpaka inafikia wakati kile kirisiti kinapotea sasa inakuwa ni tatizo kubwa la kupata kile cheti cha kuzaliwa, kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri katika hili kwa sababu sasa hivi watoto wetu wote tunakaa tunawapeleka skuli wakiwa wadogo tunakimbia kulea, tunawapeleka watoto wetu kulelewa katika skuli za chekechea. Mtoto anafika miaka mitatu au minne kwenda chekechea cheti hakijapatikana, sasa kuna kipindi tulipanda kama ni ukosefu wa magamba. Sasa

sijui mpaka leo magamba hayo bado hayajapatikana au vyenginevyo na hasa tatizo hili lipo Afisi ya Vizazi na Vifo Wete, Chake pia kuna afadhali.

Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri, katika hili alisimamie kuwapatia watu haki zao hizi ili tujue hasa mtu baada ya kuzaliwa na kupeleka risiti yake pale katika Ofisi ya Vizazi na vifo, ni muda gani atapata cheti kile ili kuondoa usumbufu, kwa sababu watu wetu wengi wanaishi vijijini maisha ni magumu, mtu kila siku anatoka Ole pengine anatoka Kojani, anatoka Mtambwe anakwenda Wete kwa kufuatilia, anapoteza muda mwangi mpaka anakata tamaa ya kupata cheti hichi.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye Chuo cha Mafunzo. Kama walivyochangia wenzangu Chuo cha Mafunzo ni ukweli usiofichika, nikisema hili mbali na kamati ilivyopita na sise pia kama Kamati ya Ustawi wa Jamii tumefika katika Chuo cha Mafunzo cha Wete, hali tulioikuta pale Mhe. Spika, hairidhishi kwa binadamu yeoyote wa kawaida kukaa pale. Majengo ni mabovu ya wanafunzi, askari wetu pia wanapata tabu, hata hiyo siku wanayotokezwa na hao wageni pale, basi hicho kijichumba kinachotakiwa kukaa pale kwa hao wageni ni chumba kidogo sana, hakikai hata viti vinane. Na bahati mbaya ile dari yote imeshatoboka, siku za mvua, mvua yote inawanyeshea ndani.

Kwa hiyo namuomba Waziri husika kwa sababu tunategemea hawa askari wetu wafanye kazi nzuri, na kazi waliyonayo ni ngumu, sasa na wao wanahitaji pahali pazuri pa kufanya shughuli zao.

Mhe. Mohammed Haji, alipozungumza alisema kuhusu tofauti ya gereza na mafunzo. Ni kweli tumebadilisha jina hili kuwa ni Chuo cha Mafunzo baada ya Gereza, lakini bado imo midomoni kwa vitendo tena. Kwa sababu ingekuwa ni mafunzo basi angalau ule ubovu na ile hali mbovu iliyokuwepo pale ingeondoka tukaona si gereza, lakini bado inaendelea kuwa ni gereza kwa sababu hali walizonazo ni nzuri sana katika maeneo mawili haya niliyopata kuyatembelea mimi pamoja na kuunganisha maneno ya Kamati; Wete na Kengeja.

Mhe. Spika, katika agizo Nam. 9 Kamati ilikubaliana na ushauri uliotolewa baadhi ya wanafunzi waliopo gerezani kwa kuwashirikisha wadau katika kurudisha ile hali ya zamani ya kuwa ni vyuo, ili wakitoka pale wawe angalau ni wajasiri amali. Wizara katika majibu yake imekiri na imekubali hilo, lakini mimi nataka niwaombe Wizara, kwa sababu wamelikubali hilo na vijana wetu wanaokwenda kule ni wengi mno na serikali inapiga kelele kila wakati vijana kujiajiri wenyewe. Sasa wakikaa mule ndani mtu atakaa mule ndani miaka mitano lakini akitoka baada ya kupanda mchicha na bilingani hajui jengine.

Mhe. Spika, nalitilia mkazo sana suala hili la kurudisha yale mambo ya zamani ya kuwa mafundi wa kufuma kama ni wanawake, kusuka mikoba, kushona, useremala ili wakitoka wao wenyewe watajajiri na pia watapata kuajiri vijana wengine.

Mhe. Spika, katika maagizo ya Nam. 11, katika wizara hiyo hiyo kamati ilishauri wizara ishirikiane na Wizara ya Katiba na Sheria kulitafutia ufumbuzi suala la mrundikano wa rumande wa magereza Kilimani. Idara kwa kushirikiana na Wizara imewasiliana na Wizara ya Katiba na Sheria kuwaomba majaji na mahakimu kufanya hivyo.

Mhe. Spika, wale watu wakikaa ndani kwa muda mrefu kuna gharama kubwa sana inazochukuliwa pale na bajeti zetu ni kama tunavyoziona, bajeti ni ndogo hazitoshi. Sasa mrundikano ule ukijaa mule ndani kuna gharama za chakula, kuna gharama za matibabu. Hii ni kuitia zaidi serikali hasara, jambo ambalo kila siku tunalamikia kwa sababu ya bajeti ndogo.

Kwa hivyo namuomba sana Waziri wa Katiba na Sheria kwa kulichukulia uzito wa hali ya juu hili, wale ambao tayari wameshakaa mule kwa muda mrefu na wana matatizo madogo madogo basi waondoshwe ili kuipunguzia mzigo serikali na Chuo kwa jumla.

Mhe. Spika, kwa sababu mambo mengi yameshazungumzwa naomba niishie hapa, nakushukuru.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, kwanza nikushukuru na mimi kwa kunipa fursa hii. Mimi nafikiri sitochukua dakika nydingi ili wenzangu japo mmoja apate kuchukua dakika zangu, ndio wajibu wetu ukiwa nacho kidogo msaidie mwenzako.

Nianze na ukurasa wa kwanza kwa haraka haraka, kifungu (c) kufuatia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kitaifa na miradi ya wananchi na Wizara husika. Hapa kidogo pana mushkeli na pana mashaka, kama ni kamati ilikuwa iangalie suala zima kutokufuatia miradi ya maendeleo hasa suala la wananchi. Wananchi kwa kipindi kirefu sasa wamekuwa na mashaka na suala la ajira. Kama juu ya suala hili ilikuwa likae, liangaliwe na lifuatiliwe kwa umakini suala hili.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika kuchambua mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya wizara husika juu ya mapato na matumizi ya kila mwaka. Kifungu (e) hichi ukurasa wa kwanza. Kamati suala hili ilikuwa iliangular vizuri kwa umakini katika utendaji wake.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nije nilipopakusudia hasa ukurasa wa (2) Ofisi ya Rais kwa upande wa Pemba bado inakabiliwa na tatizo la usafiri hadi hivi sasa. Idara ya Utawala Bora, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kweli gari ina thamani gani hata ikafika Ofisi kama hii nyeti haijaweza kupatiwa gari kitengo kama hichi. Ninachojua mimi gari ya *Noah* ni kama dola elfu mbili au elfu tatu. Ndio pale niliposema kuna mambo mengine kama hatujawa tayari serikali basi tusiwe tayari. Kitengo muhimu kama hichi gari ya dola elfu mbili, elfu tatu, mpaka muda huu haijapatiwa.

Mhe. Spika, ukosefu wa Ofisi Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi. Nilisema hapa miaka miwili iliopita au miaka mitatu iliopita wakati huo wizara hii iko kwa Mhe. Haji Omar Kheri, nikasema tusianzishe shughuli kama hatujawa tayari serikali, Mheshimiwa lakini hili suala uliangular.

Mhe. Spika, kutoka hapo ukosefu wa Ofisi ya *CAG* Pemba na changamoto zake. Hapa bado pana mtihani na nyengine changamoto serikali bado inakuwa haijawa tayari kwa nini wanakubaliana mambo haya, hapa nayo vile vile pana matatizo hayo.

Mhe. Spika, kubwa zaidi nije kwenye Ofisi ya Manispaa kunako soko la Marikiti ya kuchinjia kuku. Soko lile wananchi wanalipa shilingi elfu mbili, elfu tatu, wanapanga mboga zao, leo sijui miaka ishirini au miaka kumi na tano bado pana mtihani amba si mdogo, mabati ambayo hayafiki hata mia moja yanayohitajika kuezekwa vibanda vile, lakini bado watu na mvua hizi za masika zinazoendelea wanazidi kuvujiwa.

Nije suala la wafanyabiashara wa Forodhani. Kwa kweli kile wanachokilipa shilingi elfu 90 kwa mwezi ukilinganisha na biashara zao na hali inavyokwenda kwa kweli jambo hilo linatia uchungu na linatia huruma. Mkae mlifikirie, suala hilo, nimeshalipigia kelele kwa muda mrefu. Ukitazama pale ni meza tu wanayoiweka ingawa panahitaji usafi kidogo, lakini shilingi elfu tisini kwa hali ya biashara zinazokwenda pale kwa hali kwa kweli na hasa maisha haya tunayokwenda nayo na ukizingatia kwamba ajira ni ngumu. Hili suala likae lifikiriwe na serikali.

Tuje kwenye suala la *round about* ya Michenzani. Mimi nafikiri serikali pale ishushe pumzi zake iachie kusafisha eneo lile ni kupoteza pesa kwa muda mrefu. Nikitoka hapo Mheshimiwa nije hasa hapa kituo cha Daladala. Serikali pale sijui niseme imefanya kitu gani walichokifanya. Wakati gari tayari za daladala zipo zinakaa, leo sijui pale wamefanya nini, matokeo yake wanafunzi wanakosa kwenda skuli kwa wakati, madaktari wanakosa kufika kazini kwa wakati. Kile kituo pale wamekwenda kuweka gari zimewekwa tu, imekuwa wameondosha hili wameweweka hili. Mhe. Waziri, hili ulifikirie na pale kituo kilipo hivi sasa barabara yote ule ukuta wa Kisiwandui wameshapanda juu na kumeshachimbika, wananchi wanazidi kuumia, wananchi ndio serikali, serikali ndio watu.

Mhe. Spika, jengine hapa alipokuja Rais wa Ujerumani tulishuhudia mji wote ulikuwa safi, mji umeoshwa kwa maji. Kwa masikitiko makubwa yale makalbi pale Bandarini Malindi sijui kayarejesha nani, tunatoka pale tunarudi nyuma. Tumefanya nini makalbi yaliondolewa, leo yamerejeshwa tena, tunafanya nini? Tunapiga kelele humu, imekuwa kelele zote bure, kumpigia mbuzi gitaa, makalbi yale Mhe. Waziri, bora mukayaondoe, yamekuwa bugudha kati kati ya mji, watalii wanateremka pale wanaona uchafu kama ule. Kitu gani kilichofanyika kile, walipokuja Rais yameondolewa vizuri, leo yamerejeshwa tena, huu si usanii?

Mhe. Spika, taa za barabarani zimetiwa juzi sasa hivi nyengine hazifanyi kazi. Jengine katika Kamati yangu kuna kilio nyumba waliyoichukua JKU, Wizara ya Biashara wanaihitaji ile nyumba yao, imekuwa ni kelele za muda mrefu. Nafikiri Mhe. Spika, baada ya hayo nimemaliza.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Mhe. Spika, ahsante mimi Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, na kwa kuwa haya yaliyokuwemo humu tuliyaaandaa shirika. Na kwa kuwa wajumbe wengi wameshatoa michango ya kutosha nataka niseme maneno mawili madogo tu, nayasema haya kwa sababu yanetokea wakati tumeshafanya kazi za Kamati.

Moja Mhe. Spika, bado tuna changamoto kubwa *scale* za mishahara hili litakuwa linagusa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, tunalalamika sana kwa sababu tunalalamikiwa na wafanyakazi tunayafikisha yanapohusika. Wanajaribu kuyarekebisha lakini kazi ya kibinadamu haiwachi makosa. Kwa hivyo, pamoja na marekebiso yanayofanywa lakini bado matatizo yanaendelea kuwepo.

Kwa mfano hivi karibuni walijaribu kuwaangalia walimu wale amba wana *experience* ya muda mrefu wakawarekebisia. Lakini waliangalia wale walimu waliotimiza miaka thalathini tu, *regardless* elimu zao. Hicho ndio kilio kilichokuwepo kwamba mwalimu anamsomesha mtoto mpaka mtoto ana- *graduate* halafu anakuja anampita kwa mshahara ye ye anabakia kule nyuma, wamewaona. Lakini walimu wa miaka thalathini, kuna walimu kuanzia miaka 26, 28, 27, 25, hawaajaangaliwa na wao wanalia.

Sasa mimi nadhani utaratibu bora wangefanya hivyo wanavyokusudia kwamba *top* iwe miaka thalathini ndio kwenye *experience* kubwa ya kuangalia. Lakini hebu na washuke huku chini amba hawatimii miaka thalathini japo na wao wawagaie gaie ili hili tatizo liondoke. Kunakuwa kuna malalamiko mengi kwamba jamani hivi hawa waliokuwa hajafika hiyo miaka thalathini lakini wana miaka 20, 25, 28, wao hawajakuwa na uzoefu. Ndio nikasema kwamba kazi ya kibinadamu haiachi makosa.

Mimi nadhani watu wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma hebu na hili waliangalie. Pengine wakili *-solve* wakilipatia utaratibu hili haya manung'uniko yataendelea kupungua, hilo moja.

Mhe. Spika, la pili bado tunaendelea kupata malalamiko makubwa sana kuhusu Idara ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Idara hii inatoa vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi ambavyo vina faida kubwa sana kwa wananchi, wala sio faida moja ni faida kubwa sana. Tatizo linalotokea utaratibu huu wa kutoa vitambulisho una wadau wengi, moja katika mdau muhimu kweli kweli ni Sheha.

Mheshimiwa, tumejitahidi sana kusema na masheha, tumekuja mpaka kwa Mawaziri wao wakati huo alikuwa Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini, na hivi karibuni pia tulizungumza na Waziri wa sasa Mhe. Haji Omar Kheri na ye ye akatuahidi kuwa atalifanya kazi, lakini mpaka leo Mhe. Spika, manung'uniko yanakuja, masheha bado ni wagumu kuwapa watu huo utambulisho wao, kuna barua za utambulisho kumtambua kwamba huyu ni mwananchi wa shehia yangu ili asizuiliwe kupatiwa hicho kitambulisho, mpaka leo hilo ni tatizo.

Mheshimiwa hii nyimbo ni ya siku nyingi, ijapokuwa wenyewe wanakanusha, lakini tusingejiimba hii nyimbo bado tatizo lipo. Hebu Mhe. Waziri achukue *effort* zaidi kusema na hawa masheha, hatujui kwa nini masheha wanakuwa wasugu kiasi hichi Mheshimiwa kwa nini, hizi ni haki za watu. Siku nyengine mtu anaweza akakosa hata mirathi yake kwa sababu ya vitambulisho. Anaweza akakosa safari, na mambo mengi kwa sababu ya vitambulisho. Hebu tusiangalie upande mmoja tu, kitambulisho kinagonga mambo mengi, naomba hili lifikiriwe vizuri sana. Linaweza likaleta *chaos* baadaye katika nchi kwa sababu linaambatana na haki za watu.

Mhe. Spika, jambo jengine na niliseme kwa ufupi sana, mimi nakaa ule mtaa wa Mombasa pale na rafiki yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee, siku hizi tukishasali laasiri pale au ule wakati wa kwisha kusali laasiri pale kuna wenzetu wakristo sijui ni kanisa lipi lakini wanakuwa wanatia kanda, wanatuadhibu kweli kweli wakati wa kusali. Sasa waumini wa dini mbili zaidi tumo ni Waislamu amba ni karibu asilimia 99 na wenzetu wakristo amba wapo wachache, lakini tulikuwa na utamaduni wa kuheshimiana kwamba tusikerane.

Naiomba sana Ofisi ya Mufti, ilitafute hili Kanisa linalotia nyimbo wakati ule sisi tunasali laasiri wawakataze, hebu wafanye ibada zao kimya kimya kama sisi. Hii inakera watu Mhe. Spika, itafika siku watu watachoka kukerwa watafanya balaa. Naomba sana kabla hatujafika huko hebu turekebishe huu utaratibu.

Jambo la mwisho Mhe. Spika, limeshasemwa sana ni kuhusu maslahi ya wafanyakazi wa Ofisi ya DPP na sio maslahi yao tu mpaka bajeti yao ni finyu mno. Hii idara ni muhimu sana kwa kulinda haki za watu. Tulikwenda kule Mhe. Mkurugenzi akatalalamikia mpaka karibu alie. Watu amba wameshakuwa na uzoefu wa wanamsaidia sana

katika kazi za kusimamia kesi wanaondoka kwenye Idara yake wanakwenda kwenye Idara nyengine kwa sababu ya maslahi duni na mazingira magumu wanayofanyia kazi.

Mhe. Spika, tumeisema hiyo mpaka kwenye Kamisheni ya Utumishi wa Umma na wakatwambia kwamba tumewaangalia, lakini ni kweli wameangalia lakini hajatosha kwa sababu tunachotaka sisi ni kuona ile Ofisi ya *DPP* inapata ufanisi, kwa sababu nayo ni ofisi inayoambatana na haki za watu. Sasa wale watu ambao tumeshawasomesha wameshapata uzoefu pale wanaweza kufanya kazi vizuri, lakini sasa wakiangalia mazingira yao ni magumu.

Mhe. Spika, kuna jambazi moja hivi karibuni limepigwa pale Darajani likauliwa, yule bwana alikuwa hatari, kila Mwanasheria wa Ofisi ya *DPP* alikuwa anamu-*harass*, anamtishia maisha yake, anafanya hivi halafu anakwambia mtu huyo anakwenda kazini lakini hata usafiri hawana. Hebu tuwfikirieni hawa watu wanapata tabu sana na wataendelea kututoka kila siku.

Tunawasomesha kwa gharama kubwa kwa ajili ya kutusaidia lakini hatimaye kunakuwa na mazingira magumu ya kazi, wale watu wanaondoka pale. *DPP* atakuja kujishtukia hana hata mwanasheria wa kuwapeleka huko, ni hatari mno. Haki za watu zitaganda, kwa hivyo naomba sana kama ni Kamisheni ya Utumishi kama ni Tume ya Utumishi, kwa kweli wale watu waendelee kuwfikiria ili washawishike kubakie kufanya kazi katika mazingira yale magumu.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, nasema sina mengi kwa sababu hii hotuba ni ya kwangu naishia hapo, ahsante.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Musa:** Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo tukaweza kukturana hapa kwa ajili ya kuhitimisha au kuendelea na kazi ambazo tumejipangia ili kuleta maendeleo katika nchi yetu yaweze kufikia mustakbali wake.

Mhe. Spika, baada ya hapo nichukue fursa hii vile vile kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mambo mawili matatu yanayohusiana na ripoti ya Kamati inayoshughulikiana na masuala ya Katiba na Sheria, ambayo ripoti hii inajumuisha mambo yanayohusiana na Wizara tatu kama ambavyo Waheshimiwa Mawaziri walikuja kuwasilisha mbele yetu tokea juzi na jana yake vile vile.

Mhe. Spika, nijaribu kwenda ndani sana katika ripoti za Kamati na kimsingi nimekwenda takriban Kamati karibu zote. Nimegundua katika Kamati hizi au taarifa hizi kuna mambo ambayo yanaoana sana ambayo ni changamoto naweza nikasema au ni maagizo yaliyokuwa yametoka au mambo ambayo yanatakiwa yaelekezwe katika Wizara tofauti tulizonazo katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mambo hayo yalikuwa yanaelekeza zaidi katika masuala mazima yanayohusu bajeti, mambo ya usafiri, mambo ya upungufu wa wafanyakazi, lakini vile vile na vitendea kazi katika maeneo tofauti.

Nilipokuwa naendelea na kazi yangu ya utafiti kwa nini mambo haya yaweze kujitokeza katika utaratibu huu, nimepita katika maeneo mengi sana Mhe. Spika, ili kuweza kujua haya matatizo ambayo yanaoana, takriban kwa Ofisi zote. Kwa nini yanajitokeza kila katika Wizara ambazo tunazo katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa bahati nzuri nikapata wataalamu katika masuala ya Fedha wakanielewesha na kwa namna fulani nikaweza kupata na angalau muelekeo kwa nini tukawa tunapambana na matatizo haya ambayo yamekuwa ni endelevu katika Mawizara yetu mbali mbali Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwanza nilitaka kujua mapato yetu yanakusanywaje katika nchi yetu ya Zanzibar na vyanzo vyetu vya mapato ni vipi. Kwa bahati nzuri nimeweza kupata maelezo ambayo kwa namna fulani yameweza kuniweka pahala nikaweza kukubaliana na baadhi ya mambo ambayo yameonekana katika hizi taarifa ambazo tumekuja kuletewa hapa. Isipokuwa Mhe. Spika, kuna jambo moja tu ambalo linahusu wafanyakazi.

Jambo hili nahisi limo katika uwezo wetu sisi wenyewe kuwabidilisha wafanyakazi kutoka eneo moja kwenda eneo jengine, haya ni masuala ambayo tunaweza kuyafanya sisi wenyewe pasi na kupata gharama ambazo zitahitaji fedha nyingi kwa ajili ya kufanya mabadiliko ya watendaji hawa kutokana na kada ambazo zina upungufu wa watu hususan ukitalia maanani kwamba wako watu ambao wana uwezo zaidi ya eneo ambalo mtu analifanyia kazi, lakini

baada ya kwisha kufanya utafiti huo Mhe. Spika, nimeomba kutaka kujua mapato halisi yanayopatikanwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, wakati awamu hii ya 7 inaingia madarakani, Serikali yetu ilikuwa na uwezo wa kukusanya bilioni 13 na kidogo katika kipindi kile, lakini kwa sasa hivi Mhe. Spika, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusanya zaidi ya bilioni 25 na kuendelea mbele, pengine inawezekana ikawa kuna takwimu kubwa zaidi lakini mimi ninasimamia hapa kwenye *minimum* ya 25.

Vile vile kama ambavyo wenzangu walionitangulia walikuja kuchangia hapa na kutaka kufahamu kwamba sekta ambazo zinapaswa kukusanya mapato kwa nini zinatoa kauli kwamba zinakusanya zaidi ya yale malengo ambayo walikuwa wamejiwekea.

Hili nilipata jawabu na ukiangalia takwimu zetu Mhe. Spika, ZRB wanakusanya asilimia mia ya malengo yao ambayo wamekuwa wame tegemewa kukusanya au pengine zaidi. TRA wanakusanya zaidi ya asilimia 90 lakini vile vili kuna mapato madogo madogo ambayo yanatokana na Wizara za Serikali nazo pia Wizara hizi zina jukumu la kukusanya mapato ikiwemo Wizara inayoshughulika na masuala ya utalii, nayo vili vili inakusanya mapato yanakuja katika Serikali. Lakini hapo hapo tuna matatizo katika masuala ya GBS pamoja na misaada ambapo hapa sasa ndiko matatizo yetu yanapoanza kujitekeza katika masuala mazima ya kuweza kupata kuona haya mapato yetu yanakuwa viyi na yanatumika namna gani.

Eneo la mwisho ambalo linatuathiri vili vili Mhe. Spika, ni eneo la mikopo ambayo inatokana na wahisani. Sasa maeneo haya mawili ya mwisho haya Mhe. Spika, ni maeneo ambayo yanababisha ule ufinyu wa bajeti zetu kutokana na uhalisia wa matumizi ambayo tunayo ndani ya Serikali ambapo tunaendelea kutumia siku hadi siku katika kuendeleza mambo ambayo hayana budi kutekelezwa na Serikali hii, ili tuweze kufikia mustakbali ambao tulikuwa tumeutarajia.

Mhe. Spika, nikiachia eneo hilo naomba niende moja kwa moja sasa katika yale maneno ya hekima ambayo katika kampeni yetu ya mwaka 2010 ya tarehe 30 tulikuwa tumefungua chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein pale Kibanda Maiti mjini Unguja. Naomba kunukuu Mhe. Spika. Dr. Shein katika mkutano ule alizungumzia maneno yafuatayo naomba kunukuu Mhe. Spika:

"Nataka nitamke wazi bila ya woga wala kutafuna maneno yale yote yaliyotamkwa kwenye ilani ya CCM ya mwaka 2010 tutayatimiza kama tulivyoahidi mbele ya wananchi hata kama uwezo wetu utakuwa ni mdogo lakini ahadi hizi kwa mashirikiano tutazifiki. Naomba ndugu wanachama wa CCM na wananchi wapenda amani na wapenda nchi hii munipe kura zenu za ndio, ili niweze kuyatekeleza hayo". (*Makofî*).

Mhe. Spika, tukiacha maneno haya ya hekima ambayo mzee wetu alikuwa ameyazungumza lakini pia katika tathmini ambayo imefanywa juzi juzi tu kuitia hizi Bango Kitita ambazo huwa zinafanyika pale Ikulu kwa Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Spika, naomba kutamka sasa kwamba katika tathmini iliyo fanywa juzi imeonesha kwamba utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na yale maagizo ambayo yanatokea katika Bango Kitita yametekelezwa kwa asilimia 120. Hii inathibitisha kwamba yale mambo ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeweza kutekeleza mambo yote ambayo ilikuwa imejipangia pasi na kuwa na kigugumizi cha aina yoyote.

Mhe. Spika, inasikitisha sana, inahuzunisha sana, na si jambo ambalo linatarajiwa leo hii tunafika hapa anakujua kusimama mionganii mwetu, mmoja wetu anasema kwamba Serikali hii imeshindwa kutekeleza mambo ambayo ilikuwa inayataka wenyewe na wananchi watakuja kuihukumu Serikali hiyo. Serikali hiyo ni ya aina gani Mhe. Spika. Serikali hii kwa ajili ya makubaliano, na mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 2010 ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika nchi yetu, Serikali ambayo kuna Wajumbe kutoka vyama vyote vya upinzani pamoja na Chama Tawala ambavyo vina uwakilishi ndani ya Baraza lako Tukufu la Wawakilishi la Zanzibar Mhe. Spika.

Sasa ningependa vili vili kuwaeleza Wajumbe ambao wamo katika Baraza hili Tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla pale ambapo anapotokezea mijumbe atasema kwamba wananchi wataihukumu Serikali yao, ni Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa au kuna nyengine.

Kwa sababu Serikali hii ukiiangalia inaongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein lakini upande wa kulia kuna Maalim Seif Sharif Hamad na upande mwengine kuna Balozi Seif Ali Iddi, hapa ndio viongozi wakuu ambao wanaongoza Serikali ya pamoja Mhe. Spika. Sasa hizi kauli nyengine naomba vile vile ziwe zinabakishwa bakishwa tusimalize maneno katika kuzungumza.

Tukiacha hapa sasa Mhe. Spika, narejea tena katika ile hoja ya kwamba kwa nini Wizara za Serikali haziwezi kufikia malengo yake na kuweza kupata *OC's* zinazohitajika katika maofisi husika.

Mhe. Spika, mimi kwa masikitiko makubwa kabisa, nakubali kwamba kila binadamu ameumbwa na Mwenyezi Mungu akampa mitihani katika dunia hii ikiwemo maradhi na mambo mengine, lakini Mhe. Spika, nataka tufahamu kwamba katika matumizi ambayo ni ya lazima ambayo yanafanya na Serikali hii basi napenda nitamke bayana kabisa ni pamoja na matibabu ya wananchi wake ambao wamo katika Serikali hii pamoja na nchi hii ya Zanzibar kwa ujumla wao Mhe. Spika.

Ikiwa tunakwenda tukaweza kufika pahala tukaweza kutumia zaidi ya shilingi bilioni mbili na ushei kwa ajili ya matibabu, inawezekana ikawa kwa mtu mmoja tu, sasa hili hatuoni kama ni tatizo nalo pia.

Mhe. Spika, fedha za wananchi wa Zanzibar zinatumika zaidi katika matibabu yetu sisi wenyewe binafsi kwa watu mbali mbali ambao wanakwenda kufanyiwa matibabu katika maeneo tofauti. Na hili zaidi Mhe. Spika, tutakuja kulichangia itakapofikia ile ripoti itakayohusiana na Wizara ya Afya na mambo mengine, kuhusiana na suala hili juu ya mambo haya.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nitakwenda katika maeneo ya vikosi. Mhe. Spika, humu katika ripoti nilizozisoma kuanzia ukurasa wa 20 mpaka 28 kuna maeneo yalikuwa yanazungumzia juu ya bandari bubu. Kamati inaripoti kwamba kuna bandari bubu nyingi sana ambazo matumizi yake yanatumika katika utaratibu ambao kidogo ni mtihani kwa nchi yetu.

Na kama tunavyojuu Mhe. Spika, bandari ni sehemu ya mapato ya nchi yetu, ningeliomba sana pamoja na majukumu mengi na mikakati ambayo tumeipanga, Wizara zinazohusika zifanye kazi ya ziada kuhakikisha kwamba hizi bandari bubu zinadhibitiwa na kuona kwamba mambo yote ambayo au mizigo yote ambayo inaletwa katika nchi yetu inapita katika bandari ambazo ni za uhakika, ili mapato ya nchi yetu yawewe kupatikana kama ambavyo taratibu zetu tumejiwekea katika nchi hii.

Jengine ambalo Mhe. Spika, nilikuwa nataka kulichangia, jana kuna baadhi ya Wajumbe wanachangia hapa nilisikikitishwa sana na nikawa niko *very much interested* kufuatilia lile suala ambalo lilikuwa limeulizwa hapa juu ya masuala mazima ya mali ya wakfu ambao uongozi ulikuwa umetatizana katika maamuzi juu ya suala lile.

Katika jambo hili nitaiomba Serikali baadae ije itufahamishe zaidi nini hasa kimejiri katika lile eneo la Pemba ambalo hapa Mkuu wetu wa Shughuli za Serikali humu ndani na MwenyeKITI wetu Balozi Seif Ali Iddi ilisemekana kwamba yeze alikuwa ametoa kauli juu ya kauli kwa Waziri wake ambayo alikuwa tayari ametoa maelekezo.

Mhe. Spika, mimi nimefuatilia suala hili na nikagundua kwamba ilikuwa kuna matatizo yametokezea kwa eneo ambalo tayari wananchi wanakaa na eneo lile likaja likawekwa vibao baadae na kuelekezwa kwamba eneo lile lilikuwa ni la wakfu na mali ya amana, wakati tayari wananchi wako pale wanaishi na shughuli zao.

Alichokifanya Makamu wa Pili wa Rais ilikuwa ni kwenda na kuweza kuondosha pale ile hatari ambayo alihisi inaweza kutokea katika eneo lile. Sasa baadae naiomba Serikali sasa ije itoe ile hadithi hasa inayohusiana na eneo lile na kadha ambayo ilikuwa imejitokeza hata ikapelekea kwamba Makamu wa Pili wa Rais aweze kutoa maamuzi ambayo mwanzo ni maamuzi mengine na yale aliyokuja akatoa yeze akatoa kwa ajili ya kunusurisha matatizo ambayo yangeliweza kutokea katika eneo lile.

Baada ya maelezo hayo sasa Mhe. Spika, na kwa kuzingatia muda wako ulikuwa umenipa nakubaliana na naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma:** Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuamka salama asubuhi ya leo na sasa hivi kupata wasaa mdogo huu wa

kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa. Kwa bahati ninashukuru sana waheshimiwa ambao walichangia hoja yetu ni:-

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk  
Mhe. Ismail Jussa Ladhu  
Mhe. Abdalla Mohammed Ali  
Mhe. Ali Salum Haji  
Mhe. Abdalla Juma Abdalla pamoja na wengine ambao wamechangia kwa ujumla kwa wizara nyengine.

Hoja za kimsingi Mheshimiwa zilielekezwa sana katika masuala ya nyaraka. Ninashukuru Mhe. Mshimba bahati mbaya hayupo lakini nitajibu hivyo hivyo, alizungumzia suala zima la nyaraka na hali ya karatasi zetu zilivyo na afya ya wafanyakazi.

Mheshimiwa tumefanya juhudini kubwa, kwa ujumla wale wote waliozungumzia nyaraka, hata hivyo nimesikitika sana Mheshimiwa mmoja aliposema kwamba Serikali hajui thamani ya nyaraka. Si kweli kwamba Serikali hajui thamani ya nyaraka. Laitani ingekuwa hajui thamani ya nyaraka leo tusingeweka ma-CCTV cameras pale tukaweka maposhoto maalum kwa wafanyakazi wetu wanaofanya kazi katika maeneo yale nyeti kwa ajili ya kukinga afya zao na kuwasaidia wapate nguvu kidogo.

Kwa hivyo si sahihi kusema kwamba Serikali hii haithamini, hajui umuhimu wa nyaraka, tunajua umuhimu wake na sasa hivi ningewaomba Waheshimiwa wale ambao walihisi hivi kwamba nyaraka zile hatuziangalii vizuri basi wangekwenda Idara ile yetu ya Nyaraka, wangeona jinsi gani wafanyakazi wetu wanavyojituma kufanya kazi asubuhi na jioni kwa ajili ya kutunza nyaraka zile.

Na ushahidi wa hayo Mheshimiwa mimi nilitembelea nyaraka hivi karibuni, nimeona nyaraka nyingi sana na ninashukuru mionganoni mwa nyaraka ambazo zimeonekana ni msahafu ule ambao umetembezwa sana kwenye mitandao ni sahihi, ingawa kuna taarifa kidogo ambazo zinataka marekebisho.

Msahafu ule uliokutikana mwanzo wake ultoka Makunduchi baadae ukaenda Tumbatu. Na huko Tumbatu sio kwamba ulifukiwa lakini ulikuwa kwenye msikiti, baadae msikiti ule ukaanguka na ukageuka gofu, ndio katika kufukua kufukua katika kutazama magofu yale ndio ukakutikana msahafu ule, baada ya kupatikana umerejeshwa nyaraka.

Upo pale msahafu ule wa historia Mheshimiwa karibu miaka 700 na zaidi na wanaotaka kwenda kuona wakautizame uko katika hali nzuri sana, mimi ninawapongeza sana vijana wetu wameuangalia vizuri na wanaendelea kuuangalia vizuri ingawa tumeuficha, lakini ukienda kwa maombi maalum utaoneshwa.

Lakini la pili Mhe. Ismail nizungumzie suala zima la Qatar. Kwanza nataka nthibitishe kwamba ziara ya Qatar aliyoifanya mwanzo kwenda Qatar alikuwa Waziri wa Kazi na Uwezesha jiji wakati ule. Nilipata mualiko na mualiko ule bahati nzuri nilisema hapa nimealikwa na mwenyewe mfalme, kwa faida ya waheshimiwa nilialikwa vipi na mfalme na mimi ni kijana mdogo sana.

Mfalme wa Qatar yule ambaye ameondoka sasa hivi, Sheikh Hamad alikuwa mapumzikoni Zanzibar, alipokuja mapumziko Zanzibar akawa amekuja kupumzika. Kwa bahati nikapewa heshima mimi ya kwenda kumpokea, katika kumpokea bahati nzuri ninajua kusema *please* na *thank you*. Kwa hivyo nikazungumza nae kwa kuanza na *please* na baadae nikamwambia *thank you*.

Maana yake akanambia sasa umekuja kunipokea hapa na mimi nitafanya njia nikupokee kule Qatar. Kwa hivyo ni kweli Disemba akanialika mwaka 2012 na mimi nikaenda zangu Qatar nikakutana naye na akanikutanisha na Waziri anayehusika na mambo ya kazi. Ni vizuri kutoa hii historia kidogo na tukaandaa utaratibu mzima baadae ikaja timu kutoka Qatar ikaja Zanzibar ikawa tunaita *Qatar Foundation* lakini hapa tukataka tuanzishe *Zanzibar Foundation*. Masuala ya elimu, afya na mambo ya empowerment pamoja na masuala mazima yanayohusiana na vijana wa Zanzibar kwenda kufanya kazi Qatar.

Mwaka huo uliofuata 2013 katika mkutano wa *ILO* nikakutana na Waziri anayehusika na masuala ya kazi au ajira tukazungumza vizuri sana mimi na yeche na tukakubaliana kimsingi kwamba Zanzibar na Qatar tuwe na mahusiano

katika masuala ya *labour*. Wakati tunaandaa utaratibu ule baadae tukapata taarifa kwamba wenzetu Tanzania Bara na wao wamefanya mawasiliiano na Qatar.

Sasa kilichotendeka ni kwamba Qatar wakatia saini na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kuweka saini ile mimi nikafuutilia zaidi ilikuwaje? Lakini kilichofanyika ni kwamba Wizara ya Mambo ya Nje ndio iliopewa jukumu la kusaini kwa niaba ya Tanzania juu ya utaratibu wa masuala yanayohusiana na mambo ya kazi na ajira kwa vijana wetu kule.

Lakini tulikataa moja kwa moja kwamba Waziri wa Kazi kule asisaini kwa sababu tukasema hilo sio suala la Wizara ya Muungano. Masuala ya kazi sio ya Muungano ni suala ambalo linahusu Zanzibar mbali na Bara mbali, na ndio maana yake akaenda akasaini Waziri wa Mambo ya Nje kwa niaba yake Naibu Waziri akaenda akasaini Mhe. Mahadhi.

Hata hivyo, pamoja na yote hayo mwaka 2014 tulikutana tena nae Waziri huyu wa mambo ya *Labour* akaniambia lile suala limefanyika huko kwa Tanzania lakini tungependa sisi tufanye kwa Zanzibar, na hivi tunaandaa utaratibu wa jinsi gani na Mungu akinijaalia Mhe. Spika leo jioni naelekea huko huko na natarajia kuonana nae huyo Waziri wa Mambo ya *Labour* wa Qatar *inshaallah* tutafanya hiyo kazi.

Nashukuru sana ziara ya Makamu wa Kwanza aliyoifanya kwenda Qatar, kenda kuyakumbusha yale ambayo tayari tulikuwa tushayafanya, lakini napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba Zanzibar itaendelea kushirikiana na Qatar na tunaendelea kufanya mahusiano yetu ya karibu na kuona kwamba moja kwa moja Zanzibar kwenda Qatar isiwe ni tatizo. Na tutafanya hivyo kwa sababu masuala ambayo si ya Muungano hatuna ulazima wa kushirikiana katika masuala kama hayo. Kushirikiana si jambo baya lakini hatulazimiki kwa masuala ambayo si ya Muungano, na hasa Katiba yetu mpya ndiko inakotuelekeza huko.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa na Mhe. Ali Salum nyaraka na athari zake ndio lile ambalo nimelizingumzia mwanzo, kwamba tunajitahidi na sasa hivi tumeanzisha utaratibu wa kutoa posho maalum kwa kila mfanyakazi ambaye anafanya kazi katika sehemu nyeti kama zile.

Mhe. Abdalla Juma ye ye kazungumzia suala zima la maslahi. Yeye ni mwalimu na anaendelea kuitetea kada ya walimu, na mimi namshukuru sana ye ye ni Mijumbe wa Kamati. Sasa maslahi yameangaliwa kwa walimu wa miaka 30.

Mheshimiwa tuliowaangalia si miaka 30 ni wale *experienced teachers* wengi tu tumewaangalia isipokuwa ni kweli kilichojitekeza ni nini? Tuliowaangalia zaidi ni wale walimu ambao *form IV* miaka mingi sana, miaka 30 wamefika wengine kweli tukawatengenezea mambo yao mazuri, tukasahau kuna wengine walijiendezea kipindi hiki ambao sasa hivi wameshapata *diploma* na wameshajiendezea miaka mingi sana karibu miaka 20 au 25. Sasa hivi na wao tunawatengenezea na *inshaallah* siku si nyingi mambo yao yatakuwa mazuri vile vile.

Jambo hilo limewagusa wengi na tunarekebisha hali hiyo kwa wao na wengine na hata hawa wafanyakazi wa Ofisi ya *DPP* tunaliangalia na tunatarajia tutalifikia uamuzi wake si muda mrefu kuanzia sasa hivi.

Mhe. Spika, kwa upande wangu sikupata masuala mengi sana wala sikupata hoja nyingi, hii inaonesha kwamba vijana wetu wizara yetu wanajitahidi kufanya kazi vizuri na *inshaallah* naomba waendelee kufanya kazi hivyo na nawoomba waheshimiwa waendelee kushirikiana na sisi.

Nimalizie kwa kuishukuru Kamati hii yetu ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri waliyoifanya, na sisi tuko tayari wakati wowote kusikia ushauri wao, lakini naomba tuendelee kushirikiana tukiwa kule ofisini kwetu na tukiwa hapa Barazani, tuwe kitu kimoja kama hivi tulivyofanya leo. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuja kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja na maelezo ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia utekelezaji wa ofisi yangu ambao tuliagizwa na kamati katika kipindi kilichopita.

Mhe. Spika, waliopata nafasi ya kuchangia ni watu 12 kwa upande wangu, watu hao waliopata nafasi ya kuchangia ni:

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
3. Mhe. Abdallah Mohammed Ali
4. Mhe. Subeit Khamis Faki
5. Mhe. Marina Joel Thomas
6. Mhe. Rufai Said Rufai
7. Mhe. Ali Salum Haji
8. Mhe. Mohammed Haji Khalid
9. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
10. Mhe. Farida Amour Mohammed
11. Mhe. Abdalla Juma Abdalla na
12. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Watu 12 wamepata nafasi ya kuchangia hoja ya utekelezaji wa majukumu ya wizara yangu kama nilivyokwisha kusema hapo awali.

Na mimi nianze kwa kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mashirikiano mazuri ambayo wamekuwa wakitupa toka kamati hii ilipoteuliwa kushughulikia wizara yangu.

Pia niwashukuru kwa maelekezo na maagizo ambayo wamekuwa wakitupa na hatimae sisi kuyatafutia majibu yanayostahiki kuweza kutoa ufanuzi.

Mhe. Spika, watu wote 12 kwa ujumla wamekuja na hoja nyengine zilikuwa zinafanana na nyengine zilikuwa hazifanani, lakini nitajaribu kutoa ufanuzi kwa kadri ya nitakavyoweza kuzitolea ufanuzi hoja hizo.

La kwanza ambalo liliibuka kwa baadhi ya Wajumbe ni suala ya kituo cha daladala kwamba ni kero, ijapokuwa lugha hii huwa haipendwi lakini ndio utaratibu wa kiserikali lazima tuseme hivyo.

Jambo hili kimsingi na kisheria wajumbe wengi ufahamu wanaona kama ni jambo la Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Kwa mujibu wa sheria ya usalama barabarani ni jambo la Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe kwa kuthamini michango yenu jambo hili lilipokuwa linalekezwa kwangu nilijaribu kutafuta utaratibu wa kisheria nikaligundua jambo hili linasimamiwa na Wizara ya Miundombinu.

Hata hivyo, mimi kama serikali, kama Waziri wa Serikali sikukwepa jukumu la kusema kwamba jambo hili ni la wizara hii na niiachie wizara hii. Serikali kama mnayotukumbusha siku zote tunafanya kazi kwa pamoja kama mawaziri tukiwa ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Nilichukua hatua ya kumuandikia waziri mwenzangu wa Miundombinu tukafanya vikao ili tuelewane kuhusu jambo hili. Nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba jambo hili tumelishughulikia na hivi karibuni tu basi litapata ufumbuzi wa yale maamuzi namna tulivyoyaamua. Kwa hiyo, wale wote waliochangia jambo hili kwanza wawe na uelewa, na hata wale wanaouliza maswali kuanzia sasa kuhusu jambo hili masuala yao wayaelekeze kwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ndiye mwenye sheria anayesimamia suala hili na sio Baraza la Manispaa.

Baraza la Manispaa kuititia ofisi yangu kazi yangu ni kuendesha baada ya wao kuweka ama vituo vya daladala ama vituo vya kupakia abiria, hiyo ndio shughuli yangu mimi. Shughuli za *operations* za kila siku ndio kazi zangu mimi lakini shughuli za kuainisha wapi kituo kiwepo au wapi stendi iwepo ni shughuli ya miundombinu na mawasiliano.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo limejitokeza kwa uchungu sana ilozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni juu ya suala la usafi wa mji.

Na mimi nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kwamba nitoe hadhithi moja Mwalimu Haroun huwa anatoa sana ya yule jamaa mmoja wa Makunduchi aliyeshtakiwa akaambiwa hata sabuni haleti. Jibu lake likawa *sabuni naleta hela halu tu*.

Kwa hiyo, Baraza la Manispaa linajitahidi kuimarisha usafi, lakini wakati mwengine lazima tukiri tunazidiwa kutokana na changamoto zinazojitokeza, na hizi changamoto Waheshimiwa Wajumbe kusema tunazimaliza kabisa mimi sijui tutafanya miujiza ya namna gani, lakini tutajitahidi tukabiliane na tatizo hili.

Tatizo liliopo ni kwamba katika kipindi cha mwezi mmoja nyuma tumepata tatizo la magari yetu mawili ya *compactor* kuharibika, na kwa bahati mbaya magari yale *spare* zake zinapatikana nchini Uhlanzi. Tumejaribu kwenda kwa *dealers* wote lakini tumeambiwa lazima tuagizie huko. Kwa hiyo, tunaomba radhi wananchi wa Mji wa Unguja kwa kadhia ambayo imejitokeza.

Hata hivyo, nilipokuwa nikijibu swalii hili katika siku za nyuma nilikuwa nikisema kwamba tunayo magari ambayo tumeyapata kupitia mradi huu wa *ZUSP*, magari yalifika lakini kukawa kuna tatizo la vifaa vya kunyanyulia vikapu.

Napenda niliarifu Baraza lako Tukufu kwamba vifaa hivyo vilishafika kupitia wizara ambayo ilifanya shughuli hii na tumeshakabidhiwa rasmi, na zoezi la kuweka vikapu kwenye majaa litafanyika kuanzia sasa na suala liliopo la kadhia ya taka tunapenda tuwaahidi wananchi wakaazi wa Mji wa Zanzibar kwamba hili litaondoka ndani ya wiki hii kabla ya Jumapili *inshaallah*.

Suala jengine ambalo limeelezwu kilichoonekana na hili amelizungumza sana rafiki yangu Mhe. Ismail Jussa kwamba badala ya kuona yale mambo aliyoahidiwa yanafanyika wameona vikuta vikajengwa katika majaa. Ni kweli kazi hiyo ilikuwa ni sehemu ya uimarishaji wa uzoaji taka ndani ya mji wa Zanzibar. Kwa nini? Vile vikuta vilivyojengwa maana yake ndipo yatakopakaa yale makontena ambayo yanatakiwa yawekewe taka baadae yaje yale magari yaje kunyanya na kupeleka kwenye jaa kubwa. Kwa sababu hivi ni vituo vya kupokelea taka kutoka kwenye maeneo ya wananchi, na kwa hili mtatuwia radhi kutokana na hali halisi ya mji wetu ulivyopangika mpaka hapo baadae.

Na ni imani yangu Wizara ya Mipango Miji imeshakamilisha kazi hii, tutakapoona sasa mji wetu tunaupanga vipi. Ni kwa vyovoyete vile vituo vya kupokelea taka vitakuwepo ndani ya maeneo yetu, tunachotakiwa sisi watu wa Baraza la Manispaa kupitia ofisi yangu kuharakisha kuzizoa taka kwa wakati na Mungu akipenda tutajitahidi.

Vile vile naomba wananchi waelewe tuna majaa 62, tuna magari 7 ya kuzolea taka, lakini jaa kubwa la kutupia taka liko Kibebe ni maili ngapi kutoka Mjini mpaka Kibebe. Gari 7, majaa 62 uzalishaji wa taka umeongezeka. Serikali inachowenza kusema kuwaambia wananchi wa Zanzibar kwamba itajitahidi kuongeza magari kwa ajili ya uzoaji wa taka na itajitahidi vile vile kulipa uwezo Baraza la Manispaa ili lipate fedha kwa ajili ya kutoa huduma hiyo kwa wananchi.

Pia nataka nitoe wito kwa wakaazi wa Mjini Unguja nao washirikiane na wafanyakazi wa Baraza la Manispaa ili kuhakikisha kwamba taka zinazolewa.

Limejitokeza suala la kwamba wafanyakazi hawana vifaa. Ni kweli hata mimi nimepita lakini wafanyakazi hawa baadhi yao tabia yao sio nzuri. Ndani ya miezi mitatu hii wamepewa vifaa vyote hivyo, wamepewa *rain boots*, wamepewa *gloves* za kuvala mikononi, wamepewa *overalls*, wamepewa *overcoats*, wapepewa *helmets*, wamepewa kila kitu lakini wanauzu. Serikali haina upungufu huo wa kutokuelewa afya za wafanyakazi wake, lakini tatizo ni hilo.

Ninalotaka kuwashakikishia sasa hivi nitashirikiana na uongozi wa Baraza la Manispaa wakati tunawapa wafanyakazi vifaa hivyo tufunge nao mkataba, na tukibaini kwamba kuna mfanyakazi ambaye ameuza vifaa hivyo basi tutamchukulia hatua za kinidhamu, ama kumkata fedha zake katika mshahara wake, lakini hili ni jambo kweli kama Mhe. Ismail ulivyosema wafanyakazi wanazoa kwa mikono lakini si kusudio la serikali wala Baraza la Manispaa, wanauzu. Kwa hiyo, mimi nataka niseme waache tabia hiyo kwa sababu si jambo zuri, matokeo yake inaonekana kama serikali haiwajali.

Limezuka suala la kuwapima afya zao. Wanapimwa afya zao wafanyakazi na wengine wamekuwa na tabia ya kukimbia kwenda kupimwa afya zao kwa kuhofia pengine wakigundulikana wana matatizo pengine wanaweza

wakaambiwa kazi basi. Sasa mimi nadhani serikali yote haya inayafanya kwa lengo la kuwapenda wafanyakazi wake.

Ni kweli tatizo la *overtime* lilikuwa halijaratibiwa vizuri, lakini unalipa *overtime* kwa yule mfanyakazi ambaye anafanya kazi ya kawaida kwa mujibu wa sheria halafu saa za ziada afanye kazi ya *overtime*. Wafanyakazi hawa wengine wanaingia kwa *shift* lakini wengine kutokana na tatizo ambalo liko ndani zaidi kwenye Baraza lenyewe wanakuwa wanakimbia kazini, lakini hata hivyo jambo hili ni langu nataka nilihakikishie Baraza kwamba nitalisimamia kwa wale wafanyakazi ambao wanaonesha uzembe basi tuweze kuwachukulia hatua za kinidhamu, lakini kwa wale wafanyakazi watakaokuwa wanafanya kazi za *overtime* nataka niwhakikishie kwamba watalipwa *overtime* zao.

Tatizo tulikuwa nalo kweli la upungufu wa fedha kama tunavyojuwa kwamba huko nyuma serikali ilikuwa inatupa ruzuku ambayo haitoshelezi kulipia mishahara yote ya wafanyakazi wa Baraza la Manispaa. Hivi sasa serikali inatupa mishahara kamili kwa wafanyakazi wote wa Baraza la Manispaa, na lengo lilikuwa zile fedha ambazo tunazikusanya ziweze kuingia katika shughuli za operesheni na shughuli nyengine za kulipa maslahi mengine ambayo hayaendani na mshahara unaotokana na *pay role* ya serikali. Kwa hiyo, hilo jambo nimelisikia naomba nimhakikishie Mhe. Ismail Jussa kwamba tutalichukua na tutakwenda kulifanya kazi kwa madhumuni ya kuona kwamba yule ambaye anafanya kazi ya *overtime* anapata haki hiyo ili tatizo hili liweze kuondoka.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, amezungumza mambo mengi mengine sitaki niyazungumze, mimi nataka nimthibitishie tu kwamba serikali hatujashindwa kazi kama tungeshindwa kazi si aibu mtu kusema nimeshindwa. Mimi mmoja siku nikishindwa kazi basi nitakwenda kwa miguu kwa Rais nikamwambie nimeshindwa kazi aniondoe, lakini muda huo bado haujafika ukifika nitafanya hivyo. Lakini kwa maana ya Serikali ya CCM bado serikali yetu haijashindwa kazi, kwa maana ya Serikali ya Mapinduzi yenyenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa bado hatujashindwa kazi. Sasa mimi sina namna ya kuzungumza vyenginevyo katika hili ningeomba niishie hapo.

Vile vile limejitokeza suala la maslahi madogo kwa askari wetu. Ni kweli suala hili lipo hata mimi waziri nalitambua, serikali nzima tunalitambua, Mhe. Rais na wasaidizi wake wanalitambua. Tumejaribu mara zote ambapo serikali imefanya marekebisho ya mishahara ya wafanyakazi wa serikali basi maslahi ya wapiganaji yamekuwa ni juu zaidi kuliko wafanyakazi wengine wa kawaida kwa kufahamu umuhimu wa wapiganaji wetu.

Ninachowea kusema kwamba bado serikali inaangalia zaidi uwezekano wa kuweza kuwaongezea wapiganaji wetu maslahi mazuri zaidi pale hali itakapokua nzuri, hatuna namna nyengine ya kufanya nje ya bajeti ya serikali, kwa sababu katika jambo ambalo huwezi kupata mtu akakusaidia ni jambo la mishahara ya watumishi wako. Kwa hiyo, serikali itaendelea na juhudhi zake za kukusanya zaidi na kupanga vizuri zaidi ili wapiganaji waweze kupata maslahi mazuri.

Suala la fedha za uhamisho ni kweli wapiganaji wetu mpaka sasa tunawapa pesa za nauli kwenda kule ambako tunawapeleka na hatimaye kama anahamishiwa familia yake idara inachukua jukumu la kuweza kuhamisha vile vifaa ambavyo anakwendanavyo. Lakini kwa sasa ni kweli askari wanapewa nauli badala ya kupewa zile pesa za uhamisho na ni kwa sababu ya ufinyu tu wa bajeti na ufinyu wa bajeti sote tunauelewa. Kwa hiyo, mpaka pale serikali itakapojipanga vizuri katika kuwa na bajeti nzuri bila kutegemea misaada kutoka nje, basi nadhani hili tatizo linaweza likashughulikiwa.

Hata hivyo, wizara yangu ina mpango madhubuti wa kuona kwamba jambo hili tunaweza tukaliingiza kwenye bajeti ya mwaka huu ili tuondokane na kadhia ambayo ipo kwa askari wetu, kusafiri na kutangulia katika vituo vyao vya kazi na familia zao zikachelewa kwa muda baadae zikawafuata kwa muda mrefu. Tunatafuta ufumbuzi wa kuweza kushughulikia jambo hilo.

Mhe. Spika, suala la majengo yawe ya makaazi ya askari na hapa zaidi kimezungumziwa Chuo cha Mafunzo. Nataka nitumie nafasi ya kufafanua suala la kubadili jina ambalo amelisema Mhe. Mohammed Haji Khalid. Hili ni jambo la kisheria, pale tutakapopokea mawazo kutoka kwa wahusika kwamba sasa tubadili jina inabidi kwanza tubadilishe sheria, hatuvezi kubadili jina la taasisi hii kwa maoni tu ambayo utaniambia waziri halafu mimi nikwambie tumekubali, lazima twende kwenye sheria halafu ndipo tuweze kubadili jina hili, kwa sababu jina hili lipo kwa mujibu wa sheria.

Kwa nini Chuo cha Mafunzo? Chuo cha Mafunzo ni taasisi, jengo la Chuo cha Mafunzo ni gereza hakuna anayebisha, lakini jina la taasisi ni Chuo cha Mafunzo jengo ni gereza, anayekwenda kule pamoja na kupewa mafunzo lakini kwa mujibu wa sheria za Zanzibar anatumikia kifungo. Kwa hiyo anakwenda kule kwenye vyuo vya mafunzo lakini atalala ndani ya gereza.

Majengo ya Magereza kuwa na hali mbaya na mimi sitaki nibishane na Waheshimiwa Wajumbe kila aliye kwenda anatambua hali hiyo. Lakini lazima tuseme yapo mambo ambayo tumeyaimarisha katika kipindi hiki. Kwa mfano, vyoo tumeviimarisha na kila jengo jipya tunalojenga sasa haliwi na utaratibu ule wa zamani wa mtondoo hapana, tumerekebisha kwa sababu tunakwenda na wakati.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe mimi kama sasa hivi nataka yale yawe kama sawa sawa na *villa* zile zilioko katika maeneo mengine. Nitoe hadithi moja ambayo niliwhi kuipata kutoka kwa Mzee wetu mmoja kwamba huku hendi mmoja.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa tuzingatie na muda.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Ahsante sana, huku hendi mmoja. Niliwhi kupata hadithi kule Afrika Magharibi kulikuwa na Waziri wa Fedha na Waziri anayeshughulikia Vyuo vya Mafunzo. Waziri anayeshughulikia Vyuo vya Mafunzo akamwambia Waziri wa Fedha nipe pesa niimarishe magereza, kwa bahati mbaya bajeti za nchi zetu za Kiafrika ndio hizo hizo, ikatokezea siku serikali ili yopo madarakani ikapinduliwa. Waziri wa Fedha na Waziri wa Vyuo vya Mafunzo wote gerezani, Waziri wa Fedha kwa sababu ya fedha kidogo hayuko mkakamavu kufika kule analia *portion* ile ya chakula ambacho amepewa, Waziri wa Magereza bahati nzuri mimi sina, ye ye yuko *very strong*; akamwambia nilikwambia unipe pesa sasa unaona zile pesa kama ungenipa sote leo tungefaidika na pesa zile ambazo umenipa.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe nashukuru kwamba mtaendelea kutupigia debe ili tupewe fedha tuimarishe Vyuo vya Mafunzo kwa sababu kule hakuna mmoja, nataka nimalizie hapo.

Mengine kwa sababu ya muda nasema hakuna Mkuu wa Chuo cha Mafunzo Pemba asiyeshirikishwa katika kupanga bajeti ya Vyuo vya Mafunzo. Kamanda wa Vyuo vya Mafunzo ni Mjumbe wa Kamati Tendaji na ni Mjumbe wa Kamati ya Uongozi ya Chuo cha Mafunzo. Chuo cha Mafunzo kinapoandaa bajeti kinakaa na wakuu wake wa idara na *section* zote. Kwa hiyo, suala la kwamba hashirikishwi halipo, inawezekana wakati wa ile *OC* inapokuja kwa mujibu wa mgao pengine muda huo ukawa haupo, lakini wakati wa kupanga bajeti lazima ashirikishwe. Ningemuomba Mhe. Rufai Said Rufai suala hili aelewé kwamba hakuna kiongozi yoyote ambaye hashirikishwi.

Kwa haraka haraka nataka nzungumzie suala la ufinyu wa bajeti. Suala la ufinyu wa bajeti ni kweli, mapato yanayokusanya yameongezeka lakini kuna tatizo la upatikanaji wa fedha. Ni tatizo kweli na tatizo hili haliko katika nchi yetu tu ya Zanzibar, katika nchi zetu nydingi zinazotegemea misaada na mikopo kutoka kwa wahisani. Zanzibar ni sehemu ambayo inategemea fedha za *GBS*, kwenye bajeti yetu kulikuwa na shilingi 40 bilioni kusaidia bajeti ya Zanzibar, mpaka muda huu tunazungumza Waziri wa Fedha atakuja kuzungumza vizuri zaidi tumepokea shilingi bilioni saba tu katika 40.

Kwa hiyo, yale maeneo ambayo yalipangiwa yapewe fedha kuititia *OC* kiwango chake kimeshuka. Hilo ni tatizo na tatizo hili si kwamba serikali inakusudia lakini kutokana na hali halisi ya makusanyo na ile bajeti imebidi zaidi isambazwe katika maeneo mengine muhimu zaidi tugawane kidogo kidogo naweza nikasema hivyo.

Kwa hiyo, niwaombe Wajumbe, serikali katika kukabiliana na hili mwaka huu tunakuja na utaratibu, Waziri wa Fedha atakuja kueleza zaidi, zaidi kupanga mambo yetu kutegemea bajeti na makusanyo tunayokusanya ndani kuliko kutegemea hii mikopo na misaada kutoka nchi za nje. Hatusemi kwamba tunaacha, lakini tutajihakibiza kwanza kwa kuangalia makusanyo yetu na uwezo wetu wa ndani kuliko kutegemea uwezo wa nje. Kwa hiyo, mambo hayo yakikamilika basi na sisi watu wa *local government*, watu wa vikosi na watu wa idara maalum tutafaidika na hilo.

Mhe. Spika, la mwisho kuhusu suala la Tume ya Utumishi Idara Maalum kuwa na eneo finyu. Nakiri kutokea hivi lakini, ofisi zetu takriban zote tunalo tatizo la ufinyu wa nafasi. Serikali tunaendelea na mikakati yetu ya

kuhakikisha kwamba ofisi zetu zote zinapata majengo na maeneo ya kuweza kufanya kazi vizuri. Katika wizara yangu tunao mpango mkubwa tu wa ujenzi wa ofisi tukimaliza mpango huo tunategemea tatizo hili litamalizika.

Kuhusu bajeti ya Tume ya Utumishi Idara Maalum, kama zilivyo tume nyengine serikali mwaka huu itawapa *vote* maalum badala ya kutegemea ile kasma ambayo iko wizarani kama zilivyo tume nyengine za utumishi zinavyopata hii *vote*. Kwa maana hiyo, wakipata *vote* watakuwa na uwezo wa kuweza kufanya mambo vizuri zaidi kuliko yalivyo hivi sasa.

Ukosefu wa magari na vifaa vingine. Serikali ina mikakati mingi tu ya kuweza kuhakikisha hilo. Hata hivyo, hali ilivyokuwepo mwaka jana sivyo ilivyuo mwaka huu hasa kwa upande wa magari na vifaa vingine vyta kutendea kazi katika Idara Maalum za SMZ. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe waendelee vile vile kutusaidia na kushirikiana na sisi ili matatizo haya tuweze kuyatatu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu ya muda, kwa sababu mengine yaliyotolewa ni ushauri kama yale yaliyotolewa na kamati kwa utaratibu wetu tunatakiwa tuje tuyatooe. Na hili suala la kukaa mwaka mzima ni suala la Baraza lenyewe tu, utaratibu wa zamani ilikuwa mwezi kama huu tukipewa maagizo wakati wa bajeti tunakuja kuyatolea ufanuzi. Sasa tukiona kwamba tunachukua muda mrefu katika kuyatolea ufanuzi masuala haya ni jukumu la Baraza kuweza kufanya maamuzi. Kwa hivyo, kama tunahisi mwaka mmoja ni mkubwa twambieni hata wakati wa bajeti tutakuja kutoa ufanuzi juu ya masuala haya isionekane kama ndio utaratibu tulio kubaliana. Utaratibu huu umewekwa na Baraza lako tukufu kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa. Kwa ubunifu Baraza liliamua kuweka utaratibu huo, ukionekana utaratibu huu haufai basi sisi serikali tutasikiliza ushauri ambao tutapewa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya kwisha kusema hayo nataka tena niwashukuru wote waliochangia wizara yangu. Ni imani yangu hawakuchangia kwa namna ya kutaka kuleta mambo mengine ya kukomoana hapana, wamechangia kwa kutukumbusha na kutaka tufanye kazi zaidi kuliko hivi tunavyofanya. Ahsante sana naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kujumuisha yale mambo ambayo yalizingumzwa na Waheshimiwa Wajumbe. Katika michango iliyotolewa Waheshimiwa 12 walizingumzia katika suala langu mimi.

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
3. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
4. Mhe. Subeit Khamis Faki
5. Mhe. Marina Joel Thomas
6. Mhe. Rufai Said Rufai
7. Mhe. Ali Salum Haji
8. Mhe. Mohammed Haji Khalid
9. Mhe. Farida Amour Mohamed
10. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
11. Mhe. Abdalla Juma Abdalla na
12. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa

Katika michango yao yote hiyo kulikuwa na mambo karibu manne au matano ambayo yamefanana. Sasa mimi kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niyazungumze yale mambo ambayo wameyazungumza kwa pamoja kwa hivyo hayo yatajibu Waheshimiwa wote hao.

Kwanza lilikuwa ni suala la mishahara ambapo mishahara hii imegawika sehemu tatu, kuna wafanyakazi, mahakimu wa mwanzo, wafanyakazi wa *DPP* yaani Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na wafanyakazi wa *Law Review Commission*.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba wafanyakazi hasa mahakimu wa mwanzo walikuwa na matatizo kidogo ya mishahara, lakini nashukuru kama nilivyowaahidi wakati wa nyuma kwamba tulizingumza na watu wa utumishi na tukakubaliana na mishahara ya *PCM* sasa imeongezwa, ingawa haitoshi lakini imeongezwa. Zaidi ya hivyo, ni kwamba mbali ya mishahara wanapata *allowance* maalum ili kuongezea yale maslahi yao.

Mhe. Spika, suala hilo pia lipo katika Ofisi ya *DPP*. Ni kweli wafanyakazi wetu wa *DPP* wana hali ngumu sana, mishahara yao ilikuwa ni kidogo na *nature* ya kazi zao zilikuwa ni ngumu wanatishwa au wanatishwa maisha yao. Kwa kweli hili liliwafanya wengi kuvunjika moyo, lakini mimi naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wafanyakazi hao wa *DPP* kwamba ni watu amba wana moyo wa kujenga taifa lao na hii ndio inayotakiwa *patriotism*, uchungu wa nchi. Kwa sababu mishahara katika serikali siku zote inakuwa ni midogo kuliko mashirika ya umma, sasa kama huna ile *patriotism* hasa kwa kweli wengi wanaweza wakakimbia hata katika kazi nyengine za kawaida. Lakini nawashukuru wafanyakazi wetu hawa wa *DPP*.

Kutokana na hayo tumejitahidi kuzungumza na Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma na nina furaha kusema kwamba na wao hawa wameongezewa mshahara wao. Najua na nakubali kwamba hautoshi na ndio binadamu katika mishahara hii haitoshi siku zote, lakini angalau tukianza kidogo kidogo basi hatimaye tunaweza tukafikia pahala pazuri. Lakini nakuhakikisha Mhe. Spika, kwamba wafanyakazi wetu hawa na wao wameongezewa kwa kuheshimu na kwa kusaidia hali zao ngumu walizokwananazo.

Halkadhalika katika wafanyakazi wa *Law Review Commission* nao pia walikuwa katika hali hiyo hiyo na tumezungumza na Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma wamesaidia na wafanyakazi wa *Law Review Commission* hivi sasa pia na wao wameongezewa mshahara. Ninachopenda kusema ni kwamba ingawa mishahara hii imeongezwa, lakini kweli kutokana na hali na kazi zao bado hajjatosheleza sana, naomba sana wafanyakazi hawa watizame hali ya nchi pamoja na hali tuliyonayo. Ninachopenda kuahidi kwamba kila mara tunapopata nafasi basi tutazidi kusaidia ili na wao wawe katika hali nzuri zaidi, lakini mishahara yao sio kama ile ambayo ilikuwa zamani. Zaidi ni kuomba tu kwamba wawe na uchungu wa nchi ili waweze kujenga taifa lao.

Mhe. Spika, suala la pili ambalo lilizungumzwa ni suala la washauri wa Mahakama. Ni kweli tulikuwa tuna deni la karibu shilingi 140 milioni za *assessors* na deni hili kila mara tulikuwa tunalilipa na hivi sasa tumebakia na karibu shilingi 40 milioni arobaini milioni au chini kidogo ya hiyo. Lakini matatizo ya *assessors* ni makubwa, ni makubwa kwa sababu hata kama utalipa leo deni hili Mahakamani *assessors* wanatakiwa kila siku kuna Mahakama kuu kuna Mahakama ya Kadhi kesi nyengine ambazo lazima upate *assessors*, kwa hivyo kila siku si chini ya 12 wanaokwenda Mahakamani.

Kwa hivyo, hili deni kila siku linaongezeka hata ukilipunza lote bado litaendelea kuongezeka. Hivi sasa baada ya kuona matatizo haya tulikaa na maafisa wangu tukatizama njia gani tunaweza kufanya ili kupunguza matatizo haya na bado hatujafikia katika uamuzi lakini tunafikiria kwamba kwa mfano siku moja *assessors* kiasi 12 wanaokuja Mahakama Kuu. Sasa kwa nini wale wote hatuwakati tukawaweka wataatu amba wakisikiliza kesi hii wakitoka hapa wakenda kesi hii. Kwa hivyo, utaona hapo tumepunguza kwa kiwango kikubwa.

Huo ni mfano tu natoa bao hatutafikia maamuzi, lakini tukikubaliana baadae inaweza kabisa ikasaidia matatizo haya ya *assessors*. Lakini kweli ma- *assessors* ni wengi na deni hili litaendelea kuongezeka kutokana na idadi ya kesi sheria inavyotaka kwamba kila wakati tunapaoofanya kesi hizi tuwaite ma- *assessors* kwa hivyo wanaendelea kuongezeka katika hali hiyo.

Mhe. Spika, ninachopenda kusema tu kwamba suala hili tumeliona lakini lile deni la nyuma tumejitahidi kulipunguza ana kama nilivyosema kutoka milioni mia moja na arubaini au chini ya hapo kidogo ambazo tunadaiwa na hizi kila tunapopata pesa tunajaribu kuzizilipa.

Kuhusu kesi za ubakaji, ni kweli kesi hizi zipo nyangi kidogo, matatizo yapo lakini haya matatizo kama nilivyosema mwanzo hayako Mahakamani peke yake wala hayapo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka peke yake wala hayapo Polisi peke yake. Matatizo haya ni yetu sote jamii kama hajatushirikiana jamii kesi hizi zitaendelea kuwepo hasa wazee au jamii uliopo nje ya vyombo. Unapofanya kesi lazima uwe na mashahidi katika kesi hizi ni ndugu yake aliefanya kitendo hicho au mama yake au baba yake au mjomba wake au shangazi yake au jamaa, unawapowaita Mahakamani hawendi wanasema hawataki ama wanasema watadhalilisha zaidi yule mtoto au itakuwa ni aibu.

Sasa unapomwita shahidi halafu haji hiyo kesi Mhe. Spika, itafutwa. Sasa ombi langu siku zote na naendelea kuomba kwamba jamii tusaidieni kwa kukubali kuja kutoa ushahidi. Sasa kama hamkubali kutoa ushahidi Mahakama haina njia isipokuwa kufuta. Lakini pale ambapo tunapata ushahidi tunahakikisha kwamba hivi sasa kesi

za aina hii tunatoa adabu kubwa kama mlivysikia kuanzia miaka 15 na kuendelea 2,027 ili tuhakikishe kwamba matokeo kama haya hayapo tena.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la dhamana na hili alilizungumza Mhe. Makame Mshimba. Dhamana imebadilika kisheria na ni Wajumbe sisi hapa tuliobadilisha sheria ya dhamana. Zamani ilikuwepo sheria iliyokuwa ikitisema kwamba kwa makosa kwa mfano ya mauaji na kwa makosa kama hayo yanayokaribiana na hayo hupati dhamana. Lakini Baraza hili Mhe. Spika, likabadiilisha sheria likasema dhamana apewe mtu yejote ni haki ya mtu yejote, sasa mtu alieua kwa mujibu wa sheria tulioipitisha Hakimu au Jaji anayo haki ya kutoa dhamana kwa kutizama yale mazingira yalivyo. Na hivyo ndivyo ilivyotokea.

Sasa kama hatutaki tena hayo tuje hapa hapa tubadilishe sheria tuseme mtu yejote akiuwa asipewe dhamana, mtu yejote akifanya hivi asipewe dhamana. Lakini tuseme kwamba hii dhamana ni haki ya binaadamu halafu akipewa haki ile tukaanza kupiga makelele, lazima twende na sheria.

Hapa katika utoaji wa dhamana jukumu kubwa analo Hakimu au Jaji la kutizama je, mazingira yale kesi iliyopo tukio lile lilitotokea na jamii tukimyima dhamana huyu au tukimpa dhamana itakuwaje kwa jamii huo ni wajibu wa majaji wetu, pengine jaji anaweza akateleza ni binaadamu. Lakini kama akiteleza haki ya kukata rufaa ipo. Sasa nafikiri tutizameni hii sheria na twendeni kwa mujibu wa utaratibu wa aina hiyo.

Mhe. Spika, kuna suala ambalo lilizungumzwa hasa na Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Mahmoud Muhammed. Suala hili ni suala la migororo ya ardhi ya wakfu. Naomba niseme hivi kwamba hakuna matatizo yoyote baina ya Kiongozi Mkuu na wizara hakuna matatizo. Ni katika utekelezaji wa sheria zetu.

Sheria ya wakfu ya mwaka 2007 namba 2 ya mwaka 2007 inasema Mhe. Spika hasa katika kifungu cha 16 kinasema;

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana itahakikisha kwamba ardhi yote ya wakfu inarejeshwa katika Kamisheni.

Kifungu hicho kiko wazi kifungu cha 16(1,2 na 3) na kifungu cha 16 (3) kinasema;

Kamisheni ya Wakfu itahakikisha au ihakikishe kwamba kama kuna eneo ambalo eneo lile ni la Wakfu na kwamba limechukuliwa au limekaliwa basi Kamisheni ihakikishe kwamba ardhi ile ya wakfu inarejeshwa kwa wakfu.

Sasa tunachofanya sisi wakfu ni kutekeleza sheria hii na tunaitekeleza kwa nia safi. Mimi nafikiri jamii iwashukuru sana Wizara ya Katiba hasa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa sababu sote tunajua hapa Waislam na Wakiristo kwamba ukitumia mali ya wakfu matatizo yake huko akhera huko ni moto. Ukinyanganya mali ya wakfu basi utapata moto ndio tunavyoambwa.

Sasa sisi wakfu tunachofanya ni kuisaidia jamii kwamba tuwakinge na huo moto kwa masuala haya kwa namna gani. Unajua kwamba umechukuwa mali ya wakfu sisi tunachokwambia ardhi hii ni mali ya wakfu lazima itekelezwe kwa mujibu wa utaratibu wa wakfu, pengine mali ya yatima na mambo mengine kama hayo, ikiwa wewe ushajenga pale hata kama umeshajenga, umejenga katika ardhi ya wakfu na kama umejenga katika ardhi ya wakfu ina maana unatumia mali ya watu ya wakfu una matatizo kesho tujaalie ukiafa.

Sasa tunachosema, tunasema tukubaliane angalau tuepukane na matatizo haya tunatoa *token* ya bei ile ya ardhi kiwanja pengine kinauzwa pengine milioni ishirini siku hizi lakini sisi tunakwambia labda toa angalau milioni mbili ili kuhalilisha hichi kiwanja kiwe ni chako mwenyewe usipate hayo matatizo kesho ukifa, ndio tunachosema.

Sasa Mhe. Spika, haya yametokea si kwa shamba tu kama lililozungumzwa tu hapa lakini kuna mashamba kwa mfano Mfenesini kwa Mhe. Ali Abdalla tulikaa nae tukazungumza na utaratibu gani wa kufanya hivyo, kuna shamba Kifoe Wete na kuna shamba la Ndugu N'Kitu la Chake chake, kuna shamba la bibi mmoja nimemsahau jina lake lakini liko Madungu Chake chake yote hayo yana matatizo hayo.

Alichofanya Makamu wa Pili wa Rais kama yeye ni Kiongozi na ni Mkuu wa shughuli za Serikali alikwenda kuwasikiliza wananchi wana matatizo yao hawajui pengine. Sasa Makamu wa Pili alikuwa na haki kwa upande wake kusema zuieni kwanza hiyo ni haki yake, sisi tunafanya huku lakini Makamu wa Pili ana haki ya kusema kwamba zuieni hilo mnalolifanya na yeye ametwita twende tukampe maelezo ilikuwa leo saa 5 tuzungumze nae kwa nini tukafanya hivyo ili na yeye awe katika kuelewa zaidi. Lakini kwa bahati hatukuweza kutoka saa 5 kwa sababu ya shughuli hii.

Kwa hivyo, mimi nasema hakuna matatizo baina ya Makamu wa Pili wa Rais na Wizara ya Katiba ni sawa sawa Makamu wa Pili wa Rais alifanya shughuli zake kama yeye ni Kiongozi wa nchi na Wizara ya Katiba inafanya shughuli zake katika kutekeleza sheria hiyo na Makamu wa Pili wa Rais ni sawa kabisa alivyofanya ili kutaka kujua kuna nini kwa wananchi na huo ndio utaratibu wa utawala.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema ni kwamba matatizo hayo ya wakfu yapo katika mashamba hayo mengi kama nilivyoyataja hayo na wakfu ina wajibu kwa mujibu wa sheria nilivyosema mujibu wa kifungu cha 16 (1). Kwa hivyo, hayo ndiyo yaliyojiri hasa katika hilo shamba ambalo Wajumbe walikuwa wanazungumza hapa na *inshaallah* tutakaa na Makamu wa Pili wa Rais ili tumpe *brief* yote na shughuli zote ambazo zinatekelezwa si kwa hapa tu lakini hata kwa hayo mashamba mengine kwa mfano ya Mfenesini shamba la Ndugu N'Kitu Chake chake na kadhalika.

Mhe. Spika, kuna suala la vizazi na vifo lilizungumzwa hasa katika suala la Magamba. Katika suala la vizazi na vifo kuna mambo mawili *late registration* na kuna *registration* hii ya kawaida. Kama tulivyoahidi kwamba *registration* ya kawaida tumejitahidi na hivi sasa haichukuwi muda ukipata cheti chako kile hasa kwa Mjini Magharibi tumeshaanza ule utafiti wote unaweza ukapata cheti chako wa muda siku mbili, tatu, nne basi.

Kuna matatizo kweli katika mawilaya, kwa sababu katika mawilaya masuala haya ya *registration* hayapo hasa katika wizara yetu kapo katika Mikoa na Wilaya. Sasa mfanyakazi yule yule wa wilaya ambaye tumempa dhamana hiyo ya vyeti anakazi nyengine ya wilaya unaweza ukaenda hayupo, unaweka ukaenda kapewa kazi nyengine hili tumeliona na tunajaribu kulishughulikia, ili mtu ambaye atashughulika na vyeti vya vizazi awe ni mtu *permanent* katika suala lile.

Kweli kulikuwa na matatizo ya magamba ya vyeti na tuliwahi kusema na nikatoa taarifa kwamba matatizo ya magamba yapo kwa sababu *printing press* iliharibika vyeti vikawa havipatikani na baada ya kutengenea vile vyeti ikawa vinaweza kupigwa lakini ile mashine ya kutia namba ikawa haiwezi kutia namba. Kwa hivyo ikawa hatuwezi kutimia vyeti vile kwa sababu havina namba ingeliwu vina matatizo.

Kwa hivyo, kuna kipindi tulichelewa kidogo kiasi miezi sita, saba hivi vyeti vilikuwa havipatikani, lakini hivi sasa vimeshapatikana na tumepeleka katika maeneo, tumepeleka Pemba vyeti kiasi elfu mbili Wete, Chake chake, Mkoani hivyo hivyo tumepeleka, tumepeleka na mwahala mwengine najua hivi vitakuwa havitoshi, lakini ilivyokuwa mashine sasa imeshaanza kutumika kila mara tutafanya hivyo.

Katika tatizo kubwa liliopo ni katika *late registration* ina matatizo kwa sababu kuna vyeti vingi vya bandia inaweza ikawa ni pale pale ofisini, inaweza ikawa ni nje ya ofisi. Kwa hivyo tunapofanya *late registration* tunakuwa makini sana tunataka *information* nyangi mpaka tukizipata tukihakikisha ndio tunaweza tukampa mtu *late registration*.

Mhe. Spika, tatizo jengine ambalo limezungumzwa ni suala la wakfu ambalo kuhusu suala la misikiti na mambo mengine kama hayo. Kwa kweli wakfu na mali ya amana haishughuliki na misikiti isipokuwa pale ambapo tunapata ruzuku, tunaitizama misikiti na misikiti hiyo ile ambayo tunahisi inataku kusaidiwa, lakini si suala letu.

Suala la Mufti pia lilizungumzwa kidogo katika sala za waislamu na wakiristo. Suala hili nalo ni gumu Mhe. Spika, mimi nimeshawahi kuwaita waumini wa kiislam na waumini wa kikiristo mapadri na ma-father na mashekhe waliokuwepo hapa tukazungumza suala. Mimi nafikiri watu wa kulaumiwa na napenda nilisema hapa ni mashekhe na mapadri hawa ndio wanaotaka kutuharibia nchi. Kwa sababu aidha kanisa litakuwepo hapa au msikiti utakuwepo hapa lakini shekhe ataruhusu kwenda kujenga msikiti pale penye kanisa au padri ataruhusu kujenga kanisa pale ulipo msikitiki, sasa kama wewe ni shekhe au padri unahisi kwamba suala hili tukilifanya hivi litaleta mgogoro.

Kwa hivyo, wewe shekhe au padri ndio unaepaswa kulaumiwa na hilo nimewaita na nikawaambia na tukasema sasa tunachochukuwa na nilichoamua ikiwa kuna msikiti mwanzo akenda padri akaruhusu kwenda kujenga kanisa pale

kanisa lile tutalivunja na ikiwa kuna kanisa shekhe akenda kujenga msikiti pale pale msikiti ule tutauvunja kwa sababu hawa ndio wanaotafuta matatizo.

Kwa hivyo, katika hili suala la *interface* tukaeni pamoja tuyatatue matatizo hayo sio kwamba hapa upo msikiti hapa tunajenga kanisa au hapa lipo kanisa hapa unajenga msikiti hatutofahamiana hivyo, kwa sababu kanisa kuna shughuli zake na msikiti una shughuli zake. Kwa hivyo, hebu katika hili suala la *interface* tukae pamoja tutizameni utulivu wa kisiasa katika suala la dini. Hayo Mhe. Spika, ndio mambo ambayo yanajitokeza katika matatizo haya ya misingi ya dini.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba tumeyachukuwa maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria, tunawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na tutayachukuwa naoni yao na tutazingatia ili tuweze kutekeleza vyema shuguli zetu za wizara. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri kuna dakika tano na Mwenyekiti amenambia kwamba atahitaji muda zaidi kidogo ya huo pengine dakika 10 zaidi. Sasa kama tunawafiki basi hebu au jioni. Mhe. Mwenyekiti tutakwita jioni muda uliobaki dakika tano Waheshimiwa wanataka wapumzike ili jioni waje saa 11:00 barabara wawepo hapa. (*Makofî*)

(Saa 6: 55 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(*Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia*)

**Mhe. Spika:** Naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny: Mwenyekiti wa Katiba, Sheria na Utawala):** Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana tena jioni hii ili kumalizia michango yetu ya ripoti ya Katiba, Sheria na Utawala sambamba na kuchangia ripoti za utekelezaji wa maagizo na ushauri uliotolewa na kamati kwa Serikali.

Mhe. Spika, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nimalizie ku-*wind up* ripoti ambayo niliisoma jana na Wajumbe wamechangia ripoti hiyo. Mhe. Spika, shukurani za pekee ziende kwa Waheshimiwa Wajumbe kwa kuchangia ripoti yetu ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala sambamba na kuchangia ripoti za utekelezaji wa maagizo na ushauri uliotolewa na kamati kwa Serikali.

Vile vile Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala naomba nipokee pongezi ambazo Waheshimiwa Wajumbe wamezitoa kwa kamati kwa kazi nzuri ambayo kamati imekuwa ikifanya katika kipindi chote cha mwaka.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kuwatambua Wajumbe ambao waliochangia:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
3. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
4. Mhe. Subeit Khamis Faki
5. Mhe. Marina Joel Thomas
6. Mhe. Rufai Said Rufai
7. Mhe. Ali Salim Haji
8. Mhe. Mohamed Haji Khalid
9. Mhe. Farida Amour Mohammed
10. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
11. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
12. Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa

Mhe. Spika, kwa ufupi ripoti yetu imechangiwa na Wajumbe 12.

Kwa kuanzia Mhe. Spika, naomba nianze na masikitiko ambayo yamejitokeza mionganoni mwa Wajumbe juu ya Serikali kutotekeleza maagizo ama kutokuyafanya kazi ushauri ambao kamati hutoa kwa Wizara husika. Hili siyo kwa kamati hii tu Mhe. Spika, ninaamini na ripoti nyengine ambazo zitakazokuja malalamiko haya bado yatajitokeza.

Mhe. Spika, imekuwa ni *trend* sasa, yaani imekuwa ni jambo la kawaida kamati zinapoagiza maagizo hayafanyiwi kazi ipasavyo na mara nyengine kutokufanyiwa kazi kabisa, kiasi ya kwamba Baraza lako Tukufu kupitia Kamati za Baraza linaonekana halifanyi kazi ipasavyo kutokana na kutokuonekana kwa matokeo chanya (*positive result*) za kazi za kamati zinazofanya.

Mhe. Spika, masuala mengine mbali mbali yamejitokeza mionganoni mwa Wajumbe waliochangia, masuala ambayo ni yale yale ya kawaida ambayo kamati imekuwa ikipigia kelele kipindi chote, takriban kwa Wizara zote zinazosimamiwa na kamati. Mhe. Spika, na hili limeelezwa vizuri wakati Mhe. Ismail Jussa Ladhu alipokuwa akichangia ripoti.

Vile vile Mhe. Spika, masuala mbali mbali mengine ambayo yamejitokeza yakiwemo maslahi ya wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ na Mhe. Waziri amejitahidi kuyatolea maelezo. Bajati ndogo zinazopatiwa vikosi, suala la Serikali za Mitaa hasa kwa upande wa Baraza la Manispaa na Halmashauri za Miji juu ya suala zima la usafi wa miji yetu.

Mhe. Subeit Khamis Faki naye alizungumzia hili kwa uchungu sana pamoja na Mhe. Rufai Said Rufai na Mhe. Ali Salim Haji.

Vile vile suala jengine limejitokeza ni rushwa katika Mahakama zetu. Pia Wajumbe walizungumzia Ofisi za Vizazi na Vifo juu ya upatikanaji wa vyeti, suala zima la maslahi ya wafanyakazi ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, masuala ya Wakfu na Amali ya Amana pia yamegusiwa. Lakini pia kulijitokeza suala zima la mradi wa *e-government* ambao kwa muda mrefu sana Wajumbe pamoja na kamati yenye ilikuwa ikilipigia kelele sana suala hili.

Mhe. Spika, pia kuna mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyagusia kwa namna moja au nyengine na kwa mantiki hiyo naomba Serikali iyape uzito masuala yale ambayo Wajumbe wamechangia. Na wakati Mawaziri wana-*wind up* hapa Mhe. Spika, walijitahidi sana kutoa ufafanuzi lakini pia kuahidi kuyafanya kazi yale ambayo bado hayapatua utatuza.

Mhe. Spika, bado tuna imani na Serikali hii na tunaamini bado ipo haja ya kuipa nafasi tena Serikali hii ili ikamilishe yale ambayo kwa namna moja au nyengine bado Serikali ipo katika juhudhi za kuzitafutia utatuza changamoto hizo. (*Makofî*)

Mhe. Spika, tunaamini Serikali imesikia vilio hivi na malalamiko haya ya Waheshimiwa Wajumbe na sasa itachukua juhudhi za makusudi katika kuyafanya kazi kwa pamoja, kwa sababu tunaamini kuwa Serikali inafanya kazi kwa pamoja. Kwa maana ya kwamba *collective responsibility* lakini pia kushindwa kufanya kazi kwa Serikali hii haina maana kuwa kushindwa kwa Dkt. Ali Mohamed Shein, bali ni kushindwa kwa Serikali yote kwa pamoja kuanzia uongozi wa juu, wakianzia washauri wakuu mpaka *line* yote hii ya mbele Mhe. Spika. (*Makofî*)

Baada ya hayo Mhe. Spika, ninawashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe kwa michangio yao na naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe majumuisho ya Mwenyekiti ndiyo hayo, hatua iliyobaki ni kupokea ripoti ya utekelezaji wa Serikali pamoja na ripoti hii ya Kamati, Sheria na Utawala.

Idadi ya Wajumbe waliomo ndani haituwezeshi hivi sasa kuipokea hiyo. Kwa maana hiyo ili twende vizuri na tusichukue muda mkubwa naomba twende kwenye hatua ya kwanza na *quorum* ikitimia hii tutaipokea rasmi.

Kwa sasa idadi ya Wajumbe waliopo haituwezeshi pamoja na kuhimiza kwamba tungefika mapema. Kwa sababu hivi ni vitu muhimu vionekane vimekwenda kwa mujibu wa taratibu ya Kanuni zetu, ingawa hivi sasa Wajumbe wanaingia wengi. (*Makofî*)

Katibu hebu nihesabie Wajumbe waliopo.

Ninaambiwa Waheshimiwa Wajumbe waliopo ni 31.

*(Hapa Wajumbe walikuwa wakiingia kwa haraka)*

Bado kidogo hatuwezi tukamaliza kazi hii Wajumbe hawajatosheleza bado, ingawa ninawaona wengine wanakuja kwa haraka ili kukamilisha *quorum* iliopo tuweze.

Tunawaomba Wajumbe waliopo nje waingie kwa haraka ili tumalizie kazi hii twende kwenye hatua ya kwanza ya Kamati ya Wanawake na Ustwi wa Jamii.

*(Hapa makofi yalipigwa kuashiria Wajumbe wakiingia kwa haraka)*

Hayo makofi ni kwa sababu ya wale wanaochelewa. (*Makofi*)

Ninafikiri ili tusikae bure twende hatua ya kwanza na *quorum* ikifika nitaomba Waheshimiwa Wajumbe mumepokea ripoti ya utekelezaji pamoja na ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Kwa sasa naona bado hawajatimia. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe kwa muelekeo huo naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

**Mhe. Mohamed Mbwana Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Kamati wa Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):** Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa....

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa nimejisahau kidogo. Kumbe kwanza tunadai ripoti ya utekelezaji ya shughuli za kamati hizi zilizopita. Na kwa mtiririko wa hapa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

**Mhe. Waziri wa Afya (Kny: Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto):** Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, ninapenda kuwasilisha utekelezaji wa maoni ya maagizo ya kamati yaliyotolewa katika ripoti ya mwaka 2013/2014 kwa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, utekelezaji wa maagizo yaliyopendekezwa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Uwezeshaji wa Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto katika ripoti ya 2014.

Tunaanza na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti:

### **Agizo**

Kamati inaitaka Wizara kushajihisha jamii kushiriki kikamilifu katika kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji ili zipate ufumbuzi.

### **Utekelezaji Wake**

Wizara inaendelea na kazi zake za kuihamasisha jamii katika suala zima la kushiriki kikamilifu katika shughuli za kupambana na udhalilishaji wa jinsia. Hii ikiwa ni pamoja na kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji ili zipate ufumbuzi. Katika utekelezaji huo Wizara imezindua rasmi kampeni ya kupinga vitendo vya udhalilishaji wanawake na watoto.

Kampeni ilizinduliwa rasmi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein. Katika uzinduzi huo maonesho ya watoa huduma pamoja na machapisho mbali mbali yalitolewa, pia vipindi mbali mbali vimetayarishwa na kurushwa hewani kupitia redio na televisheni ya umma pamoja na redio jamii.

Shughuli zote hizi zililenga kuihamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ikiwemo kutoa ushahidi.

Aidha, wizara ilitayarisha na kuchapisha vipeperushi vilivyosambazwa katika sherehe ya mapinduzi ya 2015. Vipeperushi hivyo vilionesho hali halisi, hatua zilizochukuliwa, changamoto pamoja na hatua za kuchukua ikiwa ni pamoja kukubali kutoa ushahidi wakati wa kesi za udhalilishaji wa jinsia zikiendelea.

Mikutano ya Wakuu wa Wilaya kwa Unguja na Pemba, mikutano ya wadau wanaoshughulikia masuala ya udhalilishaji wanawake na watoto, pamoja na mikutano ya washirika wa maendeleo iliitishwa kujadili namna ya utekelezaji wa kampeni ya kupinga vitendo vya udhalilishaji wanawake na watoto. Katika jitihada hizo imeonekana kuwa tayari idadi ya kesi zilizopata hukumu inaongezeka.

Kamati inataka Wizara kuendelea kuzisimamia Kamati za Shehia zinazoshughulikia masuala ya kuzuwa na kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, kuvishajihisha kupata maeneo yao rasmi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zao na kuziwezesha kifedha pindi panapotoka mahitaji ya msingi.

### **Utekelezaji**

Katika utekelezaji wake wa kila siku Wizara pamoja na mambo mengine inaendelea kuvishughulikia Kamati za Shehia za kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ili viweze kumudu vyema kazi zao. Wizara imefanya tathmini ya Kamati 59 ya kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanawake na watoto.

Kati ya hizo Kamati 24 za Unguja na Kamati 36 za Pemba. Lengo la tathmini hiyo ni kujua uwezo na mahitaji ya kamati hizo kiutendaji ili kuweza kupanga mikakati madhubuti na kuiwezesha na kufikia lengo lilokusudiwa.

Suala la maeneo ya kufanya kazi kwa kamati hizo bado ni changamoto. Kamati nyingi hufanya kazi zake Ofisi za Sheha au nyumbani kwa Wajumbe wa Kamati.

### **Idara ya Mikopo**

Kamati inaitaka Wizara kuwapatia Idara ya Mikopo wafanyakazi wa kutosha na wenye sifa ili kufanikisha kazi zao kwa ufanisi.

### **Utekelezaji**

Wizara katika bajeti yake ya fedha ya 2014/2015 imezingatia tatizo hilo kwa kuziomba nafasi tupu katika *nominal roll* na kwa kuzingatia sifa zinazohitajika. Nafasi hizo tatu tayari zimeshajazwa.

Kamati inashauri Wizara kuipatia Wizara kuipatia Idara mikopo itakayokidhi mahitaji hayo, kwani ofisi iliyopo hivi sasa hairidhishi.

### **Utekelezaji**

Kimsingi Idara ya Mikopo imepangiwa kuingizwa katika jengo la Wizara ilipo Mwanakwerekwe baada ya kumalizika ujenzi wa jengo lake ilipo Mwanakwerekwe. Hivi sasa Wizara inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha kupata fedha za ukamilishaji wa jengo hilo.

### **Agizo**

Kamati inashauri kupatiwa mafunzo kwa wafanyakazi wa Idara ya Mikopo ili wafanye kazi zao kwa utaalamu zaidi.

### **Utekelezaji**

Suala la kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Idara ya Mikopo limepewa uzito unaostahiki. Idara imewapatia mafunzo ya ndani (*In house training*) watendaji wake wote juu ya uendeshaji wa shughuli za mikopo.

Aidha, mtendaji mwengine alikwenda nchini India kwa mafunzo mafupi ya uendeshaji na uwekezaji na fedha za mikopo. Watendaji wengine wanen Unguja na watatu Pemba wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika fani za uchumi, mikopo midogo midogo, usimmizi wa fedha na biashara. (*Makofi*)

### **Agizo la Kamati**

Kamati inaitaka Idara kuchukua juhudzi za makusudi kuhakikisha kwamba inatoa elimu kwa wananchi juu ya masuala ya mikopo.

### **Utekelezaji**

Idara imekuwa ikiwatumiwa Masheha na Wakuu wa Wilaya katika kusambaza taarifa za kuwepo kwa mfuko huu na hususan taratibu za kuweza kupata mikopo katika mifuko.

Njia nyengine zinazotumika ni kuandaa vipindi maalum vinavyohusu masuala ya mikopo na taratibu zake. Aidha, wizara imekuwa ikitangaza shughuli za mfuko kila wanapopata fursa ya kukutana na wanachi kupitia shughuli zake mbali mbali.

### **Idara ya Ustawi wa Jamii**

Kamati inaitaka wizara kuwapa ushirikiano wa karibu Wizara ya Fedha ambao waliahidi kulipa deni lote la fidia kwa wafanyakazi walioumia kazini, kabla ya kufika mwezi Machi, 2014. Baada ya kukamilisha baadhi ya taratibu ikiwemo uhakiki wa madeni wanaodai fidia. Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, deni lililokuwepo la fidia la karibu shilingi milioni 100 kwa ajili ya wafanyakazi walioumia kazini, lililipwa kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2013/2014 kama kamati ilivyohadiwa.

Kamati inaitaka wizara kuvipatia vituo vya mkono kwa mkono usafiri wa uhakika, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kutembelea Shehia mbali mbali kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii.

### **Utekelezaji**

Vituo vya mkono kwa mkono viko chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya, na ndio yenye dhamana ya kuvipatia huduma ya uendeshaji ikiwemo usafiri. Hata hivyo, kupitia wizara hii Shirika la *Save the Children* wamesaidia kununua vyombo vya moto kwa ajili ya watendaji wa vituo vitano vya mkono kwa mkono, ikiwemo Mnazi Mmoja, Makunduchi, Kivunge, Chake Chake na Wete ili kuharakisha utendaji wao.

### **Agizo la Kamati**

Kamati inashauri wizara kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kamati ya Shehia, kuwashudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, ili wanajamii waweze kushajihika katika kuchangia kamati hizo.

### **Utekelezaji**

Wizara inaendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia mashirikiano na kamati za Shehia za kudumu, watoto wanaoishi katika mazingira magumu, na zaidi katika kuwashajihisha wanajamii kuzichangia kamati hizo, ili zitowe huduma na kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi.

### **Agizo la 11**

Kamati inaitaka wizara kuwapa mafunzo wafanyakazi wanaolea watoto wenye mahitaji maalum, ili waweze kulea watoto wa aina tofauti.

### **Utekelezaji**

Wizara imeanza kulifanyia kazi agizo hili kwa kuanza kutoa mafunzo ya siku tatu, kuhusu matunzo ya hifadhi ya mtoto katika mazingira tofauti kwa wakuu wa vituo vya kulelea watoto.

## **Agizo la 12**

Kamati inaitaka wizara kuajiri wafanyakazi wa kada za chini kwa ajili ya nyumba ya kulelea watoto Mazizini, kwani msafishaji aliopo hivi sasa ni mmoja tu.

### **Utekelezaji**

Tayari hatua imechukuliwa jumla wafanyakazi watatu wa kada ya ulinzi wa nyumba ya watoto mmoja, muhudumu mmoja na mlezi mmoja wameajiriwa.

## **Agizo la 13**

Kamati inaitaka wizara kulitutia ufumbuzi suala la usafiri, kwa ajili ya nyumba ya wazee Sebleni, ili waweze kurahisisha mahitaji ya wazee waliopo.

### **Utekelezaji**

Wizara inaendelea kulifanyia kazi suala hili kadiri hali ya fedha itakaporuhusu.

## **Agizo la 14**

Kamati imeridhishwa sana na juhudhi ya wizara ya kuyafanyia matengenezo nyumba ya wazee Sebleni. Hivyo, inaitaka wizara kuzipatia nyumba hizo wahudumu wa kutosha ili nyumba hizo ziweze kutunzwa kama inavyohitajika.

### **Utekelezaji**

Wizara imepokea agizo hili na inaendelea kulifanyia kazi.

## **Idara ya Ushirika**

Maagizo ya kamati

Kamati imeitaka wizara kuipatia Idara ya Ushirika fedha kwa ajili ya kulifanyia matengenezo jengo lao kongwe waliopatiwa, ili waweze kuhamia na kufanyia kazi zao kwa ufanisi.

### **Utekelezaji**

Wizara imepatiwa jengo katika eneo la Migombani na kazi ya kulifanyia ukarabati jengo hilo imeanza.

## **Agizo la Kamati**

Kamati inashauri Idara ya Ushirika kupatiwa usafiri wa uhakika, ili waweze kutekeleza majukumu yao ya msingi ya kufuatilia vyama vya ushirika.

### **Utekelezaji**

Wizara imetekeliza agizo hilo kwa ufanisi, ambapo imeweza kushirikiana na program ya miundombinu ya masoko, uingizaji wa thamani na mazao ya huduma za fedha vijijini na imefanikiwa kutenga fungu kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usafiri, vikiwemo gari mbili na vipando vespa na pikipiki.

Hivi sasa taratibu za ununuzi kwa njia ya zabuni zinaendelea kwa mujibu wa sheria ya manunuzi inavyoolekeza.

## **Agizo la Kamati**

Kamati inaitaka wizara kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Idara ya Ushirika, ili wawe na taaluma juu ya masuala wanayofanya kazi. Mafunzo yajumuishwe mafunzo ya muda mfupi na mafunzo ya muda mrefu.

### **Utekelezaji**

Wizara imewapatia fursa ya mafunzo wafanyakazi 10, Unguja wafanyakazi wanane na Pemba wafanyakazi wawili. Wafanyakazi hao wanaendelea na mafunzo kwenye fani mbali mbali ikiwemo utunzaji wa kumbukumbu, masjala, takwimu, utawala wa nguvu kazi, human resource management, sheria, ujasiriamali na fani ya maendeleo ya jamii.

Pia, kwa kupitia programu ya huduma za fedha vijijini, wafanyakazi 25 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kwenye fani ya uongozi wa uendeshaji wa *SACCOS*. Mafunzo hayo yameendeshwa na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

Aidha, wizara imeandaa mafunzo mengine kama hayo kwenye fani ya ukaguzi wa hesabu ya vyama vyaya ushirika. Mafunzo hayo yataendeshwa na Shirika la Ukaguzi wa Vyaka vyaya Ushirika Tanzania Bara. Maandalizi yanaendelea na mafunzo yameanza katika mwezi wa Februari, 2015.

Hatua hizi zitasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa elimu na usalama kwa watendaji wa kukuza ufanisi katika idara hii.

Idara ya Uratibu wa Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

### **Agizo la Kamati**

Kutoa elimu kwa jamii juu ya dhana ya uwezeshaji kupitia vyombo vyaya habari, ili jamii ipate kufahamu na kuweza kujishughulisha katika kazi mbali mbali zitakazo wakwamua kiuchumi.

### **Utekelezaji**

Elimu juu ya dhana ya uwezeshaji imekuwa ikitolewa kupitia vyombo vyaya habari na kupitia programu ya mafunzo kwa wajasiriamali.

Agizo la pili ni kuandaa mikakati mbali mbali ya kuwapatia mahitaji wajasiriamali na masoko ya uhakika, ili fedha zinazotumiwa na serikali katika kuwawezesha wananchi zitumike ipasavyo.

### **Utekelezaji**

Hili limetekelezwa kwa vitendo na linaendelea kufanyiwa kazi, kwani wizara kwa kupitia Idara ya Uratibu, tayari imefungua kituo cha kulelea wajasiriamali ambacho kitaweza kutoa huduma zote na kutatua changamoto zinazowakabili. Idara imeweza kupeleka wajasiriamali 38 kushiriki maonesho ya kimataifa nchini Kigali Rwanda, ili kuweza kutangaza biashara zao na kuweza kutanua fursa ya masoko.

Mhe. Spika, baada ya hayo napenda kuwasilisha. (*Makofî*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Naomba sasa baada ya kumshukuru Kaimu Waziri wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, nimkaribishe sasa Mhe. Waziri wa Afya.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Allah kwa kutupa uhai na uzima, naomba kwa ruhusa yako kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, Utekelezaji na majibu ya baadhi ya hoja zilizotolewa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Afya, katika ripoti ya mwaka 2013/2014.

Mwanzo ilikuwa ni kitengo cha maradhi yasiyoambukiza. Maoni na maagizo ya kamati.

Kwanza, kamati inaitaka wizara kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya, ili waweze kugundua na kutibu magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa mujibu wa miongozo mbali mbali ya afya. Pia inaishauri wizara kuendelea

kutoa elimu kwa jamii kwa kutumia njia tofauti zitakazoweza kufikisha ujumbe kwa ufanisi juu ya njia za kujikinga na magonjwa hayo.

Pili, aidha kamati inaitaka serikali kuisaidia wizara katika kuhakikisha kwamba huduma za magonjwa yasiyoyakuambukiza zinaimarika katika ngazi zote.

### **Majibu**

Katika kuhakikisha wafanyakazi wanatoa huduma katika vituo mbali mbali nya afya, wanajengewa uwezo wa kugundua na kutibu magonjwa yasiyoambukiza. Wizara ya Afya kupitia kitengo chake cha maradhi yasiyoambukiza yaani NCD, *Non Communicable Diseases*, imeandaa muongozo maalum unaoitwa kwa jina la lugha nyengine *NCD treatment guideline*, yaani matibabu ya maradhi yasiyoambukiza, muongozo wa maradhi yasiyoambukiza, kwa ajili ya kuwawezesha wafanyakazi hao kufanyakazi zao kwa ufanisi zaidi.

Aidha, baada ya kukamilika kwa muongozo huo kitengo cha NCD kimefundisha jumla ya wafanyakazi 192, kutoka vituo nya afya daraja la kwanza, hadi hospitali ya rufaa pamoja na kuwapatia elimu wasimamizi 10 wa timu za afya za wilaya, yaani *district medical Officers DMOs* kwa ufupisho Unguja na Pemba.

Kwa upande wa kuelimisha jamii kitengo cha maradhi yasiyoambukiza kimetumia njia mbali mbali za kutoa elimu kwa jamii kuhusu maradhi yasiyoambukiza. Kitengo kimefanikiwa kupita katika wilaya zote kumi za Unguja na Pemba na kufanya mikutano ya uhamasishaji na timu za wakuu wa wilaya, Masheha pamoja na Madiwani. Lengo la mikutano hii ilikuwa ni kuwahamasisha viongozi hao ili na wao kwa nafasi zao waweze kufikisha elimu hiyo kwenye jamii zao husika. Baada ya mikutano hii kitengo kiliweza kupata mialiko hususan Shehia kadhaa kwa ajili ya kufikisha elimu hiyo.

Sambamba na mikutano hiyo, kitengo pia kiliwapatia semina waandishi wa habari wapatao 40 wa Unguja na Pemba, kutoka vyombo tofauti nya habari na makala mbali mbali zilichapishwa katika magazeti, ma-blog na pia taarifa hizo kurushwa katika redio na televisheni.

Aidha, kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji Zanzibar ZBC, filamu ilioandalika na kitengo cha NCD iliweza kuoneshwa katika Shehia zipatazo 20, zilizomo katika baadhi ya wilaya za Unguja. Pia CD hizo ziligaiwa kwa Masheha na Madiwani wote walioshiriki katika mikutano ya uhamasishaji kwa Unguja na Pemba.

La pili, ilikuwa huduma za maradhi yasiyo ya kuambukiza kwa sasa zinatolewa hadi kwenye vituo nya afya daraja la pili. Kufanya kwa mafunzo kwa watoa huduma kumefanya idadi ya vituo vinavyotoa huduma za kugundua na kutibu magonjwa yasiyoambukizwa, kuongezeka kutoka vituo vitatu hadi kufikia vituo 26 kwa Unguja na kwa upande wa Pemba huduma hizo zimeongezeka kutoka vituo vinne hadi vituo 18.

### **Kitengo cha Kupambana na Maradhi Yasiyopewa Kipaumbele**

#### **Maoni na Maagizo ya Kamati**

Kamati inaitaka wizara kuizungushia uzio Ofisi ya Kitengo cha Magonja yasiyopewa kipaumbele iliopo Mianzini, ili kudhibiti wizi wa rasilimali za ofisi na pia kamati inaitaka wizara kuchukua jitihada za kuelimisha jamii umuhimu wa kutumia dawa za kichocho ambazo gharama yake ni kubwa, lakini jamii imekosa mwamko wa kuzitumia dawa hizo.

### **Majibu**

Ni kweli dawa za kichocho zinaghari mu fedha nyingi na wizara kupitia kitengo cha maradhi yasiyopewa kipaumbele, kwa kushirikiana na wadau wa Shirika la Afya la Dunia WHO, dawa hizo zinapatikana. Moja kati ya mikakati ya kutokomeza kichocho hapa nchini, ni kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo nya habari nya kitaifa na nya kibiashara pamoja na mashulenii.

Pia kitengo kinaendelea kujenga mafulio katika Shehia 45 za Unguja na Pemba zenye maambukizo makubwa ya maradhi ya kichocho. Pia walimu wa skuli wamepatiwa mafunzo, ili waweze kutoa elimu kwa wanafunzi dhidi ya

maradhi ya kichocho. Kwa upande wa suala zima la kumeza dawa za kichocho, minyoo na matende, elimu imetolewa ili kutokomeza kabisa maradhi haya fakili hapa nchini kwetu.

Kuhusu suala la kuzungusha uzio, wizara bado haijaweza kulitekeleza agizo hili kutokana na uhaba wa fedha.

### **Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi**

Kamati inaitaka wizara kuipatia usafiri wa uhakika Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi, ili kuweza kutekeleza shughuli zake mbali mbali, zikiwemo za ukaguzi wa schemu za kazi, kufanya uchunguzi wa afya za wafanyakazi na kutoa elimu ya afya katika taasisi tofauti, zikiwemo za serikali na za binafsi.

### **Majibu**

Hadi sasa Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi bado hakijaweza kupatiwa usafiri kwa ajili ya shughuli zake za ukaguzi, hii ni kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, pale panapohitajika usafiri kwa kazi za uchunguzi, wizara hukipatia kitengo hicho usafiri ili kuendeleza shughuli zake za kila siku, usafiri huo huazimwa kutoka katika vitengo vingine.

### **Kitengo cha Lishe**

#### **Maoni na Maagizo ya Kamati**

Kamati inaitaka wizara kuhakikisha kuwa kitengo kinapatiwa fedha za kutosha, ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwani kutegemea wafadhili pekee kunadhorotesha utekelezaji wa majukumu ya kitengo. Kamati inaagiza wizara kuvisimamia vituo vya afya kwa kuhakikisha kuwa takwimu za watoto waliochini ya umri wa miaka mitano vinavyohusiana na utapiamlo mkali vinawekwa vizuri, ili utekelezaji wa matibabu ya utapiamlo mkali uwe wa ufanisi na pia kuishajihisha jamii kuwapeleka watoto katika vituo vya afya kwa ajili ya kupata matibabu mapema pindi watakopogundua kusumbuliwa na maradhi mbali mbali ikiwemo utapiamlo.

Pia kamati inaitaka wizara kuhakikisha kuwa wanawaajiri wafanyakazi wenye fani ya lishe katika wilaya zilizo na upungufu, ili hatimaye waweze kuhudumia wilaya ipasavyo.

### **Majibu**

Wizara inaendelea kukipatia fedha kitengo hicho pale hali ya fedha inaporuhusu, kwa vile bado wafadhili wanaendelea kutufadhili huduma za lishe, hivyo wizara huangalia maeneo mengine ambayo hayana ufadhili kwa sasa.

Suala la kuboresha takwimu za lishe zinazohusiana na utapiamlo mkali, wizara imepanga kufanya mkutano shirikishi kwa ajili ya kuimarisha takwimu hizo, na ambapo kitengo cha lishe kimepanga kubadilisha uzoefu na kitengo cha chanjo *ETI*, ili kuona mbinu wanazotumia kwa ajili ya kuimarisha uwekaji wa taarifa hizo.

Wizara inalishughulikia suala la kuwaajiri wafanyakazi wa fani ya lishe katika ngazi ya wilaya, kwa sasa fani hii imekuwa na upungufu katika soko la ajira. Hata hivyo, mfanyakazi mmoja aliyesomea fani ya lishe, amerudi masomoni na Shahada ya Uzamili, ingawa mfanyakazi huyo amepangiwa kazi katika kitengo cha lishe makao makuu ya wizara kutokana na uhaba kwenye kitengo.

### **Kitengo cha Huduma za Matibabu ya Macho**

#### **Maoni na Maagizo ya Kamati**

Kamati inaitaka wizara kuipatia jengo la kutosha hospitali ya magonjwa ya macho, ili iweze kutoa huduma za matibabu ya macho kwa ufanisi na kuweza kuhifadhi vyema vifaa vya hospitali. Kamati pia inaitaka wizara kupitia bajeti yake, wakipangie kitengo cha macho mgao wa fedha za bajeti, ili waondokane na utegemezi wa wafadhili moja kwa moja na pia kulitafutia ufumbuzi suala la usafiri na dereva katika hospitali ya macho.

## **Majibu**

Wizara imo katika taratibu za kutayarisha nyaraka kwa ajili ya ujenzi wa jengo la macho kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja. Michoro tayari imeshatayarishwa kwa ajili ya kuwasilisha kwenye bodi ya zabuni kwa hatua zaidi. Pia wizara imepokea ushauri wa kamati na inaaahidi kuufanya kazi katika mwaka ujao wa fedha wa kitengo hicho, kuhusu suala la usafiri wa kitengo hicho na dereva, tayari imeshapatiwa ufumbuzi. (*Makofsi*)

**Mhe. Spika:** Haya, tumsikilize Mhe. Waziri, baada ya pongozi kwa wale waliochelewa watatu, walioingia sasa hivi.

## **Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja**

### **Maoni na Maagizo ya Kamati**

Kamati imebaini kuwa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinahitaji kufanyiwa ufumbuzi wa haraka. Hivyo, kamati inaitaka wizara kuunda idara maalum itakayoshughulikia afya ya akili na tiba ya madawa ya kulevyia. Kufanya hivyo kutapelekea kuimarika kwa tiba ya akili na tiba ya madawa ya kulevyia na kuondoa usumbufu ulioko sasa.

Kamati pia inaitaka wizara kufanya ununuzi wa tanuri la kuchomea taka za hospitali, na ununuzi wa sehemu iliyobaki ya *DNA machine*, ununuzi wa kifaa cha kugundulia damu za watoto ambaeo wamezaliwa na mama walioambukizwa *VVU* na kufanya tathmini ya vifaa vilivyokosekana katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, ili hatimaye wizara iweze kuweka vipaumbele vya kununua vifaa vilivyokosekana na kuondosha kasoro zinazojitokeza.

Kamati inaitaka wizara kukiboresha kitengo cha takwimu cha Hospitali ya Mnazi Mmoja, pamoja na kuwafanya utaratibu wa kupata eneo jengine ambalo watalitumia katika kutunza kumbukumbu za wagonjwa vizuri, kwani eneo liliopo sasa limekuwa finyu na mafaili ya wagonjwa yameshindwa kupangwa katika utaratibu mzuri.

Kamati inaitaka wizara kuifanyia matengenezo Hospitali ya Mwembeladu, katika sehemu ya huduma ya walioambukizwa virusi vya ukimwi, kwani kamati ilibaini kuwa walioambukizwa virusi vya ukimwi hupata huduma katika eneo wazi, hali inayoleta usumbufu. Kamati pia imeitaka wizara kuipatia Hospitali ya Mwembeladu madaktari ili waweze kusaidia katika huduma zinazotolewa, na pia kuifanyia matengenezo vifaa vya hospitali ili iweze kutumika kwa ufanisi.

Kamati inaitaka wizara kuwapatia walinzi Hospitali ya Mwembeladu, kutokana na kuwa wafanyakazi wengi walipo ni wanawake, na wamekuwa hawana usalama wa kutosha. Kamati inaitaka wizara kuiwekea Hospitali ya Mwembeladu gari maalum la kubeba takataka za hospitali ili kuondokana na tatizo la kurundikana kwa taka na harufu mbaya katika eneo hilo.

## **Majibu na Utekelezaji**

Kwanza Wizara kwa sasa haina nia ya kuifanya hospitali ya wagonjwa wa akili kuwa ni idara inayojitegemea, kinachoendelea kwa sasa ni Wizara kuifanyia kazi waraka wa kuifanya hospitali ya Mnazi Mmoja iwe ni taasisi inayojitegemea kama ilivyoainishwa kwenye sera ya afya ya mwaka 2011. Ni matarajio yetu mchakato huu utaisaidia hospitali ya wagonjwa wa akili ya Kidongo Chekundu kuwa katika hali nzuri ambayo hospitali hiyo ipo chini ya idara ya Mnazi Mmoja. Wizara tayari imeshanunua matanuri mawili ya kuchomea taka hatarishi hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo inafanyakazi vizuri.

Jengine kitengo cha takwimu cha hospitali ya Mnazi Mmoja kimekuwa kikikabiliwa na uhaba wa nafasi ya kuwekea kumbukumbu za wagonjwa kwa muda mrefu, hii inatokana na kukosekana kwa nafasi katika hospitali inayosababishwa na utanuzi unaofanywa na majengo ndani ya hospitali ili kuongeza baadhi ya huduma zake. Hii ilipelekea eneo hilo la kuwekea kumbu kumbu za wagonjwa kutumika kujengea chumba cha mtambo wa AC, jitihada mbali mbali zimekuwa zikichukuliwa ili kujaribu kulitattua suala hili. Kati ya jitihada hizo ni kuangalia namna ya kubadilisha mfumo wa kumbu kumbu ulivyo sasa na utaratibu mzima tayari unaandalila ili kuelekea katika taratibu za kielektroniki kwa kumbu kumbu.

Huduma za walioambukizwa VVU kwa upande wa Hospitali ya Mwembeladu zinatolewa katika sehemu ya nyuma ya hospitali hiyo, wagonjwa wanaohudumiwa hapo sio wote waliopata maambukizi ya VVU bali wapo wale waliopata maradhi mengine yanayosababisha ya kujamiana, lengo la Wizara hii ni kusambaza huduma hizi hadi kwenye vituo vya afya kwani kuzitoa kiuficho sana huduma hizi zimeongeza unyanyapaa.

Wizara tayari imeandaa utaratibu mzuri wa madaktari kutoka Mnazi Mmoja wale wanaofanya mzunguko katika hospitali ya Mwembeladu. Ikumbukwe kwamba hospitali ya Mwembeladu ipo chini ya idara ya hospitali ya Mnazi Mmoja hivo mambo yote yanayohusiana na uzazi huratibiwa kwa pamoja.

Idara ya hospitali ya Mnazi Mmoja tayari imeipatia hospitali ya Mwembeladu ulinzi wa uhakika baada ya kutiliana mkataba na kampuni binafsi ambayo inatoa huduma hizo masaa 24.

### **Mwisho**

Idara ya hospitali ya Mnazi Mmoja imeshanunua gari maalum kwa ajili ya kuchukulia takataka za hospitali na gari hilo lipo hospitali ya Mnazi Mmoja na linatumika kwa hospitali zote mbili.

### **Chuo Cha Taaluma Za Sayansi Za Afya**

#### **Maoni Na Maagizo Ya Kamati**

Kwanza kamati imetaka Wizara kuwaendeleza walimu waliopo chuo cha Taaluma za Sayansi kielimu na kuongeza walimu wengine wenye sifa ili kuondoaa kasoro zilizopo na hatimae kutoa wahitimu watakaokuwa na sifa katika kada mbali mbali zinazotolewa chuoni hapo.

Pili kamati imesikitishwa sana na hali ya uvamizi wa maeneo na mgogoro wa ardhi ulipo katika eneo la chuo hicho, hivyo kamati imetaka Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa chuo kuhakikisha kuwa maeneo yote ya asili ya chuo yanapatikana.

### **Mwisho**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha darasa la ufundi sanifu wa vifaa ya tiba yaani *biomedical engineering* na kuitaka Wizara kuwaka fungu maalum la fedha kwa ajili ya kuvifanyia matengenezo vifaa vya hospitali, kwani kamati imebaini kuwa Serikali hutumia fedha nyingi kwa kununua vifaa vya hospitali lakini baadae vifaa hivyo kununuliwa kunakuwa hakuna matengenezo ya mara kwa mara yanayofanyika kwa vifaa hivyo. Hali inayopelekea mpaka vifaa kuharibika ama kufa kabisa.

### **Wajibu Na Utekelezaji**

Mhe. Spika, la mwanzo katika mwaka huu Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Chuo cha Taaluma ya Sayansi za Afya imewapeleka masomoni kwa viwango tofauti wafanyakazi 24 kati yao wafanyakazi 17 walianza masomo mwaka 2013 na saba wameanza masomo mwaka 2014, zikiwemo shahada za uzabibu, shahada za uzamili, shahada ya kwanza na stashahada. Aidha, wafanyakazi wa kawaida tayari wamesharudi masomoni.

Katika kuhakikisha kuwa Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya kinakuwa na walimu wa kutosha na wenye sifa, Wizara ya afya imewapatia chuo walimu wanenye katika hospitali ya Mnazi Mmoja wafanyakazi hao ni katika *clinical dentistry physical offices* na uuguzi. Wizara ya afya hivyo inashirikiana na uongozi wa wa Chuo cha Taaluma za afya karibu zaidi ili kuona kuwa matatizo yakiwa yanahusu upungufu wa walimu na wafanyakazi na mengineyo yanatatuliwa kila hali inaporohusu, bado kuna upungufu mkubwa wa fani ya walimu katika kada ya famasia.

### **Ya Pili**

Uongozi wa Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya umefanya ziara rasmi kwa Waziri wa Ardhi Makaazi, Maji na Nisharti kwa ajili ya kufuatilai suala la mgogoro wa ardhi na upatikanaji wa hati miliki mpya ya matumizi ya eneo hilo. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maazi, Maji na Nisharti alieleza kuwa suala la mgogoro limekwisha wameridhika na

kesi iliyokuwepo Mahakamani imeshamalizwa nje ya Mahakama, ambapo wadai na wavamizi wa eneo la Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya wameshaphatiwa eneo mbadala.

Mwanzoni mwa mwezi wa Februari 2015 uongozi wa Chuo cha Taalima za Sayansi za Afya ulifuatana na Mkurugenzi wa utumishi na Uendeshaji kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi kufuutilia kwa mara nyengine tena suala hilo, kama ilivyoikuwa maelezo ya Mhe. Waziri, Katibu Mkuu nae alitueleza kuwa suala la mgogoro uliokuwa umemalizika ni kwa uongozi wa Chuo cha Taalauma za Sayansi na Afya, urejeshe hati miliki ya eneo la Chuo uliopo ili itengenezwe nyengine mpya kwa mujibu wa eneo lililopo.

Uongozi wa Chuo cha Taaluma za Sayansi na Afya tayari umeandika barua ya kuirejesha hati hiyo kama ilivyoagizwa ambapo hivi sasa wanashubiri majibu ya barua hiyo. Aidha Wizara inaendelea na majadiliano na Wizara ya Ardhi ili kufikia muafaka wa suala hili.

### **Mwisho**

Wizara imepokea pongezi za maoni ya kamati na inatoa shukurani zake za dhati kwa kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kuliona suala la kuanzisha darasa la ufundu sanifu kwa vifaa vya tiba, yaani *biomedical engineering*, vile vile Wizara imepokea maoni ya kuweka fungu la fedha kwa ajili ya matumizi ya vifaa mbali mbali vya hospitali.

### **Bodi Ya Ushauri Ya Hospitali Binafsi**

#### **Maoni Na Maagizo Ya Kamati**

Kamati imeitaka Serikali kuititia Wizara ya Afya kuisaidia bodi kifedha ili iweze kujitegemea na hatimae kufanya kazi zake mbali mbali kwa ufaini. Aidha, Wizara iipatie bodi usafiri wake binafsi ili iweze kujipangia kazi za ukaguzi katika hospitali na vituo vya afya.

#### **Majibu**

Wizara inaifanyia kazi suala hili na imekuwa na utaratibu wa kuwapangia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali ingawa bado upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kila kitengo bado ni changamoto kutokana na ufinyu wa bajeti, aidha suala la kupatiwa usafiri tumelipokea na kutokana na ufinyu wa bajeti tunashindwa kutekeleza kwa wakati, lakini inapotokea huhitaji kwa usafiri kwa ajili ya ukaguzi kitengo hupatiwa usafiri huo.

### **Bodi Ya Chakula Dawa Na Vipodozi**

#### **Maoni Na Maagizo Ya Kamati**

Kamati inaitaka Serikali kuipatia bodi ruzuku ili kutekeleza shughuli zake mbali mbali na kuweza kulinda jamii ya Kizanzibari, pia kamati imeitaka Wizara kuipatia bodi fedha za kumaliza ujenzi wa Ofisi ya bodi mpya iliyopo Mombasa. Kamati imeitaka Wizara kuifanyia marekebisho sheria ya chakula dawa na vipodozi ya mwaka 2006 ili iwe mamlaka ya chakula dawa na vipodozi.

#### **Majibu**

Mhe. Spika, majibu na utekelezaji wa Wizara ni kama ifuatavyo, kwanza ombi la kupatiwa ruzuku bodi ya chakula dawa na vipodozi limeshawasilishwa Wizara ya Fedha kwa barua ya tarehe 13/3/2015 yenye kumbu kumbu No/CB/154/ 21301 hivyo bodi inategemea kupata ruzuku hiyo kwa mwaka ujao wa fedha 2015/16 baada ya ombi hilo kufanyiwa kazi.

Wizara imetoea jumla ya shilingi milioni 20 kwa ajili ya kusaidia kumaliza ujenzi wa afisi ya bodi iliyopo Mombasa.

### **Mwisho**

Mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya chakula dawa na vipodozi ya mwaka 2006 tayari yamewasilishwa kwenye kikao cha Makatibu wakuu ambapo imeshauriwa mapendekezo hayo yawasilishwe kwa Afisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, bodi tayari imeshawasilisha mapendekezo hayo kwa Mwanasheria Mkuu na Wizara inasubiri maelekezo yake.

### **Baraza La Tiba Asili Na Tiba Mbadala**

Mhe. Spika, maoni ya kamati ni kama ifuatavyo. Kwanza kamati imeitaka Wizara kuwa karibu na Baraza pamoja na kuwasikiliza matatizo yao mbali mbali, ili uwezo wa Baraza uwe ni kwa ajili ya kuweka mazingira ya tiba asili nchini na kuwafanya wafanyakazi wa Baraza hilo kujisikia kuwa ni sehemu ya wafanyakazi wa Wizara na pia kufuatiwa mionganoni miongozo mbali mbali pindi wanapohitaji. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa Baraza linafunguliwa *account* yake maalum kwa ajili ya urahisi wa kuhifadhi fedha zake.

### **Majibu Na Utekelezaji**

Mhe. Spika, hadi kufikia Februari 2015 Wizara imeipatia baraza jumla ya Tanzania shilingi milioni 4,700,020,000/= fedha hizi zimetumika katika utekelezaji wa mpango kazi wa bodi hii ikiwemo kufanya kikao chake cha sita cha Baraza la tiba asili na tiba mbadala, kutengeneza kanuni mpya na tayari kanuni hizo zimeshaanza kutumika, kutafsiri sheria ya tiba asili na tiba mbadala kwa lugha ya kiswahili ili iwe rahisi kwa watumiaji.

Pia baraza limeandaa mkutano maalum na wakuu wa taasisi za Serikali ili kujadili hali halisi ya tiba asili juu ya usajili na uuzaaji wa dawa misikitini na barabarani pamoja na uingizaji dawa ndani ya Zanzibar.

Pili, baraza la tiba asili na tiba mbadala bado halijafunguliwa *account* mbali na jitihada nyingi zimechukuliwa na uongozi wa baraza hili.

### **Baraza La Wauguzi**

#### **Maoni Na Maagizo Ya Kamati**

Kamati ilitaka Wizara kufuatalia upatikanaji wa bajeti ya baraza kama ilivyopangwa ili baraza liweze kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuendesha vikao, ufuataliaji na tathmini kuhusiana na baraza.

Kamati inaishauri Wizara kutafuta mbinu za kushiriki mikutano ya kitaifa na Kimataifa Baraza la Wauguzi Zanzibar ili kuenda sambamba na mabadiliko ya ukuaji wa Taaluma za uhusiano na Baraza.

Kamati imeitaka Wizara kuharakisha kukamilisha kwa sheria mpya ya Baraza la Wauguzi na Wakunga ili Baraza liwe na mamlaka kamili ya kufanya kazi ikiwa pia kuweza kupatiwa changamoto katika Baraza.

### **Majibu**

Baraza linalo bajeti yake ambayo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15 limepangija kutumia jumla ya shilingi milioni 37 kwa kazi zake za kawaida, ikiwemo kuendesha vikao na kazi za ufuataliaji, ambapo baadhi ya fedha hizo zimetumika kufanya marekebisho sheria ya wauguzi ya mwaka 2014.

Baraza kwa kushirikiana na *Agakhan University* limehudhuria mikutano ya kimataifa nchini Burundi, katika mikutano huo maafisa wetu waliweza kuwasaidia wauguzi wa Burundi kutengeneza sheria ya Baraza la wauguzi.

Mwisho Sheria ya Baraza la Wauguzi na Wakunga tayari limeshakamilika imeshapitishwa katika baraza hili tukufu, imetiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mwisho kabisa Mwenyekiti wa baraza hili tayari ameshateuliwa na Mhe. Rais tayari kupata na wajumbe wengine kuanza kazi zao.

### **Afisi Za Timu Za Afya Wilaya**

#### **Maoni Na Maagizo**

Moja kamati imoitaka Wizara kulitafutia ufumbuzi tatizo la usafiri wa timu za afya za Wilaya ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na kuepuka kutumia bajeti yao katika kufanya matengenezo ya mara kwa mara.

Pili, katika kupunguzwa tatizo la upungufu wa dawa na kukaa kamati inashauri kuanzisha sheria ya utaratibu wa kuchangia huduma za afya hasa tukizingatia kwa sasa mara nyingi watu hulazimika kununua madawa na vifaa wanavyoandikiwa, ambapo ingekuwa ni wepesi kama utaratibu wa kuchangia ungekuwepo.

Tatu, kamati imoitaka Serikali kubeba gharama za malipo ya umeme pamoja na malimbikizo ya madeni yake ili wafanyakazi wanaoendelea kukaa katika nyumba za Vituo vya afya waondokane na kulipa madeni ya kurithi, na pia Serikali iandae utaratibu mzuri wa kulipaumeme katika nyumba na vituo vya afya.

Kamati imoitaka Serikali kuipatia Wizara bajeti ya kutosha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa ili hatimae Wizara iweze kupatia vituo vya afya dawa na vifaa kwa wakati ambao zitawenza kutumika kwa muda mrefu kabla ya kumalizika muda wake. Pia kamati imoomba Wizara kuwapatia posho la dhamana watendaji wa timu za afya za wilaya.

Tano, Kamati imeishauri Wizara kuandaa utaratibu wa kuweka ulinzi katika vituo vya afya kwa kuwatumia wana jamii wenyewe waliopo katika maeneo ya vituo ili kupunguza wizi na uharibifu wa vifaa.

Mwisho kamati imeshauri Wizara kuzihusisha timu za Afya za Wilaya katika kufanya uteuzi wa wafanyakazi wasio wataalam wapya, *supporting staff* katika sehemu husika hasa kwa sehemu za mashamba ili kupunguza matatizo yanayojitekeza ikiwemo kukosa nafasi ya ajira kwa wahudumu wanaojitolea.

### **Majibu Na Utekelezaji**

Kwa hatua za awali Wizara kuititia Ofisi za *DANIDA* imemkodi mtaalam wa kufanya upembuzi wa kina kutathmini idaidi ya magari yaliyopo Wizarani hapo pamoja na mahitaji yake, Mtaalam huyo yaani *Transport officer* tayari amewasilisha ripoti yake kwa wahusika, tatizo la usafiri kwa timu za afya za Wilaya zitapatiwa ufumbuzi pale hali ya fedha itakaporuhusu.

Sera ya afya ya mwaka 2011 imepitishwa na moja ya mikakati ya sera ni kuwataka wananchi kuchangia huduma za afya, kwa sasa Wizara imo katika hatua ya kutayarisha utekelezaji wa mchakato huu rasmi baada ya kuruhusiwa na Serikali katika ngazi ya Wilaya na rufaa.

Kuhusu deni la umeke katika vituo vya afya na nyumba za wafanyakazi imewasilishwa Shirika la Umeme ili deni lile liweze kutafutiwa utaratibu wa kulipwa kidogo kidogo badala ya kuingizwa kwenye mita za *TUKUZA*.

Kwa hivi sasa Wizara kuititia sehemu ya dawa dhana na vifaa ina utaratibu maalum wa vituo vyote vya daraja zote chini ya mpango wa *Zanzibar Integrated Logistic System bills* ambao utaratibu huu unamuwezesha mhudumu kuagiza dawa kutokana na mahitaji ya kituo husika, kuhusu vifaa tayari awamu ya mwanzo ya mgao wa vifaa vimegaiwa kwa mujibu wa maombi yaliyoombwa kuititia maombi maalum kwa mujibu wa daraja la kituo. Mpango huu umefadhiiliwa na Shirika la *DANIDA*.

Pia Wizara inaendelea kutathmini mchango wa jamii wa kuhakikisha kwamba vituo vyote vinalindwa kwa utaratibu maalum hasa ukitilia maanani kuwa hivi sasa Wizara ina utaratibu wa kuajiri walimu, Wizara inatoa wito kwa zile sehemu ambazo hazijaansisha utaratibu huu waanzishe ili kudhibiti wizi katika vituo vya mjini na mashamba.

Kwa kuwa suala la uajiri hivi sasa linashughulikiwa na Wizara mpya ya Afisi ya Rais Kazi, Utumishi wa Umma kwa mujibu wa sheria za utumishi Serikalini, nafasi za wafanyakazi wasiokuwa wataalam *subording staff* huwa zinatangazwa kama nafasi nyengine za kitaalam.

Kwa haya Mheshimiwa Spika, yaliyotakiwa na kamati naomba kuwasilisha Ahsante. (*Makofii*)

**Mhe. Spika:** Tunakushukuru Mhe. Waziri wa Afya na kabla sijamkaribisha Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, nimearifiwa kwamba sasa *quorum* ipo nzuri na kwa maana hiyo kwanza tumalize kazi ile ambayo tuliiwacha uporo

kidogo kusubiri wale wanaocherewa, waweze kuingia ambao walilaumiwa kwa makofi mengi kwa kila mmoja aliyeingia.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, alikwisha maliza kufanya majumuisho yake na pia kuwasilisha ripoti ya mwaka 2014/15.

Kwa hivyo sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubali na kupokea taarifa ya utekelezaji wa Serikali kuhusu ripoti ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, utekelezaji wa mwaka 2013/2014 na kupokea ripoti ya kamati hiyo mwaka 2014/15 wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** taarifa ya utekelezaji imepokelewa lakini pia ripoti ya mwaka 2014/15 ifanyiwe kazi na Serikali.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, na mimi naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, afya na uzima tukawa katika utekeleza wa shughuli za Baraza la Wawakilishi.

Pili kwa heshimiwa kubwa na taadhima naomba kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Baraza yaliyo tokana na ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na na Ustawi wa Jamii ya Mwaka 2013/2014 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza nazungumza mapendekezo ya Kamati. Kamati ilitaka serikali kuzipa kipa umbele taasisi zake katika kuwapatia hati miliki kila sehemu ya vitega uchumi vyake.

### **Utekelezaji**

Jitihada za kuandika Wizara ya Ardhi, Nishati na Madini, kuhusu hati miliki imechukuliwa na bado tunasubiri kupatiwa hizo hati miliki.

Pili, Kamati imetaka serikali kuchukua hatua za kuzikagua upya shule mpya zilizojengwa Skuli ya Dimani na nyenginezo.

### **Utekelezaji**

Wizara tayari imezipitia Skuli zote zilizojengwa kwa Mkopo wa *World Bank* na kadhalika. Kwa sasa wizara imeshatenga jumla ya shilingi milioni 100 kwa kazi hiyo. Skuli ya Uzini inaendelea na ukarabati huo. Pia ukarabati katika Skuli ya Muwanda na Chwaka Tumbe umo katika matayarisho.

### **Maelezo**

Wizara inaendelea kurekebisha kasoro zilizojiteza katika shughuli hizo na si nyenginezo kadiri ya fedha zinavyopatikana.

Tatu, Kamati inataka jamii kuunga mkono jitihada ya Serikali na Wafadhili na kuanzisha mradi wa lishe maskulini Unguja na Pemba. Ili mradi huwo uwe endelevu na kuhakikisha kwamba mradi unapunguza utoro wa wanafunzi na kuwapa wanafunzi afya na lishe bora.

### **Utekelezaji**

Mradi wa Lishe katika skuli ni kweli unasaidia kuendeleza elimu na afya bora. Wizara inapendelea kuendeleza mradi huu kwa kuhamasisha jamii, lakini pia inategemea fedha katika bajeti ya mwaka 2015/2016, itaingizwa.

Wizara inajaribu kuangalia uwezekana wa Shirika la PCD, yaani *Partnership for Child Development* yaani kuongeza muda wa mradi unaoendelea hivi sasa. Aidha, Wizara inaendelea na mazungumzo ya Jumuiya ya Zanzibar, *millennium foundation* katika kusaidia mradi huu na Jumuia inaonekana imekubali.

Nne, Kamati inaitaka Wizara ya Fedha, kuipatia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali fedha za kodi ya Bandari kwa ukamilifu wake ili wizara iweze kutengeneza madawati kwa skuli zake.

Aidha, Kamati inataku Wizara ya Fedha kuipatia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mchango halisi ya Fedha za kodi ya madawati inayokusanywa ili wizara ijipange vizuri katika utekelezaji wa kazi hiyo.

Tano, Kamati inaagiza wizara kuwapatia walimu wa Skuli ya Msingi mafunzo ya kutosha kuhusiana na mtaala mpya na kuhakikisha mafunzo hayo yanaendelea vizuri.

### **Utekelezaji**

Wizara tayari imeshawapatia walimu 450 mafunzo juu ya matumizi wa mtaala mpya wa elimu ya msingi.

### **Maelezo**

Wizara inaendelea kutafuta wahisani watakaosaidia matayarisho ya vitabu vya masomo ya kiarabu na dini na michezo katika ngazi ya elimu ya msingi. Kituo cha elimu mbadala Rahaleo.

### **Mapendekezo**

Kamati, inaitaka wizara kupanga mikakati, kwa kukipatia Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo na Kituo cha Elimu cha Watu Wazima Forodhani, walimu wa kutosha wa fani mbali mbali hasa fani ya utegaji kwani fani hiyo ina upungufu mkubwa wa walimu.

### **Utekelezaji**

Ni kweli kuna upungufu wa walimu katika skuli hizo na kile cha Watu Wazima Forodhani. Wizara inahitaji kutafuta walimu wa kutoka skuli ya Msingi ambapo wataweza kusaidia kusomesha katika vituo hivyo. Hata hivyo Wizara ya Elimu, Mbadala na Watu Wazima imepatiwa nafasi tatu za ajira ili kuweza kupunguza changamoto za kutokuwa na walimu wa kutosha.

### **Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaitaka wizara kuitia upya dhamira ya kuanzisha kwa Kituo cha Walimu Mbadala cha Rahaleo na Kutuo cha Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni ili kuweza kubaini mahusiano baina ya vituo hivyo viwili na kutatua upungufu unaojitokeza hivi sasa.

### **Utekelezaji**

Katika kuanzisha malengo ya kuwezesha wanafunzi wanaohitimu katika Elimu Mbadala katika Vyuo vya Amali viliopo. Wizara imeanza kuvii marisha programu zinazotolewa katika vituo vya amali vya elimu mbadala ili ziendelee na matayarisho ya vijana kuweza kujiunga na Vyuo vya Amali vilioko Mkokotoni.

### **Maelezo ya Kamati**

Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa Kituo cha Rahaleo kinapatiwa eneo la haraka la karakana ili wanafunzi wa fani hiyo, wapate mazoezi ya vitendo na hatimaye kujenga ufahamu mzuri wa kazi zao.

### **Utekelezaji**

Kwa sasa ni kweli Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo hakina Makarakana kwa wanafunzi wa mazoezi ya vitendo. Hata hivyo Wizara imepanga kuvimarisha vituo vipyta vinavyojengwa Unguja na Pemba kwa kuvijengea *workshop* ili kufanya kazi za *practical* kwa wanafunzi wanaosoma humo.

Nne, Kamati inaitaka wizara kuchukua hatua za haraka za kufanya matengenezo ya ukubwa katika kituo cha Elimu ya Watu Wazima Forodhani.

### **Utekelezaji**

Ukarabati wa Ukuruta katika kituo cha Elimu Watu Wazima Forodhani kimeshaanza. Wizara inaendelea na wazo la Kamati la kufanya ukarabati wa Skuli yenye na zitachukuliwa baada ya kupatikana kwa bajeti.

### **Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar**

#### **Mapendekezo ya Kamati**

Kwa kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar imekabiliwa na upungufu wa fedha za kuwakopesha wanafunzi wake. Kamati inashauri taasisi nyengine za Fedha za Zanzibar ziunganisha hatua zake za kuwakopesha wanafunzi wa elimu ya juu ili kusiwe na matatizo ya kukosa mkopo. Wanafuzi na elimu ya juu kwa kutegemea Bodi ya Mkopo pake yake wataendelea kukumbana na tatizo hilo.

### **Utekelezaji**

Ni kweli bodi inakabiliwa na upungufu wa fedha na kuwakopesha wanafunzi katika kujiedeleza elimu ya juu. Bodi katika kukubaliana na hili imeanza kuwasiliana na Mfumo wa Fedha wa Jamii wa Zanzibar (ZSSF) ili uweze kutoa huduma hii. ZSSF imelipokea ombi hili na imelikubali.

Kamati inaitaka serikali kupatia Bodi ya Fedha kama zinazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi ili kuepusha Bodi kuridhi madeni ya miaka minge ya nyuma, kuletewa hivi sasa.

### **Utekelezaji**

Katika utekelezaji mapendekezo haya ya Kamati ili kuepusha urithi wa madeni ya miaka ya nyuma. Wizara tayari imeshawasilisha maombi yake Wizara ya Fedha kuona uwezekano wa serikali kutoa fedha kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kama inavyoainishwa na Baraza la Wawakilishi.

### **Maelezo ya Kamati**

Kamati imebaini ucheleweshaji wa upatikanaji wa fedha za Bodi ya Mikopo katika hali inayowapa ugumu wanafunzi kuendelea na masomo yao. Kutokana na hali hiyo Kamati imeshauri serikali kuanzisha kodi ya kuchangia elimu ya juu ya fedha itakazopatikana ziingizwe kwenye bodi kupitia wanafunzi wanaotaka mikopo.

### **Utekelezaji**

Kweli ni vigumu kutekeleza majukumu ya Bodi kwa kutegemea bajeti ya serikali peke yake. Kwani idadi ya wanafunzi wanaotegemea mikopo hiyo inaongezeka mwaka hadi mwaka. Wizara inalifanya kazi pendelezo la Kamati ya kuanzisha bodi mbali mbali ili kuondokana na tatizo hili.

### **Maelezo ya Kamati**

Kamati inaitaka wizara kuweka mkakati wa kuipa Bodi ya Elimu ya Zanzibar jengo la kutosha ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi. Utekelezaji katika kuhakikisha kuwa Bodi inajenga la kutosha kwa kazi zake, Wizara inampango wa muda mfupi na muda mrefu.

Muda mfupi kutafuta majengo mengine yoyote na kuwapatia eneo Bodi ya Mikopo ya muda mrefu hii Bodi ya Mkopo kujengewa Ofisi yake.

## **Ofisi Kuu Pemba**

### **1) Maelezo ya Kamati**

Kamati inaitaka wizara kusaidia Ofisi Kuu Pemba katika kufatilia fedha za malimbikizo ya posho za likizo kwa walimu 1,145 yenye thamani ya shilingi milioni 136 na feddha zilizokatwa kwa makosa na mishahara ya walimu 159 yenye thamani ya shilingi 18 milioni, ambazo zimekwama Wizara ya Fedha Unguja na idhini ya kufikia malipo imetolewa na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishia wa Umma ya tarehe 10 mfungo tisa mwaka 2012.

### **Utekelezaji**

Mawasiliano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanaendelea katika Wawakilishi wa tatizo hili la malimbikizo ya posho na likizo ya walimu, fedha zake zinapatikana kadiri itakavyo yimkinika.

### **2) Maelezo ya Kamati**

Kamati inaitaka serikali kuipa wizara fedha za bajeti kama inavyoidhinishiwa ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### **Maelezo**

Wizara inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili kupatikana Fedha kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. Hii si kwa Ofisi ya Pemba peke yake, lakini kwa Ofisi zote za wizara.

3) Kamati inaitaka wizara kutoresha Ofisi ya Mkurugenzi Pemba ili iweze kufanyakazi kwa ufanizi zaidi.

### **Utekelezaji**

Wizara ina mpango wa kuitafutia Ofisi ya Mkurugenzi Pemba eneo lenye Ofisi zaidi litakalokidhi mahitaji ya kazi zao na yenye mazingira mazuri ya kazi.

4) Kamati inaitaka Wizara ya Elimu Pemba kufanya mazungumzo na Shirila la Umeme iliyopo Pemba ili kuweza kufahamu madeni yao ya umeme na maji na kuweza kuondoa utata uliyokuwepo katika madeni hao.

### **Utekelezaji**

Wizara imepokea maagizo haya na itatekeleza kama iwezavyo.

5) Maelezo ya Kamati inaitaka Wizara kuendelea kuelimisha jamii katika kuwapa maelezo watoto wao ili kuwaepusha na ndoa za utotonu na vitendo vya ubadhilifu.

### **Utekelezaji**

Pamoja na kuwa wizara inafanya kazi suala la kuelimisha jamii kama ilivyoolezwa katika Sera ya Elimu ya mwaka 2006, kazi hii inafanywa kwa kupitia vikao mbali mbali vya jamii na wanafunzi. Wazo la Kamati limeongeza msisitizo na wizara inalipokea wazo hilo. Kamati inashauri wizara kuwa makini katika kulipaji wa deni la fidia ya vipando kwa wananchi wa Vitongoji ili kuepusha kuzuka kwa migogoro katika jamii na kujitokeza watu wasiostahiki katika kupokea fidia hiyo.

### **Utekelezaji**

### **Hatua zitachukuliwa**

7) Kamati inaitaka Wizara kufanya marekebisho Ofisi takwimu ya kuweka air *condition* ambazo zitasaidia katika kuzitunza *computers* ziliopo kuhakikisha takwimu zenewe pia zinawekwa vizuri.

## **Utekelezaji**

Wizara katika jitihada za kujenga uwezo Ofisi zake ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa kazi kwa ufanisi, Wizara italizingatia pendekezo la kamati katika kuweka bajeti ijayo ya mwaka 2015/16 kwa kuweka *air condition* katika chumba chenye *computer* 4 ziliomo katika Ofisi hizo.

Nane, Kamati inaitaka Wizara kuipa kipa umbele Skuli ya Kojani kwa kuipatia walimu wa sayansi kwani kwa kipindi kirefu wanafunzo wa skuli hiyo wamekosa kusoma masomo ya sayansi na inafanya wakose fursa hiyo.

## **Utekelezaji**

Kwa sasa Skuli ya Kojani imeshapatiwa mwalimu wa somo la sayansi, jitihada za kuajiri mwalimu mwengine wa kudumu zinachukuliwa kwa haraka sana. Mhe. Spika, sasa najibu hoja za Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika yaani PAC ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

Hoja namba 12.1 inasema:

Mradi wa kuimarisha elimu ya lazima pendekezo la Kamati, jumla ya wakandarasi watatu walitumika katika kuimarisha ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Paje Mtule, Kombeni na Tunguu baada ya Wizara kukatisha mkataba na mkandarasi wa mwanzo. Wakandarasi hao watatu walitumia jumla ya shilingi milioni 895,000,000 badala ya milioni 152,000,000 ambazo zilikuwa zitumike kwa mkandarasi wa mwanzo. Kamati inaitaka Wizara kuzingatia taratibu za kisheria inapotafuta ujenzi na utumizi wa fedha za umma.

## **Utekelezaji**

Taratibu za ununuzi katika kuwapata wakandarasi hao watatu uliokamilisha ujenzi wa skuli zote tatu umefata kwa makini sana na napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu skuli hizo tatu ya Paje Mtule, Dimani na Kombeni zimeshamalizika na sasa hivi wanafunzi wanasoma katika skuli hizo.

Hoja namba 24.1.1 Kamati inaishauri Serikali kuwaingizia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amani fedha zote zinazotokana na kodi ya Bandari ili iweze kuweza kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

## **Utekelezaji**

Ni kweli Wizara inapata fedha kidogo sana kulingana na kiwango kinachokusanywa cha kodi ya Bandari na kiwango kilichokubaliwa kwamba Wizara itengewe katika pesa hizo bilioni 2 katika kodi ya Bandari ili iweze kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo Wizara inaamini kuwa Wizara ya Fedha itaendeleza maoni haya ya Kamati katika kufanikisha lengo lilokusudiwa.

Hoja namba 43.1 Hesabu za mwisho za mwaka 2012/2013

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri ni sawa kabisa Kamati ya *PAC* ingetaka utoe taarifa ya utekelezaji kuhusiana na mambo ambayo Kamati hiyo *PAC* ilielekeza kwa Wizara yako. Lakini Kamati ya *PAC* bado haijafikia hatua ya kuwasilisha ripoti yake. Kwa hivyo ninafikiri ningekuomba hizi hatua nyengine tusubiri wakati Kamati hiyo itapowasilisha ripoti yake na Wizara mbali mbali zitatoa utekelezaji wa maelekezo na maagizo ya Kamati hiyo ya *PAC* kwa yale maeneo ambayo ilionekana kwa Wizara hizo mbali mbali.

Kwa hivyo, hii ningekuomba ukaiweka kidogo ili isubiri wakati wa Kamati inayohusika. Kama kwa upande wa ile ripoti ya utekelezaji kutokana na Kamati ya Wanawake na Ustawi wa Jamii umemaliza kwa hiyo nadhani itakuwa inatosheleza kwa kiasi hicho. Sehemu nyengine hii inahusu Kamati ya *PAC* ambayo itakuja baadae.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, ninakushukuru kwa muongozo wako na naomba kuwasilisha kwa hivi sasa. (*Makofii*)

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii Wanawake Vijana na Watoto):** Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti, wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Wanawake, Vijana na Watoto

napenda kusoma muhtasari wa Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema, pamoja na kutuwezesha kukutana siku ya leo katika Baraza letu ili kuendelea kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha muhtasari wa Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya kudumu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi zinavyoeleza kupitia kifungu cha 108(14) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2012.

Aidha, Kamati katika utendaji wake wa kazi katika Wizara zote tatu ambazo imepangawa kuzisimamia, imepokelewa vizuri na kutohana na hilo Kamati inapenda kuchukua fursa hii adhimu kuzishukuru Wizara hizo na kuzitakia mafanikio mazuri katika utendaji wa majukumu yake.

Mhe. Spika, jitihada kubwa na mashirikiano waliyotunesha wajumbe wa Kamati hii, yalikuwa ndio msingi muhimu wa kuyafkia malengo ya Kamati katika kutekeleza majukumu yake, hivyo kwa moyo wa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa jitihada na mshikamano wao kwa muda wote wakati Kamati ilipokuwa katika kazi zake za ufanitaliji maagizo mbali mbali kwa Wizara, Idara pamoja na Taasisi inazosimamia.

Mheshimwa Spika, naomba sasa niwatambue Wajumbe wa Kamati hii ambao kwa mashirikianao makubwa wameiwezesha Kamati kufanya kazi zake vizuri na kwa ufanisi mkubwa. Wajumbe wenyewe ni kama wafuatayo:-

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Farida Amour Mohammed	Mjumbe
4. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
5. Mhe. Abdi Mosi Kombo	Mjumbe
6. Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
7. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Mjumbe

Mhe. Spika, pia napenda kuwataja Makatibu wetu wa Kamati ambao huwa tunashirikiana nao katika kazi zetu za Kamati na wamekua wakitusaidia kwa karibu katika kufanikisha kazi zetu nao ni:

1. Ndg. Asha Said Mohammed, na
2. Ndg. Abubakar Mahmoud Idd

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii katika kazi zake iliweza kusimamia utekelezaji wa shughuli zilizo chini ya Kamati hii kwa kufuatilia utekelezaji wa malengo ya Bajeti za Wizara, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na wananchi na utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyoagizwa kupitia Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka uliotangulia.

Mhe. Spika, Kamati katika utekelezaji wa kazi zake imepewa mamlaka ya kuzisimamia Wizara tatu pamoja na Idara na Taasisi zilizomo katika Wizara hizo. Wizara zenyewe ni Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kiujumla Kamati imeridhishwa na utendaji wa Wizara ambazo inazisimamia. Hata hivyo, bado kuna kasoro ndogo ndogo za kiutendaji kwa baadhi ya taasisi zilizomo kwenye Wizara hizo ambapo juhudzi za ziada zinapaswa kuchukuliwa na Taasisi hizo ili kuleta ufanisi wa kiutendaji kwa nia ya kuziletea mafanikio Taasisi hizo na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

## **WIZARA YA AFYA**

Mhe. Spika, Kamati ilipokuwa inafuatilia utekelezaji wa Wizara hii imebaini kuwa, Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu yake mbali mbali kupitia Idara zake zilizomo ndani ya Wizara. Hata hivyo Wizara inakabiliwa na changamoto kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, muhimili mkuu wa Wizara ya Afya ni Idara ya Hospitali ya Mnazi mmoja na Idara ya Tiba, kwani Idara hizo ndizo zinazotoa huduma za moja kwa moja kwa wananchi. Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati katika Idara hizi changamoto zilizojitokeza ni pamoja na ufinyu wa bajeti. Hii ni changamoto kubwa ambayo Kamati imekuwa ikikabiliana nayo kwa Wizara zote tatu ambazo inazisimamia. Katika Hospitali ya Makunduchi kiwango cha fedha wanachopatiwa hakilingani na kile kiwango cha fedha walichokionba kwa kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Kwa mfano ufinyu wa fedha katika Hospitali umepelekea gari la kubebia wagonjwa kukosa mafuta ipasavyo na kukwamisha utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mhe. Spika, uhaba wa nyumba za madaktari pia ni tatizo katika Idara hizi kwani Kamati imebaini kuwa uhaba huo unapelekea madaktari kujibana katika nyumba chache zilizopo hali ambayo inahatarisha usalama wa afya zao pamoja na mali zao. Hili limejitokeza sana katika Hospitali ya Makunduchi kwa Unguja na Kituo cha Afya cha Kojani kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, kwa upande wa Hospitali ya rufaa ya Mnazi mmoja ambayo ndio tegemeo la wagonjwa walio wengi haswa wale wenyewe kipato cha chini hali sio shwari kwani Kamati ilikutana na changamoto mbalimbali ikiwemo mazingira ya wodi kutoridhisha kwa afya za wauguzi na wagonjwa. Kamati imebaini hali hiyo katika wodi ya wagonjwa wa sukari sehemu ya wanawake na wanaume mazingira yake hayapo salama kiusafi kutokana na uhaba wa vitendea kazi (*gloves* na jiki) hali ambayo inaweza kusababisha maambukizi ya maradhi mengine.

Mhe. Spika, Kamati imebaini uchakavu wa wodi, uhaba wa vitendea kazi kama vifaa vya kufungia vidonda kwa wagonjwa (*dressing equipment*) na baadhi ya mafeni yaliyopo katika wodi hizo kutofanya kazi.

Mhe. Spika, kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuongeza idadi ya nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Makunduchi ili wafanyakazi wapate makazi ya kutosha na kuweza kukaa katika sehemu ambazo zitalinda usalama wa afya zao na mali zao.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuzifanyia matengenezo wodi hizo na kuzipatia vifaa vya kutosha ili watendaji wafanye kazi zao kwa ufanisi na usalama wa Afya zao na wagonjwa wanaowahudumia.

Mhe. Spika, Kamati ilipotembelea wodi ya wagonjwa mahututi (*ICU*) kongwe imebaini upungufu wa watendaji ambapo kwa sasa kuna muuguzi mmoja tu na mahitaji ya wodi hiyo ni wauguzi watano ili kila mgonjwa aweze kupatiwa huduma nzuri na uangalizi wa kutosha. Kamati inaitaka Wizara kuongeza watendaji katika wodi ya wagonjwa mahututi kongwe kwa sababu muuguzi mmoja hatoshi katika kuwashahudumia wagonjwa watano kwa wakati mmoja na inakuwa ni vigumu kwa muuguzi huyo kutoa huduma iliyo bora kwa wagonjwa wote kwani taratibu za utoaji huduma bora wa afya huzingatia zaidi idadi ya watoa huduma na idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa.

Mhe. Spika, uhaba wa Wauguzi na Madaktari wa Mifupa katika Hospitali ya Mnazi mmoja bado ni changamoto kubwa inayoikabili wodi ya mifupa, kwani muuguzi mmoja hutoa huduma katika wodi nzima na hivyo hujikuta anafanya kazi nyingi ambazo zipo nje ya uwezo wake, hatimae huduma haziwafikii walengwa katika kiwango kinachostahiki.

Mhe. Spika, kutokana na tatizo la uhaba wa wataalamu hao Kamati inaishauri Serikali kutafuta mtaalamu wa mifupa haraka iwezekanavyo na kuwashajihisha watendaji kuijendeleza katika fani hiyo kwani matatizo ya mifupa kwa sasa yamekua yakijitokeza mara kwa mara katika nchi yetu kutokana na ongezeko kubwa la ajali za barabarani.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha kitengo cha matibabu kwa waathirika wa madawa ya kulevyia (*methodonic unit*) katika Hospitali ya Kidongo chekundu kwa ajili ya kuwasaidia wahanga hao hasa wale wanaotumia madawa hayo kwa njia ya kujidunga. Kamati inaitaka Wizara kukiimarisha kitengo hicho kwa kukipatia vifaa vianavyotosheleza ili malengo yaliyokusudiwa ya kuanzisha kitengo hicho yafikiwe na kuwasaidia vijana ambaeo ndio nguvu kazi ya taifa.

Mhe. Spika, Kamati inaishauri Wizara kuipatia Hospitali ya Kidongo chekundu kifaa cha kuzimia moto (*fire extinguisher*) na kuwapatia watendaji wake taaluma ya kujikinga na ajali ya moto hasa wale wanaoshughulika na kazi za jikoni ili iwasaide katika kupambana na janga la moto pindi litakapotokezea.

Mhe. Spika, Kamati ilitembelea ujenzi wa Ofisi Mpya ya Bodi ya Chakula, Dawa na vipodozi na ilifurahishwa na hatua iliyofikiwa. Hata hivyo Kamati imebaini kuwa bado Bodi inakabiliwa na matatizo mbali mbali ikiwa ni pamoja na kutopatiwa ruzuku kutoka Serikalini na hivyo fedha wanayotumia katika kazi zao za kila siku zinatokana na makusanyo yanayofanywa na Bodi.

Mhe. Spika, Kamati katika ripoti yake ya mwaka wa fedha 2013/2014 iliaigiza Serikali kuipatia Bodi ruzuku lakini kwa bahati mbaya sana agizo hilo halikutekelezwa. Hivyo Kamati kwa mara nyengine inaiagiza Serikali kuipatia Bodi ruzuku ili iweze kutekeleza kazi walizojipangia kwa ufanisi, kwani fedha zinazokusanywa na bodi pekee hazitoshelezi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa bodi inaenda sambamba na mabadiliko yaliyopendekezwa na bodi nyengine zilizopo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo wanashirikiana katika utekelezaji wa kazi zao. Kamati inaiagiza wizara kuharakisha marekebisho ya Sheria Nam. 2 ya mwaka 2006 ya Chakula, Dawa na Vipodozi ambayo imeshapelekwa kwa makatibu wakuu kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho tokea mwaka 2013.

Mhe. Spika, kamati inaitaka wizara kuharakisha marekebisho hayo kwa sababu nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilizotiliana mikataba ya kuwa na sheria zinazofanana katika sekta ya afya ikiwemo Tanzania, Kenya, Unganda na Rwanda wameshabadilisha sheria zao za bodi isipokuwa Zanzibar pekee.

Mhe. Spika, kamati ilipata nafasi ya kukutana na Uongozi wa Ofisi Kuu Pemba na kupokea taarifa ya utekelezaji, kutembelea Kituo cha Afya cha Kojani, Kituo cha Afya cha Ukutini na Maabara ya Mkemia Mkuu.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa kukosekana kwa jengo la Ofisi kwa ajili ya shughuli za wizara ni tatizo kubwa linaloikabili Ofisi Kuu Pemba, kwani ofisi zao zipo katika jengo la Hospitali ya Wete ambalo ni finyu na watendaji wanakosa ufanisi wa kazi zao kutoptana na kuwa hakuna utilivu wa kutosha. Hivyo, kamati inaitaka Serikali kuipatia Ofisi Kuu Pemba majengo ambayo hayatumiki kwa muda mrefu kama jengo la Hoteli ya Wete ili walifanyie matengenezo na hatimae waweze kutumia kwa shughuli zao za kiofisi.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa vituo vya afya vinakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo kukosekana kwa usafiri wa uhakika kwa ajili ya kubebwa wagonjwa hali inayohatarisha maisha ya wagonjwa. Hivyo, kamati inaitaka wizara kuvipatia vituo usafiri wa uhakika hasa vituo viliyopo katika maeneo ya visiwa, kwani watendaji wa vituo hivyo wanakuwa katika wakati mgumu pindi wanapokuwa na mgonjwa wa dharura anayehitaji kupatiwa rufaa na ambapo kunakuwa hakuna usafiri wa uhakika wa majini na nchi kavu.

Mhe. Spika, aidha kamati ilipotembelea Kituo cha Afya cha Kojani na Ukutini imebaini uhaba wa wataalamu, uhaba wa vitendea kazi, uchakavu wa nyumba na vituo kukosa ulinzi wa uhakika hasa Kituo cha Kojani ambacho wafanyakazi wake wengi ni wanawake. Hivyo, kamati inaishauri wizara kuchukua jitihada za makusudi za kurekebisha kasoro zinazojitokeza katika vituo vya afya na kufanya matengenezo ya nyumba za Kojani ili wafanyakazi waweze kuzitumia kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia katika Wizara hii ya Afya, kamati inaipongeza na kuishukuru sana wizara kwa jitihada yake ya kuipeleka Kamati yetu Tanzania Bara kwenda kujifunza mambo mbali mbali yanayohusiana na huduma za afya hasa kwa kutembelea Bohari Kuu ya Madawa, Hospitali ya Muhimbili, Hospitali ya MOI na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambapo sehemu zote hizo kamati ilijifunza mambo mengi na ilibaini uhusiano wa moja kwa moja uliopo baina ya Wizara ya Afya ya Tanzania Bara na Wizara ya Afya ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kutoa fursa za kimafunzo kwa kamati yetu kama ilivyofanya Wizara ya Afya ili wajumbe wapate kujifunza yale mazuri wanayoyafanya wenzetu na kuweza kuishauri Serikali yetu.

## **WIZARA YA UWEZESHAJI, USTAWI WA JAMII, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO**

Mhe. Spika, kamati ilipokuwa inafuatilia utekelezaji wa wizara hii kuitia taasisi zake mbali mbali katika kwa vipindi tofauti, imeridhishwa na utekelezaji huo. Hata hivyo, kamati imesikitishwa na changamoto ambazo wizara inakabiliana nazo.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa, kukosekana kwa kifaa cha *DNA* kunapelekea kutopatikana kwa ushahidi wa kitaalamu kwa kesi za udhalilishaji hasa kwa kesi za watoto ambao wana magonjwa ya akili na ambao hawana uwezo wa kujieleza mpaka kupatikane kwa vipimo cha *DNA* kwa ajili ya uchunguzi na majibu ya kipimo hicho yanasadida katika kutoa ushahidi.

Mhe. Spika, kwa kuwa kumekuwa na ukosefu wa kifaa cha *DNA* Zanzibar kwa kipindi kirefu, kifaa hicho kimkuwa kinahitajika sana kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa kesi za udhalilishaji. Kamati inaitaka Serikali kufanya juhud za makusudi kwa ajili ya ununuzi wa kifaa hicho muhimu muhimu ili kusaidia katika kufanya uchunguzi wa kesi za udhalilishaji na hatimae kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, kamati inaishauri Serikali kuwa, kesi za udhalilishaji ambazo ushahidi wake utakuwa unajitosheleza na hakuna ulazima wa kufanya uchunguzi wa kitaalamu zitolewe hukumu ili kupunguza mrundikano wa kesi za aina hiyo katika Mahakama zetu. Aidha, kamati inaitaka wizara kuendelea kuishajihisha jamii kuwa na muamko wa kufika Mahakamani kwa ajili ya kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji ili ziweze kusikilizwa na kutolewa hukumu.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa Idara ya Ustawi wa Jamii haipatiwi pesa za posho kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi wanaozika maiti zisizokuwa na wenyewe. Kamati imebaini kuwa wafanyakazi wanaozika maiti zisizokuwa na wenyewe wanafanya kazi hiyo katika mazingira magumu na wanahitaji kupatiwa posho ili kuwatia moyo. Aidha, kamati imebaini kuwa, maiti zimekuwa hazina sehemu nzuri ya kuhifadhiwa kutokana na kuwa chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ni kibovu na kichakavu hali inayopelekea uhifadhi mbaya wa maiti hizo.

Mhe. Spika, kamati inaitaka Serikali kuipatia Wizara ya Afya fedha za kukifanya matengenezo makubwa chumba cha kuhifadhia maiti kilichopo Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja kutokana na kuwa, chumba hicho ni kibovu, kimechakaa na hakiridhishi na ili maiti wanaopelekwa katika chumba hicho wahifadhiwe vizuri.

Mhe. Spika, kamati imegundua kuna ukosefu wa fedha katika kutekeleza majukumu ya Idara ya Maendeleo ya Vijana hasa fedha za miradi ya maendeleo, kumeipelekea idara kushindwa kutatua changamoto zinazoikabiliIdara katika utekelezaji wa majukumu yake. Kwa mfano, katika uendeshaji wa Mradi wa *Greenhouse* uliopo Tunguu kwa Unguja, idara imeshindwa kuwapatia vijana wa Tunguu umeme wa jua katika kuendeleza utekelezaji wa shughuli zao za kilimo. Aidha, kutokana na changamoto ya fedha idara imekwama kutekeleza mradi wa aina hiyo uliyopo Pemba eneo la Mbuzini.

Mhe. Spika, kamati inaitaka wizara kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Idara ya Maendeleo ya Vijana ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, kamati inaitaka Idara kuendelea kuwashajihisha vijana kushiriki katika sekta ya kilimo kwa sababu ina tija na itapunguza idadi ya vijana wanaozurura mitaani bila ya ajira, kwani kamati imebaini kuwa vijana bado hawajajiteza kwa wingi katika kuzichangamka fursa za kilimo.

Mhe. Spika, kamati inaitaka wizara ishirikiane na Wizara ya Kilimo pamoja na maafisa wao ili kwa pamoja wawasaidie vijana ambao wameitikia wito wa kujishughulisha na kilimo kupata taaluma bora za kilimo na hatimae kufanya kilimo ambacho kitawapatia tija zaidi.

Mhe. Spika, kwa upande wa Idara ya Wanawake na Watoto Kamati imetambua kuwa ufinyu wa ofisi unapelekea shughuli za ushauri nasaha na sheria kufanyika katika sehemu ambayo inakaliwa na watendaji wengine wa idara ambapo kwa kawaida sehemu ya kutolea ushauri nasaha na huduma za sheria inatakiwa iwe yenye utulivu na usiri na isiwe na maingiliano na watu wengine. Hivyo, kamati inaitaka wizara kuipatia idara sehemu maalum ya kutoa huduma ya ushauri nasaha na sheria ili wanawake na watoto wanaowasilisha malalamiko yao wapatiwe huduma katika sehemu hiyo maalum na ikiwa katika hali ya utulivu na usiri.

Mhe. Spika, kamati imebaini kukosekana kwa Maafisa wa Wilaya kwa Unguja na Pemba, kunadhorotesha utekelezaji wa Sheria Nam. 16 ya 2013 ya Uanzishwaji wa Baraza la Vijana, kwani sheria hiyo imetaja wazi kuwa, katika utekelezaji wake kwa ngazi ya Wilaya, Maafisa Wilaya ndio watakuwa makatibu wa Mabaraza ya Wilaya.

Mhe. Spika, kamati inaitaka wizara kuomba nafasi za uajiri za Maafisa Wilaya katika Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa sababu Sheria Nam. 16 ya mwaka 2013 ya Uanzishaji wa Baraza la Vijana imetaja wazi kuwa Maafisa Wilaya ndio watakuwa Makatibu wa Mabaraza ya Wilaya. Hivyo, kuzorotesha ajira zao kutakwamisha utekelezaji wa sheria hiyo.

### **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

Mhe. Spika, kamati katika ziara zake katika wizara hii iligundua changamoto mbali mbali ambazo zinakwamisha juhudzi za wizara katika kutekeleza malengo waliyojipangia.

Mhe. Spika, kamati imebaini kukosekana kwa hatimiliki kwa maeneo ya wizara na Taasisi za Serikali kukosa kupewa kipaumbele katika kupatiwa hatimiliki ni moja ya sababu zinazopelekea maeneo ya wizara kuendelea kuchukuliwa kama vile ilivyo katika eneo la Chuo cha Kiislamu Mazizini hali inayochangia kuibuka kwa migogoro ya ardhi katika jamii. Kutokana na hali hiyo, kamati inaishauri Serikali kuzipa kipaumbele taasisi zake katika kuzipatia hatimiliki ili kuepusha uvamizi wa maeneo yake pamoja na kuepusha migogoro inayojitokeza katika jamii.

Mhe. Spika, kamati ilipotembelea Skuli ya Dimani ilibaini kuwa miundombinu ya mafeni iliyoingizwa katika madarasa ya skuli hiyo yanahatarisha usalama wa wanafunzi kwa sababu dari ya skuli ipo chini sana ukilinganisha na kiwango kinachohitajika. Hivyo basi, kipelekea mafeni kuwa karibu na madawati ambayo wanafunzi wanakaa. Hivyo, kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua ya kuzikagua upya skuli mpya zilizojengwa ikiwemo Skuli ya Dimani ili kurekebisha kasoro mbali mbali inazojitokeza katika majengo ya skuli hizo na kuzinusuru.

Mhe. Spika, kamati imesikitishwa na kitendo cha Wizara ya Fedha cha kutoipatia fedha ipasavyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinazotokana na kodi ya bandari kwa vipindi vyta miaka mitatu mfulilizo tokeza kodi hiyo kuanza kukusanywa na Wizara ya Fedha. Kutokana na uingizwaji mbaya wa fedha za kodi ya bandari, ni dhahiri kuwa wizara itashindwa kufikia malengo yake ya kutatua tatizo la vikalio (madawati) maskulini.

Mhe. Spika, kamati inaitaka Wizara ya Fedha kuishirikisha ipasavyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kufahamu makusanyo halisi ya kodi hiyo ikiwa ni pamoja na kuipatia wizara mchanganuo halisi wa fedha za kodi zinazopatikana ili wizara ipange mipango yake ya matumizi kwa mujibu wa fedha zilizopo.

Mhe. Spika, kamati inaipongeza wizara kwa kuanzisha mfumo wa lishe katika maskuli, kwani mradi huu umepunguza sana utoro maskulini. Pamoja na pongezi hizo, kamati imebaini kuwa mradi wa lishe maskulini bado unakabiliwa na changamoto ya muitikio mdogo wa wazazi katika kufanikisha mradi huo. Hali hiyo imejitokeza katika Skuli ya Mfurumatonga ambapo baadhi ya wazazi wamekuwa wakitoa mashirikiano madogo katika kufanikisha mradi huo hasa katika suala la uchangiaji wa fedha za kuwalipa wapishi.

Mhe. Spika, kamati inashauri jamii kuunga mkono jitihada za Serikali na wafadhili za kuazisha mradi wa lishe maskulini kwa Unguja na Pemba ili mradi huo uendelee na wanafunzi wanufaikie. Kamati imepata matumaini makubwa kuwa kuendelea kwa mradi huo kutapelekeea wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao na kupunguza tatizo la utoro maskulini kama ilivyobainika kwa baadhi ya skuli ambazo mradi huo unaendelea.

Mhe. Spika, licha ya changamoto ambazo wizara inakabiliana nazo, kamati inatoa pongozi za pekee kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu Zanzibar kwa jitihada wanazozichukua za kuhakikisha kuwa wanawapatia wanafunzi mikopo ili waweze kuijendeleza na elimu ya juu.

Mhe. Spika, kwa vipindi tofauti tumeweza kusikia na kushuhudia malalamiko ya ucheleweshaji wa fedha za mikopo kwa wanafunzi. Hili ni tatizo la muda mrefu na hivyo kamati inatoa wito kwa taasisi nyengine za fedha zilizopo Zanzibar zianzishe utaratibu wa kutoa mikopo ya elimu ya juu kwa makundi ya jamii ili kupunguza vijana wengi kutegemea Bodi ya Mikopo pekee.

Mhe. Spika, miiongoni mwa taasisi ambazo kamati inapendekeza kuanzishwa kwa utaratibu huo ni Benki ya Watu wa Zanzibar tawi la Kiislamu ianzishe mashirikiano na vyuo vya ndani kwa kumkopessa mwanafunzi au mzee wa mwanafunzi ada na gharama za kujikimu. Aidha, kamati inapendekeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Zanzibar (ZSSF) uanzishe utaratibu wa kuwakopesha gharama za masomo wanafunzi wanaohitaji kuijendeleza masomo yao ambao hawana uwezo wa kujilipia na ni wanachama wa mfuko au wazee wa wanafunzi ni wanachama wa mfuko huo. Kufanya hivyo kutapelekeea wanafunzi wengi kupata fursa ya kuijendeleza na elimu ya juu.

Mhe. Spika, kamati katika kusimamia utekelezaji wa wizara hizi, imebaini juhudhi za wizara zote katika utekelezaji wa majukumu yake, licha ya kukabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti. Kamati imebaini kuwa, wizara ambazo inazimamia zinapatiwa bajeti ndogo na ambayo haiingizwi kama ilivyopitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na hivyo utekelezaji wa malengo waliyoipangia kwa asilimia kubwa ni kuitia michango ya washirika wa maendeleo. Iwapo Serikali imelenga kuimarisha afya nchini, kukuza ustawi wa jamii na kuwaendeleza wanachi wake kielimu ni lazima wizara hizi zipatiwe fedha zake za bajeti ipasavyo.

Mhe. Spika, kiujumla huo ndio muhtasari wa hotuba ya ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mujibu wa Kanuni ya 108(14) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2012.

Mhe. Spika, kamati inapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa watendaji wote wa wizara ambazo kamati inazisimamia kwa mashirikiano waliyoipatia kamati wakati ilipokuwa inatekeleza majukumu yake na kufanikisha kuandaa ripoti hii. Aidha, kamati inatoa shukrani kwa Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu na Watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwezesha kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo ahsanteni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika, baada ya ripoti hiyo ya kamati na mimi napenda kutoa mchango wangu mdogo katika Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, mchango wangu mimi nauelekeza kwanza kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusiana na wale walimu 159 ambao walikatwa mishahara yao kwa makosa.

Mhe. Spika, kucheleweshwa kwa walimu hawa kulipwa pesa zao toka mwaka 2012 mpaka leo 2015 kwa kweli kitendo hiki si kitendo cha kiungwana. Walimu wanafanya kazi ngumu, walimu wanakuwa katika mazingira magumu, mishahara yao ni haki yao na Wizara ya Elimu naipongeza kwamba imenawa kwa mujibu wa majibu ya Naibu Waziri aliyotoa asubuhi baada ya kupata malalamiko ya walimu, walilipeleka suala hili Wizara ya Nchi, (OR), Kazi na Utumishi wa Umma na wizara hiyo ikapeleka maelekezo kwamba, kwa mujibu wa vielelezo vya walimu hawa wanastahiki kulipwa mishahara yao ile ambayo iliyokatwa.

Mhe. Spika, tatizo hili liko Wizara ya Fedha, nilitarajia asubuhi kwa msuguano wa maswali yalivyo basi Waziri wa Fedha atasimama na aeleze chochote katika hili, lakini kwa bahati mbaya sana Waziri wa Fedha hakusema chochote na zigo hili limeangushiwa kwake. Ni matumaini yangu kwa mchango wangu huu Waziri wa Fedha atatuambia au atawaambia walimu hawa 159 pesa zao hizi watazipata muda gani.

Mhe. Spika, namuomba Waziri wa Fedha awathibitishie walimu kuwalipa pesa zao hizi ili wajisikie kwamba Serikali yao inawajali na wala haiwapuuzi. Baada ya mchango huo niende kwenye mchango wa madawati.

Mhe. Spika, Baraza lako baada ya kuona kwamba skuli mbali mbali zinakuwa na ukosefu mkubwa wa vikalio, walipitisha kwamba ipatikane kodi ya wasafiri wa Zanzibar, kila msafiri shilingi 1000 na fedha hizi ziingie moja kwa moja katika Mfuko wa Madawati. Lakini ni masikitiko makubwa sana kwamba fedha hizi hazina muingiliano wa kutosha baina ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kwa hivyo, tunaiomba Wizara ya Fedha kwa hatua kubwa sana itupe ufanuzi wa michango hii na ilitatue tatizo la madawati. Naamini kwamba pesa za wasafiri ni nydingi kwa sababu kila siku watu wanasaferi wengi, tatizo la madawati linaweza likamalizika kwa muda mfupi sana, kinachohitajika hapa ni uangalifu, uadilifu na uaminifu. Kupatikana kwa mambo matatu haya basi nina imani kwamba suala zima la upungufu wa madawati katika Kisiwa chetu cha Unguja na Pemba litamalizika kabisa.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huo nashukuru kwa Wajumbe wako kwa kunisikiliza. Ahsante sana Mheshimiwa naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na pia nakushukuru kama Mjumbe. Sasa taarifa za Serikali zijadiliwe pamoja na Ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Tumsikilize Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kunipa nafasi jioni hii ya leo kuweza kuchangia Wizara ya Uwezesaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwanza kabla sijaanza kusema nina jambo dogo sana ambalo linahusiana na jambo la Serikali. Tuna mifumo ambayo huwa tuna-*quote* kwa wenzetu hasa katika Mabunge na hasa Bunge la Jamhuri ya Muungano ambalo tuko karibu nalo hapa. Mara nydingi sana wanapopitisha ripoti za kamati za kudumu kwa Serikali Wajumbe na halkadhalika niseme labda Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anakuwa hatoi taarifa kwa mawaziri ili maafisa wao waje katika kupitishwa hili suala la ripoti za Serikali.

Mhe. Spika, inasikitisha sana leo namuona Naibu Katibu Mkuu mmoja tu wa Wizara ya Uwezesaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto yuko peke yake. Kwa kweli suala hili linasikitisha sana kwa sababu tunapokwenda kwenye kamati tunawakuta; tunamkuta Katibu, Naibu Katibu, Wakurugenzi na Waziri; wakipunguka Wajumbe hapo tunasema hiki kikao sio halali, lakini nashangaa leo hawa hawapo kabisa, hiki ni kitu cha zarau kusema kweli inasikitisha hasa. Kwa kweli ripoti hizi zinakuwa ni muhimu, wizara tatu, mtu mmoja anakuwa ana-includes na wizara zote Mheshimiwa?

Kwa kweli hili suala sote tuhurumiwe sisi Wajumbe kutokana na hali hii, nani atajibu, nani atamsaidia waziri, hili suala kwa kweli tumo katika hali ambayo hairidhishi na inasikitisha. Sasa naingia kwenye mchango, *message* imefika na tunaendelea. (*Makofî*)

Mhe. Spika, ninaanza na Wizara ya Afya. Kuna wakati mwengine sisi Wajumbe tukisema hatusemi labda kwa kumkomoa waziri, naibu au makatibu na halkadhalika. Wizara ya Afya mimi ninavyokwambia hivi sasa ramani

yake yote ninayo mkononi hapa, si asubuhi, si mchana na si jioni ninafika. Unajua lazima tukubaliane na Wizara ya Afya iende na wakati kwa sababu wizara hii ukilitaja neno la 'afya' tu basi tayari mazingira yake yaendane na afya.

Leo Mhe. Jaku Hashim Ayoub, alikuwa anasema masuala ya upungufu wa taa mimi siendi huko, kwa sababu taa ni kitu *very simple* tu, lakini uone hivyo kwamba ni vitu vya kweli. Lakini masikitiko yangu hata ile milango ya *theater* haina bawaba. Sasa ni vitu ambavyo nasema vidogo tu tuviachie mbali, tunaweza tukavisema kama kuchangia tu na kuvitia nyama ile wizara yenyewe.

Mhe. Spika, ripoti hii ina mwaka mzima tunapeleka madaktari mashamba kwa kufanya ufanisi zaidi, lakini inasikitisha hata nyumba inakosekana, mwaka mzima. Sasa naomba sana hili suala tunakuwa hatuko *serious* na haya mambo ya kusaidia. Kwa sababu katika wizara muhimu ni ya afya, huu ukweli tuuseme jamani Wajumbe, wizara muhimu sana katika nchi ni Wizara ya Afya, nikisikia bajeti yake basi nakuwa kidogo tumbo linaniuma, kwa sababu hii wizara si ya kuichezea na sio ya kuifanyia masihara. Mimi nafikiri wanajitahidi kadiri ya uwezo wao lakini ndio hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, leo naambiwa *ICU* ina mtendaji mmoja, kweli *ICU* chumba cha kumuokoa mtu kuwe na mtu mmoja. Mimi nimewahi kulazwa *ICU*, nilipotoka kwenye operesheni tu nikalazwa *ICU*, lakini mimi mwenyewe nimeona *nurse* mmoja na *orderly* mmoja, atoke kwangu mimi anihudumie na aende kwengine wakati huo tunapotoka katika mambo ya nuskaputi pale unakuwa hujitambui unaserebuka unavyotaka, hebu nambie mna vitanda vingapi mle atamzuia nani na amuache nani. Kwa kweli naomba sana hii idadi iondokane.

Halafu pale palikuwa na watu wana *experience* na wazuri wanaosaidia kazi. Lakini masikini ya Mungu wameondoshwa, jamani hizi ondosha ondosha ovyo ovyo kuna tatizo lake. *ICU* kuna watu ambao walikuwa ni watu *experienced* kabisa, ni watu hodari wanajua *ku-treat* vizuri, wanajua mgonjwa huyu akiambiwa apate rufaa sehemu nyengine anakwenda naye vizuri, lakini leo kaondoshwa huyu na kesho kaondoshwa huyu, nayo hii inaleta zogo sana, kwa kweli si jambo zuri.

Mhe. Spika, Kitengo cha Sukari, humu Waheshimiwa wengi tuliwahi siku moja tukaenda tukapima sukari na sukari ni kitu ambacho ni hatari kubwa. Kwa kweli kitengo hiki bado hatujakipa haki yake, wana eneo ambalo ni finyu kweli, njia hiyo hiyo, tiba hapo hapo, kwa kweli naomba sana hili suala siku zote mimi nishasema sana mpaka mwisho nachoka. Naomba watafutiwe eneo lao nao wako tayari kuweza kuweka angalau na wao wakawa na sehemu ya kujidai, ikaambiwa hii sehemu ya *clinic* ya sukari. Hilo suala mpaka sasa hivi linakuwa na utata halipatikani jibu, mimi naomba sana liweze kupatikana jibu kwa haraka sana.

Mhe. Spika, niwasifu na wao wizara vile vile *Alhamdulillah*, ukweli tuwape haki yao. Mimi siku zote nasema Waheshimiwa sasa msikimbilie nje kwenda kutibiwa, leo tunapasua kichwa hapa hapa *Alhamdulillah*, jengo zuri, uti wa mgongo unatibiwa hapa hapa. Mbona unainuka Mhe. Spika, wewe huendi nje kutibiwa nasema mfano tu. Waheshimiwa sasa hivi tunayo hospitali yetu pale ya kutibiwa vizuri tu na watu wanaponia.

Kuna mama mmoja nilimuona ilikuwa uti wa mgongo unampa shida, katibiwa pale na katoka vizuri, namuuliza vipi? Anasema *Alhamdulillah* nashukuru, Hospitali ya Mnazi Mmoja bwana sasa hivi rufaa imekubalika. Kwa hivyo, nalo hili tuliseme ukweli ulivyo, haki yao tuwape ni makosa madogo madogo tu, kama karo sijui chafu, siui hamna *dettol* ya kusafishia, hayo mambo madogo madogo tu. Lakini kwa asilimia kubwa wanajitahidi na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awajaalie.

Mhe. Spika, ukienda bohari kuu sasa hivi dawa nyingi lakini niseme labda *department* inachelewa kupeleka ripoti haraka haraka zilivyopokewa zile dawa, wanakuwa wanachelewa. Hilo mimi nakubaliana nalo lakini dawa borahi ziko nyingi kabisa chini ya usimamizi wa Naibu Waziri akiongozana na waziri wake *Alhamdulillah*. Mwenyezi Mungu awabariki ili Mnazi Mmoja iendelee kuwa vizuri.

Mhe. Spika, niende kwenye macho. Jengo hilo ni historia linakuwa mdomoni, linasemwa wee kila bajeti mimi nasema tu, sasa hivi kule kwenye macho kwa kweli tushazidi sana. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Waziri namuomba sana ye ye mtundu wa kutafuta *sponsor* jitahidi sana. Juzi nilimsifu kutohana na ustadi wake wa kueleza pale, sio *specialist* lakini ameeleza vizuri sana utasema kama ni *specialist* mwenyewe, kumbe umepelekwa China kwenda kusoma nasema *Alhamdulillah*. Sasa na manaibu wengine wapewe vitu kama hivyo wakasomeshwe kwanza katika *department* zao waweze kutupa maneno mazuri sana.

Lakini nakuomba sana hili jengo linachukua muda mwangi, limetuokoa sana kwa kufanya operesheni, sasa watu wengine operesheni tunapeleka Dar es Salaam kwa sababu ni sehemu ndogo hairidhishi. Jicho si mchezo, jicho ndio kuona dunia, leo ukilifanya mchezo kidogo tu utaona nini? Huoni kitu, watu wengine wanavaa miwani hapa na wanashindwa kuona.

Halafu vile vitu vyake havitakiwi kuchezewa kuhamishwa hapa na pale vinaharibika, *vina-expire*, tutakula hasara. Kwa hivyo, naomba sana hili suala liweze kuchangamkiwa ili kufanikisha malengo.

Mhe. Spika, kuna hili suala la mashine ya *DNA*. Kwa kweli inanisikitisha sana, namwambia Mhe. Makamu wa Pili kama upo uwerekano wa kupewa uwaziri *temporary* basi mimi naomba anipe uwaziri *temporary* mashine naileta. Kwa sababu nina uwezo wa kuleta mashine ya *DNA*, *DNA* kweli ishindwe kuletwa? Nipe asubuhi na mchana chukua uwaziri wako, kamwambie Dr. Ali Mohammed Shein. *DNA* nishasema mara ngapi katika wizara hii, watoto wanadhalilishwa, *ina-increase number* sasa hivi watu kwa uhalisia kwa nini, sasa nampa hivyo vitu aone kama hajanipa uwaziri.

Mhe. Spika, kama mimi ningekuwa waziri tuna matajiri wangapi hapa Zanzibar, nakwenda kwa Bakharesa, nakwenda kwa Turky, nakwenda kwa *JK Enterprise* pale kwa Khamis Para, nakwenda kwa Mhe. Raza, nakwenda kwa Mhe. Jaku na nakwenda katika mabenki, yote nawaita sijapata mashine hii, nipe uwaziri uone. Sio utani Mheshimiwa inasikitisha, naileta mimi mashine juu halitui, kwani kiasi gani hatuna, hata pesa yenye haitimii kwenye mkono, kwani kiasi gani mashine hii ikosekane. Hivi kweli jamani, Serikali ishindwe, waziri wahusika washindwe ah! Mhehsimiwa nasikitika.

Mhe. Spika, kama kuna tatizo la Katiba, nilimwambia Mhe. Waziri tugeuzeni Katiba mtupe uwaziri wa *temporary*, hiki kitu kifanikishwe kwa sababu ni kitu muhimu, watoto wanadhalilishwa.

Nataka nisema na upande wa pili wa polisi na wao wana-*delay*, tunaambiwa mkono kwa mkono, itakuwa mguu kwa mguu sasa, hata polisi wana-*delay* katika kutafuta ripoti au kupeleka kila siku wanalishwa.

Halafu kuna mtindo mmoja, kuna mmoja anasema mimi aliyenifanya mwanangu, ndugu yangu naogopa familia, haa, hujampiga risasi tu unangoja nini, wewe ndugu yako mwenyewe akakudhalilishie mwanaao halafu unasema naogopa familia, inasikitisha.

Mhe. Spika, juzi mimi nimekuaga nimepeleka mgonjwa, unajua mgonjwa gani, kitoto kidogo kimeharibiwa, hatuko *serious* Serikali, kitoto kidogo hakina hamu, kikivaa kisuruali cha kiume utasema mwanamme lakini kumbe mwanamke, hata hakina hamu jamaa kakiharibu, kitoto kidogo hatuko *serious* na jambo hili.

Mwenzetu yule pale Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete alivyopiga kelele za Albino kenda Ulaya na mimi nitashindwa kwenda Ulaya kutafuta *sponsor*, sishindwi, ni ujanja tu, ni mbinu za ujanja jamani kuvaas suti ndio uwaziri, kuvaas suti ndio uongozi, hapana ni ujanja. Ukiwa mjanja ndio unaweza kufanya jambo la kitaifa na ukaleta neema.

Mhe. Spika, meli hapa watu walivyokuwa wanazama kwa meli tulifanya mchango haraka sana, meli tunaambiwa hiyo hapo keshokutwa inakuja mwezi wa sita, meli imenunuliwa kwa mabilioni ya fedha, itakuwaje kimashine cha *DNA!* Mhehsimiwa, inasikitisha sana. Sio kitu cha mchezo.

Mhe. Spika, nimeona hapa tunaambiwa Mhe. Rais kaitisha mkutano wa kitaifa kwa kutaka kutokomeza, halitokomezi ng'oo, sikwambieni uongo kwa sababu hatukuwa *serious* naye na hatukumuunga mkono, mwachie anitie mimi kwenye kamati aone kama haitokuwa inawezekana, sio mchezo hili suala.

Kizimkazi kuna mtwana mmoja kamuharibu mtoto, kesi mpaka leo hajenda, vitoto vidogo Mhe. Spika, vinaharibiwa haki ya Mungu nakwambia, vitoto vidogo na vijanadume, hatuna amani, hebu leo tukasirike Baraza zima, nataka nione hapa leo asiyeinua mkono wananchi msiwape kura, hebu tuoneshe *seriousness*, linatula suala hili, nani asiyekuwa na mtoto katika nyinyi hapa, nani aliyekuwa hajapiga watu wanaona nje wanasema huyu jamaa kumbe hana uchungu na waototo, hili suala linaumiza sana, linaniuma sana kwa sababu nimeona na nimelia machozi.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya naishukuru sana imenisaidia wametoa fedha haraka sana ili yule mtoto asafirishwe, hebu *imagine* wewe yule mtoto anasafirishwa anatolewa hapa kashindikana anapelekwa Dar es Salaam? Sisi Serikali tunafanya mchezo, huu ukweli tuuseme jamani. (*Makofii*)

Waheshimiwa, hali ya hatari hiyo, hili suala nakwambia linasikitisha sana. Mimi ninachotaka kumwambia Mhe. Rais, asitazame kwenye bangokitita aende *field*, hivi kweli wanakwenda kumdanganya kila siku kwenye bangokitita tu kupoteza pesa nyingi, *three hundred millions per day*, tungefanya mangapi hayo Mhe. Spika, wizara ngapi, hebu *include* na hizo. Mhe. Spika, naomba sana hili suala nimelisema sana kwa uchungu mpaka machozi yanantoka si mbwembwe *just* naumia, ili tuweze kudhibiti na kudhibiti inawezekana.

Naomba sana Mhe. Spika, tunaambiwa kuwa Serikali hatuko *serious* na mambo kama haya na sisi ndio tutahukumiwa tumeshika msahafu pale kwa masuala haya ya kuwa tutalinda, tutatetea na tutatekeleza na hatimae leo tukaa tunafanya mambo ya kitoto, haiwezekani mimi sitokubalina nao kabisa kwa hili, hapana. Mhe. Makamu wa Rais, narudia tena na wala sio dhambi nipe uwaziri wa *temporary* nakuletea mashine wala usiwe na wasi wasi wowote.

Mhe. Spika, nikiendelea na suala elimu, Mhe. Spika, nafikiri sasa hivi tuseme ukweli, sijui ile awamu ya zamani tunapotekeleza wajibu ya kujenga zile skuli halafu baadae mkatumalizia, kama utaratibu ule upo, naomba sana mtusaidie kwa sababu tayari maskuli tumeshajenga hasa Jimbo la Kitope kule sehemu nyingi maskuli tumeshajenga tunaomba ule utaratibu muweze kutusaidia.

Lakini nikupongezeni sana baada ya kuwashirikisha hawa ZSSF na wao kwa kauli humu mnavyotwambia wamekubali lakini lini na watoto wanataka kusoma haraka sana ili tupate watoto wenye taaluma nzuri. Mhe. Spika, mimi naliunga mkono tusiletewe tena kwenye bajeti, tuambiwe utekelezaji umeanza. Hizi ripoti kila siku tuko mbioni, tuko mbioni itakuwa mpaka lini hizi mbio, hazifiki, hata *marathon* zinafika muda wake.

Naomba sana suala hili tuliangalie kwa upana kabisa, ni vitu ambavyo ni muhimu hatuko *serious* navyo nasema ukweli. Kwa hivyo, mimi naomba hili tunakubaliana nalo.

Mhe. Spika, tuseme ukweli hapa hakuna Mheshimiwa hata mmoja asiekuwa na watoto wa kuweza kusomeshwa. Lakini naamini hebu na sisi Waheshimiwa angalau mtupatia sadaka hiyo, kwa sababu utakuta mtoto ambaye mpaka leo anashindwa kusomeshwa mshahara wenye kwani mkubwa, tatizo lenyewe mshahara wenye hamtupi mkubwa hapa, hili kweli tukubaliane nalo mshahara wenye shilingi 500 jimbo la kaka, mtoto anataka kusomeshwa na mtoto wa kaka anataka kusomeshwa.

Kwa hiyo, mimi naomba na hili mtupe kipaumbele msione tabu, hapa na nyinyi ndio pa mavuno kwa Waheshimiwa na sisi kama huna mwana utapata ndungu, kama huna ndugu utapata mwananchi wa jimboni kwako, wako wengi tunashindwa kuwasaidia kwa sababu hatuna sauti. Tunaomba sana Mhe. Spika, Bodi itusikilize na itusaidie ili watoto wetu kwa sababu hatufanya kuwa ni mtoto tu ila tutafanya na mwananchi kuweza kumleta pale kuweza kusadikisha.

Mhe. Spika, niingie katika suala la wanawake hasa katika suala la Mikopo.

**Mhe. Spika:** Una dakika tano, malizia mchango wako.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, zinanitosha

Mhe. Spika, mimi kwa kweli mikopo naisikia, siifahamu mikopo ikoje na sijui utaratibu wake ukoje. Kwa sababu kama kuomba mimi nimeshaomba mikopo kwa kupitia kwa wanawake na kuwapelekea kina mama kwenye majimbo, lakini mpaka leo suaona ziara wala suaona kuulizwa. Sasa ina maana gani mikopo hii, ina maana mikopo hii inakuwa kisiri siri. Naomba sana na sisi tushirikishwe kwenye mikopo na tuambiwe taaluma zake zikoje na mimi nasema siku zote ikiwa mnataka kweli kuwasaidia wananchi tuanzie kwa Masheha, Wilaya na Mikoa na sisi tuwe tunashirikishwa.

Kwa hivyo, naomba sana katika suala hili la mikopo bado wananchi wetu wanahangaika hususani vijana. Hawa vijana ajira hawana. Lakini mimi nimeshangaa humu nimeambiwa kuwa vijana wako Tunguu, vijana wenywewe pengine utawakuta sio wengi na sio Tunguu tu, twende kwenye majimbo na kule tukahamashe, wanatakiwa waende kule wakapande maua na mboga mboga, sehemu za majimbo tunazo lakini hawa maafsa wanafanyakazi gani.

Naomba sana Mhe. Spika, ili nisipinge muda wako nikatoka tena chozi, naomba niunge mkono hasa ripoti ya Mwenyekiti wangu. Naomba sana Mhe. Spika, niunge mkono kwa asilimia mia kwa mia, nakushukuruni sana kwa utuliu wenu Wajumbe walioniskiliza na hili suala la watoto kubakwa naombeni sana Mheshimiwa, Mungu atubariki, lakini kila mtu akiondoka hapa awe na nia moja kusema analani kwa hili jambo linalofanywa katika nchi yetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali:** Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi sote kumshukuru Mwenyekiti Mungu alietupa pumzi kwa muda wote huu tuliokuwemo humu ndani na kutupa afya na nashukuru kwa dhati kabisa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, kwanza nizipongeze hotuba za mawaziri na wenyeviti wa Kamati hapa walioweza kutuwasilishia hotuba hii.

Mhe. Spika, humu ndani tumekuja kwa niaba ya wananchi na sisi sote tulikuwa huko kwenye *grassroots* na Mwenyekiti Mungu akatujaalia kufika hapa na kufika hapa kwa upande wangu mimi nisingelikia kama si nguvu za wenzenetu kutoka *grassroots* mpaka hapo nilipofika nikasimama mbele ya Baraza hili la Wawakilishi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini.

Mhe. Spika, mimi nianze kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Ali Mohd Shein kwa hekima zake busara zake na usikivu wake na nasema hivyo wa sababu zangu za kusema. Mhe. Spika, matokeo yaliyotokea katika wiki hii kwa Wizara ya Afya kupitia *ZBC* matokeo ambayo kwa kweli mimi na wezangu yamehuzunisha, nafikiri jamii nzima kwa mwenye kufahamu.

Kwa kweli Mhe. Spika, kitendo hiki cha Hospitali ya Mmazi Mmoja, maana yake kwa ufahamu wetu Hospitali yoyote inatakiwa kuwa iwe safi kuliko hata majumbani mwetu tunapokaa kwa sababu wanatibiwa wagonjwa ambao wamepata mitihani wa Mungu, hakuna mtu anaependa kwenda Hospitali, lakini ni mitihani ya Mungu ndio wanakwenda.

Mhe. Spika, *ZBC* wameweka historia, lakini vile vile naipongeza Serikali hii ya awamu ya saba kwa kusimamia kidete kuona yale mambo ambayo yana maovu yake au yana ukweli wake yameanza kuonyesha Demokrasia mpya. Mimi Mhe. Spika, nampongeza sana Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Idd kwa kuona kwamba uchungu ule na hakuweza kustahamili na akaweza kufika Hospitali pale na kuona hali halisi. Hiyo peke yake inatosha

kuonesha kwamba Serikali hii imejidhatiti pamoja na vyombo vyake kuonesha vitu ambavyo vimewagusa wananchi na vimegusa jamii na tumefika hapa kwa sababu ya jamii.

Mhe. Spika, nasema hayo kwa sababu awamu wa sita Mhe. Spika, kitendo kimoja kilitokea Hospitali ya Mnazi Mmoja watoto kutembelewa na mende kwenye magodoro yao, matokeo yake Serikali ya awamu wa sita ikabidi iwasimamishe waandishi, ikabidi viongozi waingilie na waandishi wakapata matatizo makubwa. Sasa nasema kwamba Serikali ya Dr. Shein pamoja na Makamu wa Pili wameonesha ule uzalendo wa kuwajali wananchi.

Mhe. Spika, changamoto ziko nyingi na Serikali yetu imefanya mambo mengi sana; huduma za maji, barabara, uvuvi, kilimo, umeme na afya na hii yote inatokana na umasikini. Lakini Mhe. Spika, vitu kama hivi kusaidiana sisi wenyewe Wazanzibari, kwa sababu kitendo cha wagonjwa wamo ndani maana yake mtu akizungumza utasikia kunanuka, anaweka kitambaa puani.

Mhe. Spika, mimi nilishindwa kula siku mbili kwa jambo ambalo limehudhunisha sana kwa sababu pale wote waliokuwepo ni masikini wa Mungu. Kweli tuna hali mbaya za uchumi lakini sio kiasi kile, kwa sababu watendaji wetu hakuna mmoja aliekuwepo pale, wale wote wanatoka shamba, yaani wanatoka kwenye *grassroots*. Kwa hivyo, yale maradhi waliyokuwa nayo yamezidi na umasikini waliokuwa nao.

Sasa Mhe. Spika, natoa ushauri nasema hali yetu kwamba mambo haya yanapotokea sisi Wazanzibari tupo tushirikishwe katika hali hiyo na sio Serikali, Serikali maana yake ni sisi; wafanyabiashara na wananchi, kama kuna jambo tuitane jamani, ee, kuna hili suala la karo kunahitajika omo na vifaa, tuko tayari kusaidia kwa sababu tuna uchungu na nchi na lile suala ni letu sisi.

Sasa Mhe. Spika, mimi nasema kwamba Wizara ya Afya ni sehemu kubwa na bajeti yake kinachoombewa hakifiki kiwango wanachokitaka, nilikuwa nashauri uongozi mzima wa Wizara ya Afya wakae kitako ili waone tatizo liko wapi tusaidiane katika kuondosha mazingira magumu.

Sasa Mhe. Spika, mimi naomba Vyombo vya Bahari na kwa sababu Serikali imetoa tamko kwamba waendelee kwenda sehemu nyingi ili isaidie jamii.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ningeliomba kwa heshima na taadhima ningelimuomba Mhe. Waziri wa Afya kwa heshima, namstahi mzee wangu angeliomba radhi kwa wananchi katika Baraza hili la Wawakilishi ili waone wananchi na Baraza hili limegusa na waziri mwenyewe imemgusa, kwa sababu kitendo kilichotekea pale Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ndie aliyeonekana na kwa sababu ni kitendo kilichohuzunisha, Mhe. Waziri wa Afya, angeliomba radhi wale wagonjwa familia yao kwa matokea yale halafu tukasema *what is next*.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kuna vitu vingi na yote hii ni umasikini. Lakini kuna vitu vyengine *which are not compromised* hasa katika suala la afya, maana yake wagonjwa wamo ndani na wanazungumza kunanuka kwenye *ZBC Inalillah waina Ilah Rajiun*.

Kwa kweli Mhe. Spika, hili jambo tulitzame, mimi naomba Wizara ya Afya nikao tayari kuwahamasisha wafanyabiashara na nchi yoyote kusaidia kutatua matatizo haya ambayo yanaweza kujitokeza na hasa kwa sababu wizara.

Mhe. Spika, nikija katika upande wa pili wa Wizara ya Elimu, kama nilivyosema Wizara ya Elimu vile vile watoto wetu bajeti yao na hali ya fedha, maana yake Mhe. Spika, bajeti tunaweza kusema milioni mia nane, lakini bajeti mpaka inamaliza mnategemea kupata milioni mia mbili, haya yanatokana na makusanyo ya pesa. Kwa hivyo, Waziri wa Fedha anakaa anatizama kilichokusanywa ndio anachokitoa. Sasa Mhe. Spika, hivi vitu lazima tuwe na mtazamo wa upana kabisa na kutokana na mazingira.

Mhe. Spika, umeona kuona sehemu kumeathirika Zanzibar huu ndio ukweli, yaani kumeathirika Zanzibar na Bara baada ya wahisani kuzuia pesa, huu ndio ukweli. Hatukujandaa tunafanya nini, kipindi hichi tumeathirika na tulikuwa tunasoma kwenye vyombo vya habari, wenzetu wahisani pesa zile wamezuia matokeo yake *4.5 percent* za Zanzibar na kule imekuwa hai hoi, tukaanza kujibana wenyewe na koti letu.

Sasa vitu kama hivi lazima tuwe waangalifu katika suala nyeti kabisa na Mhe. Spika, kama hali hii inatokea mimi ningeshauri vile vile suala la usafiri kuwe kunapunguzwa safari ambazo hazina tija, maana yake leo Mhe. Spika, mtendaji tu akiondoka kama huna milioni name huwezi kusafiri, huu ndio ukweli.

Jengine Mhe. Spika, lile karo milioni moja haifiki pale katika Wizara ya Afya. Sasa ninachotaka kusema kwamba vitu hivi kwa Wizara ya Elimu alikuja Muhisani kutoka Dubai kwa bahati alisoma Skuli ya Chake Mfikiwa Furaha, namuheshimu sana Mwalim Saleh Mwakilishi wa Jimbo la Wawi, tena nataja jina alikuja mama Lutfia bin Brak, yeze ni mzaliwa wa Chake Mfikiwa na kwa bahati tulikwenda Pemba tulikwenda kukagua maeneo ya Skuli kwa bahati mama yule pamoja na Ahmed Said bin Brak tukatengeneza madarasa manne pamoja na skuli moja nzima. Nikapewa kazi mimi ya kupeleka madeski na viti na nikapeleka *ma-deks* 200 na viti 200 kutoka Malaysia.

Mhe. Spika, miezi mitatu iliyopita wenzangu hawa walikuja Zanzibar wakanambia Mohamedraza basi twende Pemba, nikenda nao Pemba kwa sababu ya kusaidia kwa pamoja, ni wazaliwa lakini Mwenyezi Mungu amewajaalia. Tulipokwenda Pemba tulitembea Chake Mfikiwa katika Skuli. Mhe. Spika, kama ningelikuwa najua hali halisi ya pale *Wallah* nisingewapeleka na wala nisingekwenda Mhe. Spika, viti na *ma-deks* vyote vilikuwa havipo, nilipowauliza walimu haya *ma-desks* yako wapi, ananambia unajua Raza hapa hakuna ulinzi, kwa hivyo, viti na meza zote ziko barabarani.

Mhe. Spika, kweli limenisononesha sana, naipenda nchi yangu, yaani anazunguza mwalimu kama hivi vitu vimetolewa viko barabarani, viko mitaani yaani Mhe. Spika, nina uchungu kwa sababu wale ni watoto wetu wanaosoma, nikamuenda Mwalimu Saleh, nikamfata Naibu Waziri wa Elimu, lakini sijasita hapa Mhe. Spika, kwa sababu ya uchungu nilifata Kamati nzima nikawaambia jamani nendeni mukafulize na walipokwenda kule wakaambiwa maneno hayo hayo "hapakuwa na ulinzi, kwa hivyo, hizi meza na viti vyachukuliwa".

Sasa Mhe. Spika, ikiwa leo tumehamasika, mimi nimehasika na wenzangu tumekwenda Pemba yakatolewa *ma-desks* na meza halafu yasionekane hata moja, kwa kweli Mhe. Spika, mimi nataka kusema Wazanzibari pamoja na viongozi wote lazima tuwe na uchungu na hali halisi. Nashukuru Mhe. Naibu Waziri wa Elimu akalifuatilia na akalikuta hilo, namshukuru Mheshimwia Mwalimu Saleh ambaye namstahi sana na namuheshimu sana, kwanza ni mwalimu na kwa kweli alisononeka sana Mwalimu Saleh Mwakilishi wa Jimbo la Wawi na hakuamini, nikaifuata Kamati ya Baraza la Wawakilishi ambaye Mhe. Mgeni Hassan Juma huyu hapa kwa bahati Mwenyezi Mungu kampa pumzi, uhai na ampe afya ya kuendelea akawa shahidi na kamati yake kwenda Chake Mfikiwa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nataka kusema jamani hii Zanzibar ni yetu, sasa lazima tuwe na uchungu wakati wenzetu wanapokuja kutoa misaada ile misaada inathaminiwa. Kwa bahati mbaya Mhe. Spika, nilipata tabu sana, nafikiri na kosa nilolifanya sikuenda mwanzo peke yangu nikenda nikatizama. *I had a confidence.* Vipi alisema bibi huyu Lutfia kwamba Mohamedraza nataka kuendeleza mambo mengine makubwa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ngeliomba watendaji na wananchi kwamba hili jambo letu, tumekuwa hapa kwa maendeleo Mhe. Spika, *we are all in transit.* Kwa hivyo, natoa wito, hizi kamati zinapotoa hali halisi lazima tuwe na *commitment*, wizara zinazohusika ziwe na *commitment*.

Mhe. Spika, tumekuwa na harambee nyingi tunazifanya, tulifanya harambee ya uwezashaji kuondosha umasikini kwa wananchi wetu na tulifanikiwa na mimi nilikuwa Mjumbe mmoja humu, tulikusanya mabilioni Mhe. Spika, kwa kusaidia kuondosha umasikini kwa wananchi wa Unguja na Pemba katika kuwapa mtaji katika Kamati ya Uweshaji Mhe. Mwalimu Haroun ndie alikuwa Mwenyekiti; nilikuwa mimi na Said Bakhresa, alikuwa Mhe. Ramadhan Dau, tulikusanya na tulishirikiana na Mhe. Mahmoud.

Sasa hivi vitu vinawezekana, hebu tuambieni jamani hapa tumekwama, Serikali ni yetu kwamba hapa tunahitajia mtaro milioni tano, hapa tunahitajia madawa. Sasa Mhe. Spika, hili jambo linawezekana kama tunaweza kufanya mambo mengi, kwa nini mambo haya tushindwe.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nishukuru na niendelee kuwaambia wenzangu kwamba jamani kwamba tunaringa na pumzi za Mwenyezi Mungu, vitu ambavyo vitakuja kwa ushindani havitusaidii.

Mhe. Spika, kwa kumalizia marehemu babu yangu aliniambia mjukuu wangu wenzako wakikuamini na wakikupa nafasi basi muogope sana Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hizi dhamana tunazozichukuwa na kuleta vitu ambavyo havisaidii ubabe, Mhe. Spika, bora babu yangu alivyonambia ule muhogo au sembe lakini ukimaliza muda wako wa uongozi mwanangu Raza ukitoka uwe unaheshimika, heshima yako inakuwepo pale pale. Lakini leo unaweza ukamaliza muda, mmh, balaa, kwa nini.

Sasa Mhe. Spika, hivi vitu havisaidii, yaani kuleta vitu ambavyo vitaleta ushindani tu havisaidii.

Mhe. Spika, mimi nishukuru wenzangu wamechangia, lakini ningeliomba wizara zinazohusika, mawaziri wanaohusika na manaibu waziri wanaohusika tupo sisi wafanyabiashara na wananchi tuko tayari kusaidia kwa hali na mali nchi yetu bila ya kujali rangi, kabilia na dini.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

**Mhe. Spika:** Nakushukuru sana Mhe. Mohamedraza Hassanali, kwa mchango huo na nawashukuru Wajumbe wote kwa kazi nzuri tulioifanya kuanzia asubuhi na sasa naomba niakhirishe kikao hiki hadi kesho tarehe 19/3/2015 saa 3:00 asubuhi.

(*Saa 1:43 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 19/03/2015 saa 3:00 asubuhi*)